ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kateuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 03 Julai, 2012

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuanza maswali, kama kawaida tunao wageni leo hii katika ukumbi wetu pale juu. Wageni waliokuwepo leo ni ujumbe wa serikali ya wanafunzi wa skuli ya msingi ya Rahaleo. Wageni hao ni jumla ya wanafunzi 35 pamoja na walimu wao wanne, tunawaomba wasimame ili muwasalimu Waheshimiwa Wajumbe. Karibuni sana walimu na wanafunzi ambao kwa pamoja mmekuja kama serikali ya wanafunzi na walimu wenu. Karibuni sana. Hao ndio wageni wetu kwa leo, Waheshimiwa Wajumbe nawashukuruni sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani, Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani, Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 175

Kupiga Marufuku Uvuvi Haramu

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:-

Shughuli za kuendesha maisha kwa wakaazi wa nchi yetu zinategemea ni maeneo gani wanaishi pamoja na rasilimali zinazopatikana kule. Serikali imepitisha sheria ya kutunza mazingira ya bahari kwa kupiga marufuku njia mbali mbali za uvuvi ambazo zinaaminika zinaharibu mazingira ya bahari. Ikiwa njia hizo zilizozoeleka na wakaazi wa maeneo husika kwa kuwapatia riziki zao na kwa kuwa zimepigwa marufuku.

Je, serikali imeweka shughuli gani mbadala ambazo zitawapatia riziki za halali wakaazi husika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kabla ya kujibu swali la Mhe. Mjumbe, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, serikali imeweka sheria nambari 7 ya mwaka 2010, ambayo inapiga marufuku njia mbali mbali za uvuvi ambazo zinaaminika zinaharibu mazingira ya bahari. Baadhi ya njia hizo ni ukokotaji wa nyavu za kuvulia unaopelekea uharibifu wa matumbawe ambayo ndio mazalio ya samaki, na utumiaji wa nyavu za macho madogo, zinazopelekea kuvuliwa samaki ambao ni wachanga na ni tegemeo kwa shughuli za uvuvi katika siku za usoni. Hivyo, marufuku iliyowekwa ina lengo la kudumisha na kuendeleza shughuli za uvuvi katika nchi yetu, na hasa kwa wakaazi wa nchi yetu, katika maeneo mbali mbali ya kandokando ya bahari, ili kuimarisha kipato chao kutokana na kazi au ajira hiyo ya uvuvi. Kwa kufahamu umuhimu wa marufuku hiyo, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, waliijadili na kuipitisha sheria hiyo yenye nia njema kwa wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 175 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, serikali haijaweka shughuli mbadala kwa wananchi wanaotumia njia mbali mbali za uvuvi zinazoaminika kuharibu mazingira. Hii ni kwa sababu Mhe. Spika, naomba ifahamike kuwa serikali haijapiga marufuku shughuli za uvuvi ambazo ni miongoni mwa kazi muhimu sana za kuwapatia riziki halali wananchi wa Zanzibar. Serikali inachokikataa ni matumizi ya zana na njia zote za uvuvi ambazo zinaaminika kuwa zinaharibu mazingira ya bahari, zikiwemo za kuharibu matumbawe na kuvua samaki wachanga.

Aidha, naomba kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba serikali itaendelea kuyakataa hayo kwa nguvu zake zote, kwa lengo la kuendeleza shughuli ya uvuvi katika visiwa vyetu na kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kupata riziki halali kupitia kazi za uvuvi. Naomba kuwanasihi wananchi wenye tabia ya kutumia njia za uvuvi zinazoharibu mazingira na badala yake watumie njia zinazokubalika, kwa mujibu wa sheria tuliyoipitisha katika Baraza hili, sambamba na maelekezo ya wataalamu. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais itaendelea kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuachana na uharibifu wa mazingira na faida ya kuyalinda na kuyatunza mazingira.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe.Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema serikali itaendelea kupiga marufuku uvuvi haramu.

Lakini Mhe. Waziri serikali imeshaweka kikwazo hicho, na je wananchi waliwapatia zana za uhakika zenye kuleta matumaini kwa wananchi hao na zisizoleta uharibifu wa mazingira ya baharini.
Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli nimesema kwamba serikali itaendelea na suala zima la kupiga marufuku uvuvi usiokuwa haramu. Naomba nimkumbushe Mhe. Kazija kwamba shughuli hii ilichukua muda mrefu sana, kwanza kwa kuwaelimisha wana vijiji mbalimbali ambao wanahusika na shughuli za uvuvi. Serikali ilifanya jitihada za makusudi kupitia miradi ya MACEMP na TASAF, kwa kuwapatia zana za uvuvi ambazo haziharibu mazingira.

Kwa kuanzia Mhe. Spika, siku za awali kabla ya sheria hii kutumika, wananchi walikuwa wakinyang'anywa nyavu zao na kupewa nyavu mbadala na walikuwa hawaadhibiwi, kwa nia ya kuwafanya wakubali na kuweza kuelimika kwamba kweli uvuvi haramu hauna tija. Kwa hivi sasa tunaamini kwamba wananchi wameelimika, toka mwaka 2010 hadi leo miaka imepita, na kwa hivi sasa serikali inawataka wenyewe wavuvi ambao tokea zamani walikuwa wakitumia zana za uvuvi kwa kujihudumia wao wenyewe, basi waendelee kujihudumia, lakini watumie zana ambazo haziharibu mazingira.

Mhe. Spika: Kabla ya kumruhusu Mhe. Panya Ali Abdalla aulize swali, kuna *statement* moja ndogo, Mhe. Waziri aliteleza. Alisema, kupiga marufuku uvuvi usiokuwa haramu. Lakini sahihi ni, kupiga marufuku uvuvi ulio haramu. Huo ndio unapigwa marufuku. Kwa hivyo, Hansard itengenezwe hapo. Mhe. Panya Ali Abdalla, swali la nyongeza.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa wavuvi wetu wako ambao walichomewa nyavu zao na mpaka muda huu hawajapewa, na wao ndio tegemeo lao la kupata rizki zao za kila siku.

Je, unawaambia nini wavuvi hao, na lini tuje katika wizara yako ili waweze kupata vifaa hivyo, ili waweze kujikimu kimaisha.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa kweli Wizara imechukua juhudi kubwa sana katika kuwahamisha kwenye uvuvi ambao wameuzowea na kujaribu kuwapeleka katika uvuvi wa bahari kuu. Kwa kweli Wizara imeshachukua hatua kubwa tu na tulianza kutoa boti kama 17 hivi ambazo zilitolewa kwa vikundi 22 katika vijiji au kanda ya Kaskazini. Yote ni moja katika juhudi za kuwashajihisha ili waondokane na huo uvuvi haramu. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe usiwe na wasi wasi na bado tunaendelea, tunaomba misaada ili tuhakikishe wavuvi wetu tunawapa misaada ili waende bahari kuu, ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la mwisho moja fupi kabisa. Mhe. Spika, kwanza nitoe pongezi kwa Wizara, kwa namna inavyojitahidi kuweka hifadhi nzuri ya mazingira kwa maslahi yetu na vizazi vyetu.

Lakini Mhe. Spika, kwa sababu Wizara imepiga marufuku utumiaji wa nyavu ambazo ni zenye kuharibu mazingira, za kukokota na zenye macho madogo, na kwa sababu kama swali mama linavyoeleza kuwa ule mradi wa uvuvi ndio mradi wa maisha kwa watu wanaoishi kule. Je, serikali haioni kuwa sasa ipo haja ya kuzungumza na wafanyabiashara, ili kuona kuwa wanaingiza nyavu ambazo ndizo zinazostahiki kutumika na zile ambazo hazistahiki kutumika basi zikazuiliwa zisiingie katika nchi. Lakini vile vile akashirikiana na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kwa kuwasaidia wavuvi wetu kujipanga vikundi na kupatiwa nyavu hizo zinazohitajika kwa kukopeshwa fedha na kufanya biashara yao, ili yale madhumuni ya serikali na maisha ya wananchi yaweze kwenda sambamba.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nakushukuru tena Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa kweli nakubaliana na Mhe. Mjumbe, na lengo na madhumuni hasa la mradi huu wa kuhifadhi mazingira ni kuwapunguzia umaskini watu ambao wanaishi katika ukanda wa pwani, ndio maana tukaunda kamati kwa kila shehia au kila kanda ili kuhakikisha kwamba tunawamilikisha ule uhifadhi wa ukanda ule wa bahari. Mapato yote yanayopatikana pale ni kwa ajili ya kijiji husika.

Kwa hivyo, niko pamoja na yeye na bado tunaendelea na juhudi hizo za kuhakikisha kwamba tunapata vifaa vya kuwapa wavuvi wetu, ili waondokane na uvuvi haramu. Tumeshafanya hivyo na kwa kweli tija imepatikana, nashukuru *Alhamdulillah.* Wameona vile jinsi ya kuhifadhi, baada ya muda wanaona tayari zile sehemu ambazo tumezihifadhi kwa kweli kumeongezeka idadi ya samaki.

Mhe. Spika, vile vile tumetoa njia mbadala ili kuhakikisha kwamba wavuvi wetu wanaondokana na uvuvi haramu, kwa sababu ukimwambia mtu aache hiki ni lazima awe na kitu cha kushika. Tumewapa baadhi ya vikundi boti pamoja na vifaa vyote kama nyavu na vyengineo. Lakini vile vile tumeanzisha elimu ya kufuga samaki nje ya bahari, sio nje kabisa lakini ni kwenye mikoko. Kwa kwali tumeona maendeleo mazuri sana, kama kule Pemba Pujini. Hivi sasa wameacha kazi za kwenda Dar es Salaama za biashara, wanashughulikia samaki, kwa sababu wameona kwamba wana tija.

Kwa hivyo, nahisi njia hii mbadala imewasaidia sana wakulima, na wamesema wako tayari kuachana na uvuvi haramu. Kwa hivyo, Mhe. Salim usiwe na wasi wasi bado juhudi zinaendelea za kuwashajihisha wavuvi na kuwapa vifaa ili waachane na ule uvuvi haramu na badala yake washughulikie uvuvi wa bahari kuu. Vile vile kuhakikisha kwamba wanafuga samaki ndani ya mikoko. Ahsante sana.

Nam. 90

Ukaguzi wa Watu Wanaoingia Uwanja wa Ndege Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mamlaka ya Anga Zanzibar imeanza kuwatoza Shs. 500/= watu wanaoingia na gari katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ili kudhibiti magari. Jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa na wananchi na wageni kutokana na usumbufu wanaoupata tangu kufanyika kwa mabadiliko hayo mwezi Mei mwaka huu.

(a) Ni sababu gani zinazopelekea abiria kukaguliwa zaidi ya mara 3 wakati wakiingia uwanjani hapo.

(b) Ni Sababu gani zinazopelekea kukaguliwa kwa gari kama imelipiwa ushuru wa Shs. 500/= wakati kabla ya kuingia inatakiwa kulipiwa.

(c) Kwa nini Mamlaka haijaweka utaratibu mzuri ambao utaepusha usumbufu kwa abiria wanaosafiri kupitia uwanja huo, wakati wenzetu wana viwanja vikubwa kuliko vyetu na hakuna usumbufu kama huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano -Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 90 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu wa utozwaji wa ada kwa vyombo vya moto vinavyoingia katika eneo la uwanja wa ndege wa Zanzibar ni wa kawaida duniani kote. Takriban viwanja vingi duniani vinafuata utaratibu kama huo, pato linalopatikana katika ukusanyaji huo linakuwa ni sehemu ya uendelezaji wa viwanja hivyo.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, ilichelewa kuanza kutekeleza zoezi hilo kutokana na miundombinu yake ilikuwa bado haijaridhisha, haikuwa kamilifu.

a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba abiria akiingia katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Aman Abeid Karume, anakaguliwa zaidi ya mara tatu. Sababu zake za msingi ni kama ifuatavyo;-

   i) Sehemu ya kwanza, mtu anapoingia anakaguliwa ili kuthibitisha kwamba yeye ni abiria au si abiria.

   ii) Sehemu ya pili, anathibitishwa kama anazo nyaraka zote zinazostahiki kwa msafiri ikiwemo *passport na ticket,* ili aweze kuruhusiwa kuingia katika sehemu ya tatu kwa ajili ya "*check-in counter*".

   iii) Sehemu ya tatu, anayokaguliwa abiria kama yuko salama na hajabeba vitu vitakavyopelekea athari katika safari yake ya ndege, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa vitu vyenye ncha kali yaani *Prohibited Items*. Hatua hizo zote za kufanya ukaguzi zinatokana na hali halisi ya udhibiti na usalama wa viwanja vya ndege duniani.

b) Sababu zinazopelekea kukaguliwa gari kama imelipiwa au laa, ni utaratibu wa kawaida wa kutaka kujiridhisha kuwa muhusika amefuata utaratibu wa kufanya malipo ya Shs. 500 anapoingia na gari yake.

c) Suala hili kwetu sisi tunalichukua kama ni changamoto, na azma yetu ni kuandaa mitambo mizuri ya kisasa itakayomuwezesha muingiaji katika uwanja wa ndege kuingia na kuchukua kadi yake na baadae kwenda kufanya malipo pasi na usumbufu wowote, kama vilivyo viwanja vyengine vya kimataifa duniani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri. Je, serikali inachukua hatua gani za kuweka usafi wa mazingira kwa sera ya uwanja wa ndege, ikiwemo maegesho ya magari na kuweka usafi katika uwanja wetu wa ndege, ili ufanane na viwanja vya ndege vya nchi nyengine.

Vile vile ni lini uwanja ule uliokuweko pale wa maegesho ya magari utamalizika kutiwa lami, au bado mtambo wa lami kama ulivyokuwa ukisema kuwa umeharibika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tuna matatizo ya usafi katika eneo la uwanja wa ndege. Lakini naamini kwamba Mhe. Mwakilishi atakuwa ni sehemu ya watu wanaoweza kuthibitisha kwamba kuna hatua kubwa sana katika kuimarisha usafi katika eneo la uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, azma yetu na malengo yetu ni kwamba fedha hizo zinazotozwa, pamoja na vyanzo vyengine vya fedha, itakuwa ni chachu ya kufanya mabadiliko hayo kuona kwamba uwanja wetu unaimarika, kutoka hatua uliopo na kwenda hatua kubwa zaidi ili kuridhisha watu wetu na wageni wanaokuja kutembelea. Lakini pia kuonesha taswira halisi ya usafi kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, swali la pili kuhusu lini tutatia lami katika eneo la kuegesha magari. Mhe. Spika, hatuwezi kusema ni siku gani tutafanya. Lakini jambo hili lipo katika mipango yetu na azma yetu ni kwamba kuona eneo lile linawekwa lami, ili kuweza kuimarisha usafi, lakini pia na huduma kwa wananchi wetu wanaokwenda kuegesha magari yao katika eneo lile. Lakini ni lini tutafanya hatuwezi kusema, lakini limo ndani ya mipango yetu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Ni kweli kwamba viwanja vingi vya ndege vya kimataifa huwa kunatolewa ada kwa ajili ya magari yanayoingia katika eneo hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba utaratibu wa utoaji wa chenji ya shilingi mia tano wakati magari yanapofika pale, unawachelewesha sana wenye magari kuingia ndani, jambo ambalo linaweza likasababisha abiria kukimbiwa na ndege. Je, wizara yake itafanya utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba mtu anayefika pale kulipa na kupewa chenji yake ili awahi usafiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika majibu mama tumeeleza kwamba mpango wetu ni kuona kwa kiasi gani tunaweza kuimarisha huduma ile, ili na sisi tuweze kufikia katika *standard* ile ya wenzetu ambayo mtu akifika, abonyeze, achukuwe kadi aende akalipe kule, halafu afanye huduma zake nyengine. Tunaamini kwamba tukifika huko, utaratibu huu uliopo wa sasa hivi watu kuchelewa utaondoka. Lakini kwa kipindi hiki, kabla ya kwenda huko tutahakikisha kwamba wakaaji wetu wa pale getini, wanafanya huduma ya kumrejeshea mtu chenji haraka iwezekanavyo, ili kujikinga na hii foleni inayopelekea usumbufu au ucheleweshaji wa watu wetu wanaotaka kuingia katika uwanja wa ndege.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, ni utaratibu gani unaotumika kwa Mheshimiwa anapoingia pale VIP kulipishwa shilingi 15,000/-. Kama hili suala lipo unachukua hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, sote ni mashahidi kwamba katika kipindi cha mwaka jana tulipitisha sheria nambari 8, iliyoipa mamlaka uwanja wa ndege wa kujiendesha kama mamlaka kamili. Miongoni mwa utaratibu wa kujiendesha kama mamlaka ni kuwa na vyanzo vyake vya fedha, na serikali ilifanya maamuzi ili kuweza kutoa huduma nzuri, katika maeneo yale ya kumbi za watu mashuhuri, likiwemo hili eneo la VIP. Kwa hivyo, iliamuliwa kwamba wakati umefika kuona viongozi na watu mashuhuri wanaokwenda kukaa katika kumbi zile kuanza kuchangia, ili kuhuisha na kuimarisha huduma zilizopo pale.

Kwa msingi huo, utaratibu tuliouelekeza katika serikali ni kwamba mtu anayekaa VIP achangie shilingi 20,000/- na tulifanya majadiliano kidogo katika serikali na hatimaye tukafikia maamuzi ya kuona kwamba shilingi 20,000/- ni bei halisi kama huduma za pale zitaimarika. Kwa utafiti zaidi wenzetu wa Tanzania Bara unapokwenda pale VIP, hasa kama unataka kusafiri, basi unatakiwa uchangie zaidi ya dola 40 kwa mtu mmoja kwa ajili ya kutumia huduma za VIP.

Kwa hivyo, kwa msingi huu na kwa kuzingatia kwamba bado tulikuwa hatuna eneo la *Business Lounge*, tukaona ili kuimarisha huduma kwa viongozi wetu, basi ni kuweka hiyo ada ya shilingi 20,000/- ili kuimarisha huduma nzuri zaidi kwa wasafiri na viongozi wetu watakaotumia ukumbi huo mashuhuri.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hilo swali la Mhe. Mjumbe alilouliza linahusu kuchajiwa chombo shilingi 15,000/- sio kukaa ndani VIP.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, miongoni mwa taratibu za kuona kwamba uwanja wetu unaimarika, ni kweli mamlaka ya uwanja wa ndege, imeona ni namna gani inaweza ikapunguza *crowd* katika lile eneo la VIP. Kwa sababu kulikuwa kuna matatizo, miongoni mwa viongozi waliokuwa wakisafiri eneo lile la VIP, walikuwa wakifanya ndio maegesho ya magari yao. Sasa watendaji wetu wa uwanja wa ndege wakaona ili tuweze kuondoa, kwa maana kwamba watu wanasafiri mtu anaiacha gari yake karibu wiki nzima, iwe uwanja wa ndege ndio wanamlindia gari yake. Ndipo walipoanzisha hiyo kodi ya shilingi 15,000/- unapoiegesha gari yako pale.

Mhe. Spika, utaratibu huu umetusaidia kwa sehemu kubwa sana, hivi sasa unaweza ukaenda katika eneo la VIP zaidi ya mtu anayesafiri basi hakuna gari nyengine ambayo imeegeshwa. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba utaratibu huu naomba sana watendaji wetu wa uwanja wa ndege wauendeleze, ili kuweza kuondoa ule msongamano wa magari yasiyo na sababu za msingi kuegeshwa pale. Eneo lile ni kwa mtu ambaye anasubiri huduma za usafiri, au anayesubiri huduma za kuja kupokelewa, lakini sio maegesho kama ilivyokuwa hapo kabla.

Kwa hivyo, kodi hii inatozwa kwa wale watu ambao wanataka kufanya maegesho katika uwanja wa ndege, hasa eneo lile la watu mashuhuri.

Nam. 184

Uchakavu wa Skuli ya Migombani

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Skuli ya Msingi ya Migombani ni miongoni mwa skuli kongwe hapa nchini, na sasa majengo yake yameanza kuharibika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyafanyia matengenezo majengo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 184 kama hivi ifuatavyo:

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Skuli ya Msingi ya Migombani ni moja katika Skuli zetu zilizoanzishwa zamani. Kutokana na ukongwe wake huo, unahitaji kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara, jambo ambalo wizara imekuwa ilikifanya. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara inakusudia kuendelea kuyafanyia matengenezo baadhi ya majengo ya Skuli ya Msingi ya Migombani katika mwaka wa fedha 2012/2013 kwa kadri ya uwezo wa fedha utakavyoruhusu. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri sana ambayo ni mafupi ya Mhe. Naibu Waziri yenye kutia moyo naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri katika kutembelea kwako umeona sehemu ya madirisha ya Skuli ya Migombani yalivyoharibika na kusababisha wahuni kuingia mule ndani. Kwa hivyo, ni lini skuli ile itapatiwa angalau kuzibwa yale madirisha, ili wananchi waweze kurudisha imani na serikali yao? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba mimi nilitembelea Skuli ya Migombani katika ziara zangu na tatizo la madirisha nimeliona Mhe. Spika, lakini naomba nifahamishe Mhe. Mwakilishi, kwamba katika Skuli ambayo tunaifanyia matengenezo ni Skuli yake ya Migombani.

Kwa mfano, tumefanya matengenezo makubwa kwa kushirikiana na Wawakilishi na Wabunge ambao walikuwepo, kama vile kulikuwa na matatizo ya bati kuvuja pale na tumeezeka, palikuwa na vyoo vichakavu na hivi sasa kuna vyoo 10 ambavyo vyote vinatumika tena ni visafi.

Kwa hivyo, tatizo liliopo ni hili la baadhi ya madirisha kuwa yana matatizo na sehemu ile kama tunavyojua ni sehemu ambayo wapo wala unga, hivyo wanaweza kuingia ndani na kuharibu vitu vyetu ambavyo vipo.

Mhe. Spika, kama nilivyomuahidi kwa mwaka huu wa bajeti yale matengenezo madogo yaliyobakia ya madirisha na rangi, tutahakikisha kwamba tunayamaliza. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa Mhe. Waziri kwenye maelezo yake yalionesha kuna upendeleo fulani wa kutengeneza hizi skuli. Je, *statement* hiyo ni kweli na kama si kweli kwa nini akasisitiza katika skuli zilizopata matengenezo ni ya Migombani.

(b) Kabla ya Wawakilishi kuripoti na Waheshimiwa Mawaziri kutembelea maskulini. Je, mimi namuuliza kile Kitengo cha Matengenezo ya Maskuli kipo na kina watu wangapi Unguja na Pemba na kina gari ngapi zinazoshughulikia suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama alinisikiliza vizuri Mhe. Mjumbe wakati nilipokuwa nikijibu swali mama. Kwa kweli nilisema Skuli hii ya Migombani ni ya zamani, kwa hivyo imekuwa ni chakavu na matengenezo ya mara kwa mara yanahitajika, ili kuifanya skuli ile iwe imara.

Sasa kama Mhe. Mjumbe anasema kwamba wizara ina upendeleo mimi simfahamu Mhe. Mjumbe anakusudia kusema kitu gani, kwa sababu hata Skuli yake ya Ziwani imefanyiwa marekebisho. Kwa hivyo, kama wizara ina upendeleo basi hata Jimbo la Ziwani inalipendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Kuhusu kitengo nadhani Mhe. Spika katika *session* hii ya Baraza lako tukufu nilimjibu Mhe. Mjumbe kama kitengo hiki kipo na kinafanya kazi. Kwa upande wa wajumbe wangapi wako Pemba na Unguja na hili ni suala la takwimu na kanuni zinatueleza kwamba suala la takwimu tulilete katika swali la msingi, ili tuweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, gari sidhani kama inataka takwimu, kwamba gari ngapi zipo, kwa hivyo, naomba anijibu kuhusu gari ngapi zipo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, gari za nini.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, katika swali langu nilimuuliza hapa kwamba hiki kitengo kina gari ngapi Unguja na Pemba, na wala sidhani kama swali la kuuliza gari litahitaji takwimu. Kwa hivyo, namuomba anijibu swali hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, bado nasema kwamba gari ni takwimu na nitamletea kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri hataki abahatishe ndio kawaida yake hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kuniona ukanipa nafasi hii naomba nimuulize swali moja Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Skuli ya Mkwajuni Msingi inafanana kimazingira kama Skuli ya Migombani kwa uzee wake wa muda mrefu na siku nyingi. Hivi ni lini skuli hii nayo itapata jicho la huruma la wizara yako kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo, ahsante.

Mhe. Spika: Hivi yakizuka maskuli ya kila jimbo itakuwaje. Mhe. Mjumbe tafuta utaratibu wa kuuliza swali la msingi. Tuendelee. *(Makofi)*

Nam. 134

Uhaba wa Vituo vya Afya Mkoa wa Mjini Magharibi

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja imekuwa ikipokea wagonjwa wengi, hasa kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi kutokana na uhaba wa vituo vya afya katika mkoa huo. Hali ambayo inasababisha kuonekana huduma zinazotolewa katika hospitali hiyo kuwa chini na duni.

(a) Je, Mhe. Waziri unaweza kulifahamisha Baraza hili mipango thabiti ya wizara hii katika kuimarisha vituo vya afya kama kile kinachojengwa Mwanyanya, Kituo cha Afya cha Chumbuni pamoja na Chukwani na Mbuzini, ili viwe visaidizi vya Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

(b) Ni wagonjwa wangapi walihudumiwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja tokea mwaka 2011/2012.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Afya katika kuimarisha Vituo vya Afya, ili kuipunguzia mzigo wa wagonjwa Hospitali ya Mnazi Moja ni kuvimalizia na kuviimarisha vituo vya afya vilioko mjini. Vituo vyenyewe ni Vituo vya Mpendae, Kwamtipura, Jang'ombe, Chumbuni, ili viweze kufanya kazi kikamilifu.

Vile vile vituo vyengine ambavyo alivitaja Mhe. Mjumbe ni Mwanyanya, Chumbuni, Chukwani na Mbuzini navyo pia vitaimarishwa kwa ajili ya kusaidia walioko huko Wilaya ya Magharibi.

(b) Wagonjwa waliohudumiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 ni 97,206.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Je, wagonjwa wangapi waliopelekwa nje ya nchi kwa ajili kutibiwa na serikali imetoa mchango kiasi gain.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hilo jibu tumelijibu juzi kishindo cha jana tena kwa urefu. Kwa hivyo, akaangalie *Hansard* ya juzi atapata majibu yote anayoyataka. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, fuata *Hansard* hiyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa vile ametukumbusha kwamba juzi alijibu, naomba nimuulize kama ifuatavyo.

Wagonjwa ambao amewataja kutoka maeneo ya Wilaya ya Magharibi ambao Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, naomba kujua katika hao ni wagonjwa wangapi ambao kesi zao hazikutibika hapa na walipelekwa nje ya nchi na tulitumia kiasi gain.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sijalielewa swali.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ni hivi Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba wagonjwa kama 96 elfu ndio ambao walifikia katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kutoka maeneo ambayo Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa ameyataja. Sasa katika hao ambao amewataja ni wagonjwa wangapi kesi zao hapa hazikutibika na walilazimika kupelekwa nje ya nchi, na kama walipelekwa serikali ilitoa kiasi gani cha fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi hawatoki Hospitali ya Mnazi Mmoja tu. Kwa hivyo, hatutengi kwamba hawa ni wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na wengine wanaotoka nje ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, isipokuwa ni wagonjwa wa nchi nzima na takwimu hizo nimezisema juzi. Kwa hivyo, ni wagonjwa wa nchi na wala sio wagonjwa wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kama unataka kujua rudi kwenye *Hansard* ya juzi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya ina jukumu la kuwahudumia wananchi kuhusiana na suala la afya zao.

Kutokana na utaratibu huo Wizara ya Afya ilikuwa na utaratibu wa kutoa jopo la Madaktari wa Magonjwa ya Macho na Masikio kupitia hospitali zetu, na kuwaona wagonjwa kwa ajili ya kuwasaidia gharama pamoja na kuwatibu.

Je, utaratibu huo wa jopo la Madaktari wataalamu wa Macho, Masikio na magonjwa mengine kupita katika hospitali zetu bado upo au umeondoka.

Kama upo, je ni wakati gani kwa mwaka mmoja wanapita katika hospitali zetu kwa ajili ya kuwaona wagonjwa.

Je, utaratibu upi unatumika, ili wananchi wapate taarifa na waweze kufika kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, aliyoyasema ni kweli lakini hiyo kazi hivi sasa imechukuliwa na Kitengo kinachoitwa *ZOP*, na kinafanya hizo huduma katika hospitali zote za Unguja na Pemba na takriban ipo na watu wanafahamishwa katika sehemu wanazokwenda. Kwa hivyo, angalia ratiba ya Micheweni lini ipo na wagonjwa wako wahamasishe kwa ajili ya kwenda kutibiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, ahsante tunaendelea.

Nam. 124

Nyumba za Kuishi Viongozi

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza:-

Kuna tatizo kubwa la makaazi hasa kwa Waheshimiwa Mawaziri, Mufti Mkuu, Naibu Mufti na hata Kadhi wa Zanzibar. Serikali inapoteza fedha nyingi za kuwakodia nyumba, ili waweze kupata makaazi bora yanayolingana na hadhi yao.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa nini serikali haitengi fedha maalum za kuwajengea viongozi wa nchi nyumba za kuishi kwa kipindi chote ambacho kiongozi huyo atakuwa anaihudumia serikali.

(b) Je, serikali haioni kama inapoteza fedha nyingi kwa kuwalipia kodi, fedha ambazo zingeweza kutumika kwa kazi nyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 124 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hivi sasa serikali inaandaa mpango wa kuwahamisha wananchi ambao wanaishi katika nyumba za viongozi huku Mazizini, na baadae kuzifanyia matengenezo nyumba ambazo ziko katika hali nzuri kidogo na pia kuzivunja zile nyumba ambazo ziko katika hali mbaya na kujenga nyumba mpya katika maeneo hayo ya Mazizini na maeneo mengine.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa ni kweli serikali inatumia fedha nyingi, na suala hili litapatiwa ufumbuzi baada ya kufanya majengo mapya katika maeneo hayo yaliyotajwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa amekiri ni kweli fedha nyingi za serikali zinatumika kwa kuwakodia viongozi nyumba hizi za kuishi.

Je, Wizara yake ina mpango gani wa kuona bajeti inayokuja zoezi hilo likaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli serikali imeona kwamba fedha nyingi ambazo zinatumika kwa kuwakodia viongozi wake nyumba za kuishi, na serikali imejiandaa kwa hilo na itakapomaliza bajeti tu, basi tutalishughulikia suala hili na tutaendelea vizuri.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

(a) Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kukiri kwamba serikali inatumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuwakodia viongozi hao nyumba za kuishi. Nataka kujua ni kiasi gani cha fedha kinachotumika katika kuwakodia viongozi hao nyumba hizo?

(b) Serikali inafahamu kwamba kuna baadhi ya viongozi wastaafu wamepewa nyumba zaidi ya moja na ambao hawazitumii nyumba hizo. Serikali kama inalijua hilo ina utaratibu gani wa kuziondosha mikononi mwa viongozi hao ambao hawazitumii, na kuwapa wale ambao wanaohitaji kuzitumia? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kiasi cha fedha zinazotumika kwa ajili ya kuwakodia waheshimiwa majengo huwezi kuzipata ghafla, kwa sababu ni wizara zenyewe ndizo zinazotumia gharama hiyo. Kwa hivyo, kuna haja ya kwenda kutafuta hicho kiasi cha fedha zinazotumika.

Pili ni kwamba jambo la kwanza tulilolifanya baada ya suala kama hili ambalo tulipata mwanzo ni kuorodhesha hizo nyumba, na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tumeshazipata nyumba katika maeneo mbali mbali ambazo zinatumika na hao viongozi. Sasa kazi iliyobakia ni kuwasiliana nao na kuwaambia kwamba kwa wakati huu inabidi watupishe kwenye hizo nyumba, ili tuweze kuzifanyia matengenezo. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

Mara nyingi sana Waheshimiwa Mawaziri wetu wanapenda kutoa ahadi na mwisho wake tunaishia kutolewa ahadi ambazo hazina ukakika kwenye Baraza hili. Je. Mhe. Waziri ni lini utatoa ahadi ya kusema hili suala litakuwa limeshakamilika?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, suala la kushughulikia nyumba na kujenga nyumba ni suala ambalo linachukua muda kidogo. Kwa hivyo, kama anataka nimwambie lini nitashindwa, isipokuwa ninachomuahidi ni kwamba hii kazi wizara yangu itaifanya na itaishughulikia kwa utaratibu kadri hali ya fedha itakavyoruhusu, na hizo nyumba zinazohitaji kufanyiwa matengenezo, tutazifanyia matengenezo na zile zenye kustahiki kuvunjwa basi tutazivunja, ili tuzijenge tena upya.

Lakini mambo ya kibajeti na mwaka huu ndio unaanza na ukimalizika unaendelea katika bajeti ya mwaka mwengine, ni *process* ambayo inabidi iendelee kutokana na muda mrefu hizi nyumba kukosa matengenezo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri, tunakushukuruni na tunaendelea.

Nam. 164

Vikundi vya Ujasiriamali

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Wizara ya Ustawi wa Jamii imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali za kusaidia vikundi vya ujasiriamali vya wanawake.

(a) Kwa nini serikali haiweki chombo kimoja cha kusaidia wajasiriamali Zanzibar badala ya kazi hiyo kufanywa na Wizara zaidi ya moja?

(b) Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto inashirikiana vipi na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, katika kutoa taaluma kwa wajasiriamali, ili waweze kutengeneza bidhaa zenye viwango vya ubora na kutumia Soko la Pamoja la Jumuia ya Afrika ya Mashariki?

(c) Kwa kuwa mazao ya viungo kama Mdalasini, Hiliki ni mazao ambayo yana soko, wizara ina mpango gani wa kuhamasisha wajasiriamali kuzalisha zaidi mazao hayo Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 164 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa madhumuni ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu, mimi nahisi hakuna ubaya wa vyombo vingi vyenye lengo moja la kumuendeleza mjasiriamali kumhudumia, kwani kila sekta ina jukumu lake na utaalamu ambao unahitajika kwa maendeleo ya wajasiriamali.

(b) Mhe. Spika, Wizara ina mashirikiano mazuri na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika maeneo yafuatayo:-

- Ushiriki wa Wajasiriamali wa Zanzibar katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Saba Saba na yale ya Afrika ya Mashariki;
- Ushiriki wa Wajasiriamali wa Zanzibar katika Soko la Jumapili;
- Namna ya kuongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa;
- Njia za kuimarisha Vikundi vya Ujasiriamali, ikiwemo namna ya kuwapatia mikopo na mafunzo.

(c) Mhe. Spika, mpango wa Wizara ya kuwahamasisha wajasiriamali upo kupitia ushiriki wao katika Maonesho ya Biashara yanayowahamasisha kupata uelewa na muamko zaidi juu ya mahitaji ya mazao kwenye masoko ya Zanzibar na nje ya Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana. Mhe. Waziri kwa kuwa mazao hayo yameonesha kuwa na soko Afrika ya Mashariki na Ulaya. Je, serikali imefanya utafiti kuona uzalishaji huo umeongezeka kwa kiasi gain.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Waziri kwa kuwa mazao hayo yameonesha kuwa na soko Afrika Mashariki na Ulaya. Je, serikali imefanya utafiti kiasi gani kuhusu mazao hayo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama nimemfahamu vizuri naomba nimwambie kwamba wajasiriamali, vikundi vya ushirika wanashiriki katika masoko mbali mbali kama nilivyojibu katika jibu langu mama.

Mhe. Spika: Majibu ya nyongeza Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuongeza kidogo kwenye swali ambalo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameliuliza.

Kwa kushirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto kupitia Wizara yetu ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, tumeandaa utaratibu mzuri hivi sasa wa kumleta mtaalamu kutoka Rwanda, ambaye atatoa taaluma kwa wajasiriamali wa aina hii, ili bidhaa zao hizo ziweze kutengenezwa katika kiwango ambacho kinaweza kusafirishwa, kwa ajili ya kushindana na Soko ambalo liko katika Afrika Mashariki. Kwa hivyo, utaratibu umeshaandaliwa vizuri tu. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kufika hapa katika hali ya usalama, kwa mintarafu ya kuendesha mambo yetu.

Mhe. Spika, kama swali lilivyoeleza kwamba kuna vikundi mbali mbali ambavyo vinashirikiana wizara moja na nyengine. Je, hawaoni kwamba kuna haja, kwa sababu watu wengine wa vikundi, wajasiriamali si waaminifu, wanaweza kwenda Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya ya Vijana, Wanawake na Watoto akachukua na wakaenda Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, wakaenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakachukua.

Je, haoni kama kuna haja ya mashirikiano ya hali ya juu kuelezana ni vikundi vingapi na kutoka wilaya gani, sehemu gani, ili kuepuka kuchukuliwa fedha nyingi na wengine hawalipi.*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza naomba nimwambie kwamba mashirikiano baina ya wizara hizo nilizozitaja yapo makubwa. Vile vile tunayo nafasi ya kukaa

kwa pamoja, ili watu kuwajumuisha kwa pamoja na waweze kufanya kazi kwa pamoja. Kwa kweli haja hiyo ipo, na tunakubaliana na suala lake ni la msingi. *(Makofi)*

Nam. 15

Uanzishwaji wa Hifadhi ya Uvuvi katika Maeneo ya Mnemba na Minai

Mhe. Abdi Mossi Kombo (Kny: Mhe. Ali Salum Haji) – Aliuliza:-

Lengo la kuanzishwa hifadhi ya uvuvi katika maeneo mbali mbali ikiwemo Mnemba (MIMCA) na Minai ni kulinda rasilimali za bahari, sambamba na kukusanya kodi kwa ajili ya kusaidia maendeleo katika vijiji husika.

(a) Je, migogoro inayojitokeza hasa ile kugombea ugawaji mapato inatokana na nini.

(b) Je, ni mafanikio gani yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa hifadhi hiyo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba lengo la kuanzisha Hifadhi ya MIMCA na Minai ni kulinda rasilimali za bahari na kukusanya kodi kwa ajili ya kusaidia maendeleo katika vijijini hivyo.

(a) Migogoro ilijitokeza ni kwa sababu ya ugawaji wa mapato unahusisha baadhi ya watu ambao si viongozi wa Kamati katika vijiji vya Matembwe na Pwani Mchangani, Kijini na Nungwi. Hivi sasa hifadhi inahusisha vijiji 30 vilivyoingizwa kisheria, lakini kuna watu ambao hata hawamo katika uongozi wa kamati husika wanapinga kujumuisha vijiji vyengine.

Hao ndio wanaosababisha huu mgogoro kwa kutaka yachukuliwe maamuzi kinyume na uamuzi wa kamati ambayo imewekwa na wanakijiji wenyewe. Kamati ya Wavuvi ndio waangalizi wa shughuli zote za uvuvi katika eneo husika, na ndio inayoshirikiana na Idara katika kuendesha maeneo hayo.

(b) Mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa hifadhi hiyo ni kama yafuatayo:-
   (i) Kupatikana kwa ofisi za wavuvi ambazo kamati inazitumia kwa kuendeshea shughuli zao.
   (ii) Mashirikiano kati ya Kamati za Vijiji na Serikali katika kuendesha doria, ili kudhibiti uvuvi haramu wenye kuharibu mazingira.
   (iii) Kuongezeka kiwango cha samaki katika maeneo ya hifadhi na
   (iv) Kuongezeka kwa ajira za wananchi katika Sekta ya Uvuvi na Utalii.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Kwa vile sehemu hii ya MIMCA ipo katika jimbo la Matemwe na anakiri kwamba imetokea migogoro, naomba kumuuliza swali moja tu la nyongeza.

Ni lini Wizara yake itachukua hatua ya kuirekebisha migogoro hiyo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, walikuja wavuvi kutoka Matemwe na mgogoro huo huo, ilibidi niende kule ili tukutana nao kama wiki mbili zilizopita, lakini kwa bahati mbaya kwa sababu ya shughuli za Baraza tumesema baada ya kujibu maswali haya tutakutana tena. Tutakwenda Matemwe na Mhe. Mwakilishi nitakuarifu ili tuwe pamoja tuweze kutizama kinachoendelea na tutatue hili suala kwa pamoja. Usiwe na wasi wasi, baada ya Bajeti sisi tutakwenda Matemwe kwa makusudi ili tuhakikishe matatizo hayo yanamalizika halan. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika ghuba ya Minai kumekuwa na tatizo kama ambapo kuna matatizo maeneo mengi ya hifadhi ya wavuvi kupatishwa tabu kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya masharti ya aina ya nyavu na zana nyengine za uvuvi ambazo wanapaswa kuzitumia. Wamekuwa mara nyingi wanalalamika kwamba Mkurugenzi wa Uvuvi amekuwa akitumia vitisho zaidi kuliko kutoa elimu na kuwafahamisha wavuvi juu ya namna bora ya kutumia zana mpya ambazo hazitoharibu mazingira.

Swali langu ni kwamba hivi sasa wavuvi hao wa eneo la Kizimkazi katika Hifadhi ya Minai wamepewa hadi Ijumaa kwamba Mkurugenzi atakwenda pale na kwenda kuziharibu nyavu zao. Je, Mhe. Waziri analitambua hilo na kama alitambua anafikiria kuchukua hatua gani ili kwenda kuwaelimisha na kuwasaidia badala ya kutumia vitisho dhidi ya wavuvi wa Kizimkazi

.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa kweli mimi niseme tu kwamba matatizo ni mengi ya wana Vijiji si Kizimkazi tu ni sehemu nyingi tu. Ndio maana tumejaribu kuzishirikisha zile Kamati za Wavuvi wenyewe ili kushirikiana pamoja na serikali ili kuhakikisha kwamba matatizo haya yanamalizika.

Hilo ambalo amezungumzia yeye kwa kweli nalifahamu na nimesema nina ziara hapa hapa, jana nilifanya ziara na leo nakenda huko huko Kizimkazi kwa taarifa yako kwenda kulishughulikia hilo suala mbalo analizungumzia. Naamini kwamba tutapata ufumbuzi halan. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunirejesha tena kuweza kumuuliza swali Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri sana yenye utamu kama asali.

Mhe. Waziri tangu ianze hiyo ghuba ya Minai kiasi gani zimepatikana. Je, pesa hizo wananchi wa vijiji vyenye ghuba ya Minai imenufaika na jambo gani ambalo linaonesha sasa hivi mtu akiliona anajua kwamba imetumiwa pesa za Minai.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Spika, kwa ufupi siwezi kukwambia ni kiasi gani, hilo nitakujibu baadaye kwa maandishi kwa sababu takwimu zipo. Lakini niseme tu lengo la madhumuni hasa ya huu mradi wa Hifadhi ya Ukanda wa Pwani kwanza kuwapunguzia umasikini wananchi ambao wanaishi ukanda wa Pwani na wanaishi katika mazingira ya bahari, hilo ndio lengo kubwa. Ndio maana tukaunda Kamati zile ili wao wenyewe wakusanye kodi na zisaidie vijiji vile.

Mafanikio yameshapatikana sehemu nyingi tu. Huko Kizimkazi ambapo tunasema, maafanikiyo yameshapatikana makubwa na tuseme kwamba tushirikiane kuhusiana na suala hili. Kwa sababu hii ni kuwamilikisha uvuvi sio wa serikali huu ni wanavijiji wenyewe kwa faida ya vizazi vya leo na vizazi ambavyo vinakuja keshokutwa. Hivi sasa vijiji vingi vimefaidika na mradi huo na bado tunaendelea na juhudi kwa kuwahamasisha, kuwapa taaluma ili waendelee kuhamasika zaidi. Lengo sio kukomoa hapana, ni kuwanufaisha wana vijiji kwa faida zao na vizazi vinavyokuja. Kwa hivyo Mhe. Mshimba ondoa hofu na bado tunaendelea na juhudi hizo. Ahsante sana.

Nam. 62

Huduma Sekta ya Uwekezaji Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Wawekezaji Wazalendo katika Sekta ya Utalii wameanza kuitikia wito wa kuanzisha vitega uchumi hasa Kisiwani Pemba.

(a) Je, sababu gani zinapelekea Mwekezaji wa Hoteli ya Kitalii ya Mbuyu mkavu huko Vitongoji Pemba, kutopatiwa huduma ya Maji, Umeme na kukabiliwa na uchakavu wa barabara, na kusababisha hoteli hiyo kushindwa kuajiri vijana zaidi ya 70 kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

(b) Kwa nini Wizara inatoa vibali vya uwekezaji kabla ya huduma za miundombinu kufika katika maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji.

(c) Kitendo cha kukosekana kwa huduma hizo kunawavunja moyo wawekezaji wengine kujitokeza. Je, serikali imechukua hatua gani kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 62 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Hoteli ya Kitalii ya Mbuyu Mkavu iliyoko Vitongoji imesajiliwa na Kamisheni ya Utalii kama mradi mdogo wa mwekezaji Mzalendo. Miradi ya aina hii husajiliwa baada ya mwekezaji mwenyewe kuomba na kubainika kwamba eneo linaloombwa ni sehemu iliyotengwa kwa ajili ya mradi husika. Hata hivyo, upelekaji wa miundo mbinu ya maji, umeme na barabara hutegemea mpango mkubwa wa kitaifa wa upelekaji wa huduma hizo katika maeneo hayo.

   Mhe. Spika, kwa bahati mbaya, Mbuyu Mkavu bado hadi sasa huduma hizo hazijafika na katika kipindi cha mwaka huu na ujao bado halimo katika mpango huo. Ili kuharakisha upatikanaji wa huduma hizo katika eneo hilo nguvu za pamoja zinahitajika kati ya Serikali, Mwekezaji na Viongozi wa maeneo hayo kusaidia upelekaji wa miundo mbinu hiyo.

b) Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii imekuwa ikitoa vibali katika maeneo hayo kabla ya huduma za miundo mbinu kufika, kwa sababu maeneo hayo yameshatengwa kwa ajili ya uwekezaji na huduma hizo na pia kujaribu kuzidi kushajiisha uwekezaji kama ilivyokuwa katika maeneo ya Michamvi, Dongwe na Wambaa.

c) Ni kweli kitendo cha kukosekana kwa huduma za miundo mbinu katika sehemu zilizowekwa vitega uchumi kinawavunja moyo wawekezaji. Hali hiyo inachangiwa sana na tabia ya baadhi ya wawekezaji kukimbilia katika maeneo yaliyokuwa hayana huduma za maji, umeme wala barabara kuweka vitega uchumi vyao. Kwa kuamini kwamba wanayapata maeneo hayo kwa bei nafuu. Hata hivyo, kwa kuwa kumeanza kuwepo matatizo ya wawekezaji kulalamikia, serikali sasa itapaswa kuangalia upya suala zima la utaoaji wa vibali vya uwekezaji katika maeneo ambayo bado miundo mbinu haijafika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo hilo limekabili maeneo mengi ya wawekezaji.
(a) Serikali itachukua hatua gani kwa mtu aliyeruhusu mradi huo.

(b) Serikali itamsaidia vipi muwekezaji huyo Mzalendo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, mwezi wa Januari tulifanya ziara na Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na tukakaa pamoja na muwekezaji huyu Mzalendo akatoa malalamiko yake kuhusu miundombinu ya maji na barabara, tukamueleza masuala mbali mbali yanayohusiana na tatizo hili na yeye mwenyewe akakubali kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii na Wizara yenyewe kama suala hili kwa kushirikiana na serikali litatatuliwa iwezekanavyo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa wawekezaji wazalendo katika Sekta ya Utalii wameitikia wito wa kuanzisha vitega uchumi. Wizara yako ina mkakati gani ambao ni thabiti wa kushajihisha utalii wa ndani ili badala ya kusubiri watalii kutoka nje, wananchi wazalendo wajenge tabia ya kutalii ili huduma za utalii zisizorote wakati wa *low season.*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi, lakini sasa hivi kuna Sera ya Utalii kwa Wote na Utalii wa ndani kama tunavyotembelea maeneo mbali mbali ya nje, tunaushirikisha sana na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mnatakiwa mtembee kwenye utalii wa ndani ili kuchangia serikali.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 –
Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe jana nilitoa taarifa kwamba mara baada ya kipindi cha Maswali kutakuwa na kauli ya Serikali. Ukiangalia kwenye orodha ya shughuli za leo hili jambo halimo katika orodha hii. Naomba niwape taarifa tu kwamba Waziri wa Afya aliniarifu baadaye kwamba jambo hili walitaka kutoa taarifa wanalifanyia kazi vizuri zaidi ili atakapokuja kuwasilisha bajeti ya Wizara yake taarifa hiyo itakuwemo kwa ukamilifu katika bajeti yake.

Kwa hivyo niwaombe radhi kwamba jambo hilo la taarifa ya Serikali juu ya maswali ya Afya leo halitokuwemo kwa sababu hizo nilizozitaja. Jana tumeacha wajumbe kama 10 ambao walikuwa wachangie. Lakini kaeleza kwamba kimsingi michango ilikuwa mingi ya kutosha maana yake kuna baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri wameomba wasaidiane na Wizara hii katika kutoa ufafanuzi wa hapa na pale.

Niwaombe radhi Waheshimiwa Wajumbe *back benchers* wale ambao hawakupata nafasi wanaweza wakitaka kufanya utaratibu wa kutoa maelezo yao kwa maandishi kwa Waziri kama wengine ambavyo tayari wameshaniletea taarifa zao wamefanya hivyo. Sasa tuchukue nafasi kwa wale baadhi ya Mawaziri walioomba ili wasaidie machache na hatimae tumuombe Waziri kufanya majumuisho.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kutujaalia kuamka wazima na wenye afya. Pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunichagua niwe mchangiaji wa mwanzo asubuhi ya leo katika bajeti hii ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Nianze pongezi zangu kwa kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuisimamia na kuiongoza Wizara hii na kumuachia jukumu Dokta Mwinyi Haji Makame kuisimamia. Kwa hivyo naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwake na kwa watendaji wote wa Wizara hii kwa namna wanavyojitahidi kwa kadri ya uwezo wao kuendelesha shughuli mbali mbali za wizara.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia mambo mawili, moja nitasaidia kutoa ufafanuzi suala la Ziara ya Mhe. Rais aliyoifanya Ras –Al -Khaimah ambalo lilijitokeza katika majadiliano hapa. La pili ambalo ndilo nitakalolianza, nitazungumzia kidogo na mimi mchango wangu kwa Wizara hii kwa lengo la kufanikisha zaidi na kufanya mambo yetu yawe bora zaidi.

Mhe. Spika, nianze na suala la mashirikiano kati ya viongozi wetu wa Mikoa na Wilaya na sisi viongozi wa Baraza la Wawakilishi kama ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au Wawakilishi wa Maeneo mbali mbali lakini pia tunapokwenda kufanya ziara hizo kama Mawaziri. Tunashukuru kwa kiasi kikubwa tunapata mashirikiano mazuri. Kazi zetu sisi kama mawaziri haziwezi kufanikiwa sana kama hatutokuwa karibu na Viongozi hawa wa Mikoa na Wilaya.

Tunashukuru sana sehemu kubwa ya viongozi hawa hasa wa Mikoa na Wilaya tunapata mashirikiano. Lakini bado kwa hapa na pale kuna maeneo fulani fulani bado tuna matatizo nayo. Naomba Mhe. Waziri kama ni salamu basi azichukue awapelekee, wakiamini kwamba sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunafanya kazi katika Wilaya na Mikoa. Ni vyema tukajenga mashirikiano yaliyokuwa mazuri zaidi.

La pili Mheshimiwa ambalo napenda niliseme hapa ni kupongeza vikosi vyetu vyote vya SMZ kwa kazi nzuri wanayofanya. Nashukuru kwa sababu mimi nafaidika na ulinzi pale nyumbani wa Vikosi. Kwa hivyo naomba kutokana na ninavyowaona vijana pale nidhamu waliyokuwa nayo na jinsi wanavyojitahidi katika kazi zao, wanakuja kwa wakati na kuondoka kwa wakati na naomba Inshallah waendelee kufanya hivyo.

Nilikuwa nina ombi maalum kwa Waziri. Hivi sasa kuna taarifa kwamba vijana wengi wanaajiriwa wengine JKU na maeneo mengine kama hayo. Kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi tumeanzisha kitengo maalum cha wale ambao wanatafuta ajira kuja kujiorodhesha pale. Ni vijana wasomi wazuri, wengi wao wana digirii za kwanza, wengine wana diploma. Ningemshauri sana Mhe. Waziri kama kutakuwa na

mashirikiano ya karibu kati ya wizara yake na wizara yangu ambayo inahusika na masuala ya ajira kwa vijana, tukashirikiana ili suala hili nalo likatafutiwa ufumbuzi kidogo.

Suala la tatu ninalolizungumza ni suala la ziara ya Mhe. Rais aliyoifanya Ras –Al -Khaimah. Kwa bahati nzuri ziara hii mimi nilikuwa miongoni mwa Wajumbe ambao niliofuatana naye Mhe. Rais. Katika ziara hiyo tulikuwa na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Ahmeid Nassor Mazrui. Kwa bahati Mhe. Rais alituteuwa mimi pamoja na Mhe. Mazrui kwamba ni waratib wa shughuli mbali mbali za Ras –Al -Khaimah na Sharja.

Kazi ambayo tumeshaifanya mara moja kwa kufanya kikao cha Kamati maalum. Wajumbe wake naomba kwa ruhusa yako Mheshimiwa niwataje wa Kamati hiyo kwa upande wa Zanzibar nao ni:-

Mwenyekiti ni Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika
Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.
Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
Mhe. Waziri wa Afya
Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano
Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.
Katibu wetu ni ndugu Amina Khamis Shaaban ambaye ni Katibu Mtendaji wa Tume.

Kamati hii imeshakutana mara moja kama ni *Steering Committee* na tunatarajia kukutana tena tarehe 17 mwezi huu katika kikao chetu cha pili. Tulipopata nafasi hii ya kwenda Ras –Al -Khaimah Mhe. Rais aliweza kuzungumzia mambo mengi ya ushirikiano kati ya Ras-Al khaimah na Zanzibar. Kwa bahati tulisaini makubaliano *Memorandum of Understanding* ambayo kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mimi nilisaini na kushuhudiwa na mwenyewe Mhe. Rais na Mfalme wa Ras–Al-Khaimah na kwa upande wao msaidizi maalum wa Mfalme wa Ras–Al-Khaimah alisaini na kushuhudiwa na viongozi hao wawili.

Lakini pia katika ushuhuda wa kutia saini hizo kwa upande wa Zanzibar Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na yeye aliweka saini yake kama ni shuhuda wa makubaliano hayo. Makubaliano hayo yana maeneo makuu manne ambayo ndio makubwa zaidi.

Tumekubaliana kwamba Ras–Al-Khaimah watusaidie kufanya utafiti kwa kuanzia suala la maji pamoja na rasilimali nyengine zilizokuwepo chini ya ardhi zitafuatia baadae, lakini kwa sababu tunafanya utafiti wa maji.

Kabla ya kufanya utafiti huo basi ilibidi tufanye *environmental impact assessment*. Tunashukuru sana Afisi ya Makamo wa Kwanza ra Rais imeshirikiana vizuri. Hatua za awali wameshakamilisha kufanya utafiti huo, Pemba tayari na Unguja tayari. Mafanikio makubwa yaliyopatikana ni kuwawezesha vijana watatu sasa hivi ambao kwanza wanasoma masuala ya udaktari, wapo huko wanaendelea vizuri. Lakini pia vijana watatu wengine wanasomea masuala ya utafiti na mambo yanayohusiana na mambo ya mafuta, ambapo Uingereza ni mmoja na wawili wapo Dubai wanaendelea na mafunzo hayo.

Masuala ya msingi ambayo tulikubaliana katika makubaliano hayo ni namna gani tunaweza tukaifanya bandari ya Zanzibar kwamba ni kituo cha biashara. Masuala hayo nayo yamo katika makubaliano hayo. Hili linashirikisha ndugu zetu wa ZIPA wanalifanyia kazi. Tunatarajia Mwenyezi Mungu akipenda katika kikao hichi cha tarehe 17 tutajua hatua ambazo zimefikia zaidi.

Jengine ambalo limo katika makubaliano hayo ni jinsi gani wenzetu hawa wanaweza wakatusaidia katika utaratibu wa kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hili linahusiana moja kwa moja na wizara yetu. Tayari juzi kiongozi wao wa Ras –Al -Khaimah anaitwa Raqdian alikuja Zanzibar na tumeshaonana naye na suala hili ameondoka nalo. Tunatarajia katika kikao cha tarehe 17 nalo litapata ufumbuzi wa kutosha.

Mhe. Spika, kwa ufupi ziara hii imetuletea manufaa makubwa na ndio tumeanza. Tusitarajie kwamba tungepata jawabu yake leo na kesho, lakini Inshallah tunatarajia sana kwamba manufaa yake na matunda yake kutokana na ziara aliyoifanya Mhe. Dokta Shein kule Ras –Al -Khaimah basi itazaa matunda mazuri.

Masuala haya ya mashirikiano haya yalianza katika awamu ya sita na sasa yanaendelezwa. Lakini hili la mkataba tumesaini hivi juzi tu na Mwenyezi Mungu akitujaalia Inshallah tunatarajia mambo yetu yatakuwa makuzuri. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Makunduchi, tunamtakia kila la kheria Mhe. Waziri katika bajeti yake. Tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuipitisha bajeti hiyo.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana baada ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kuchangia hotuba yangu hii ya Makadirio ya Bajeti ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliyofanywa kutwa nzima jana. Nikushukuru sana Mhe. Spika, kwa kuiongoza vizuri michango ya Waheshimiwa Wajumbe.
Mhe. Spika, Wajumbe wengi walijitokeza kuichangia hotuba hii. Najua wengi wangejitokeza lakini tatizo ni muda. Wingi huu umetokana na kama nilivyosema wizara hii ni kubwa kutokana na kuwa wizara hii ni wizara inayogusa jamii moja kwa moja maendeleo yao, niseme mambo yake yako wazi wazi, si mambo ya kujificha.

Mhe. Spika, huu ni wakati wa ukweli na uwazi. Mimi nawashukuru sana Waheshimiwa wajumbe kwa michango yao, maelekezo waliyotupa, busara walizotuonesha, maswali waliyotuuliza na kuturekebisha pale ambapo tujirekebishe. Sisi kama watendaji tunakiri mapungufu yetu, lakini tunashukuru wale waliotupongeza pale ambapo tumepata mafanikio. Haya ni mafanikio yetu sote na zile changamoto ambazo tunazo mimi nasema ni changamoto zetu. Sisi kama Wizara tutajitahidi kukaa chini tuone vipi tunaweza kuzikabili hizo changamoto kwa manufaa ya kuiendeleza nchi yetu.

Mhe. Spika, kulikuwa na michango ya hapa Ukumbini 27 na nimepata mengine ya kimaandishi 7 kwa hiyo jumla ni 34. Naomba kwa ruhusa yako niwatambue wote waliochangia hapa Ukumbini.

1) Mhe. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali Mhe. Ali Salum Haji
2) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
3) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4) Mhe. Farida Amour Mohammed
5) Mhe. Saleh Nassor Juma
6) Mhe. Abdalla Mohammed Ali
7) Mhe. Nassor Salim Ali
8) Mhe. Mohammed Haji Khalid
9) Mhe. Rufai Said Rufai
10) Mhe. Marina J. Thomas
11) Mhe. Rashid Seif Suleiman
12) Mhe. Omar Ali Shehe
13) Mhe. Hassan Hamad Omar
14) Mhe. Asaa Othman Hamad
15) Mhe. Hija Hassan Hija
16) Mhe. Salmin Awadh Salmin

17) Mhe. Subeit Khamis Faki

18) Mhe. Mohammed Said Mohammed

19) Mhe. Mbarouk Wadi Mussa

20) Mhe. Bikame Yussuf Hamad

21) Mhe. Amina Iddi Mabrouk

22) Mhe. Ismail Jussa Ladhu

23) Mhe. Wanu Hafidh Ameir

24) Mhe. Asha Bakari Makame

25) Mhe. Ali Mzee Ali

26) Mhe. Salim A. Hamad

27) Mhe. Haroun Ali Suleiman

Nawashukuru sana waheshimiwa hawa waliopata wasaa kuchangia hapa ukumbini, lakini wale ambao hawakubahatika kwa sababu ya muda lakini wamechangia kimaandishi nao naomba niwataje kama ifuatavyo:-

Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake

Mhe. Spika, wote tunawashukuru sana kwa michango yao, maelekezo yao, busara zao na kwa ujumla mambo ambayo wametuelekeza. Mhe. Spika, mambo ni mengi na nikijaribu kumjibu mmoja mmoja na nichambue ili mabuti yasiwe mengi nataka masaa mawili maana namkumbuka rafiki yangu Mhe. Mtando alikuwa kama kafanya dodoso hasa anataka hapa unambie hivi, hivi, hivi nimezihesabu dodoso 25 za Mhe. Mtando tu. Mhe. Jussa tena usiseme yeye kenda kwa *page* na *page* na wengine halikadhalika. Sasa sijitetei lakini ninachosema ni kwamba kwa kweli hayo mengi yanataka maelekezo, marekebisho nakubali. Kuna matatizo ya kiutendaji siku zote unapotenda ndio unapoona matatizo yako wapi kama hukutenda huyaoni na nyinyi ndio mnatuona utendaji wetu.

Kwa hivyo mimi nakiri tuna mapungufu yetu, sasa hayo tutakaa chini na hili darasa mlilotupa katika michango yenu ni darasa kubwa lazima tutafanya *post mortem*. Sisi tuna kamati yetu tendaji ya Wizara tunakaa, tuna kamati ya uongozi tutayapitia kwa undani yote mliotuelekeza. Lakini tunashukuru mengi ambayo mmetukumbusha kama mikato ya maaskari, mengi tumeshayarekebisha labda mlipokwenda nyuma huko ilikuwa bado lakini yale mengi sasa niseme tumeshayarekebisha. Sasa yale mambo ya *tendering appropriate* yote tumeshayarekebisha wakati huo ilikuwa bado hatujafanya, kwa hivyo nasema haya mengine mtaona labda sitowajibu lakini kwa kweli mengi haya kiutendaji baada ya kamati kutupitia, kutuelekeza na sisi tumeshaitikia tumeshajirekebisha.

Mhe. Spika, kwa ufupi naomba nizitaje zile *issues* na waliochangia. Kwanza *issues* kubwa sana iliyozungumzwa ni ujenzi wa matengenezo ya nyumba za Ikulu na nyumba za Serikali. Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Amina Idd Mabrouk ni mradi wa Baraza la Manispaa *diplomatic super market*. Hili nalo limechangiwa na waheshimiwa wengi Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Jaku, Mhe. Saleh, Mhe. Rufai, Mhe. Hassan Hamad, Mhe. Mohammed Said, Mhe. Bikame, Mhe. Wanu, Mhe. Subeit, Mhe. Asha Bakari, Mhe. Salum Hamad.

Halafu wasiwasi wa utoaji wa huduma wa Baraza la Manispaa. Baraza la Manispaa ninafikiri hakuna mjumbe hata mmoja ambaye hakuligusia. Hii inaonesha wazi kwamba wajumbe tunawashukuru sana kwa kuona kwamba kweli mji wetu lazima wende na kihadhi. Na msimamizi wa mji wetu ni Baraza la Manispaa. Kwa hivyo mimi kilio chenu au *concern* zenu nimezipata. Na lazima nikiri tunajitahidi lakini hatujafikia malengo ya kuwafurahisha wote lakini mimi nasema inaridhisha, kwa sababu ya matatizo ya vitendea kazi tuliyonayo ya watu kidogo wazee, lazima niseme kuna wengine watu wazima lakini hatuwezi kuwalea watu wote. Tuna wafanyakazi si chini ya mia saba na ushei lazima twende kiutaratibu kama sivyo tuta-*create* jambo jengine, kwa hivyo busara na siasa lazima zitumike. Lakini kwa kweli niseme jamani kwa kiwango chao nasema uzoaji wa taka 45 *percent* si kidogo sasa ndio maana wenzetu tumewaandikia mradi tukawauzia wamekubali kutufadhili ili kuweza kuziboresha, kuzifanya huduma za zile manispaa ziwe bora zaidi. Na ninakuahidini Mwenyezi Mungu akitujaalia mipango kama ilivyokwenda tukija kwenye bajeti ijayo tutakuja kuzungumza maneno mengine.

Mhe. Jussa alizungumza kwamba mbona mambo yamechelewa hakujafanyika chochote, kumefanyika chochote kumefanyika lakini zile taratibu za *World Bank* kidogo ni ndefu zina lazima uzifuate, ukizikosea basi utarudishwa mara ishirini ishirini. Sasa hatukuwa *slow* na zaidi kwamba huu mradi management uko Wizara ya Fedha sisi ni watekelezaji tu haina maana hatwendi sambamba tunakwenda sambamba lakini kidogo unajua ikiwa *management* mwengine na mwengine anatekeleza kidogo pana kasoro. Sasa tumeomba hii management yule mtu mwenyewe aje hasa apatiwe ofisi kwenye Baraza la Manispaa ili aratibu vizuri mambo yote na ninaamini ombi letu hilo wenzetu wa Wizara ya Fedha watalisikia.

Issue nyengine kubwa Mhe. Spika, ilikuwa ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya za Kikanda. Mhe. Saleh, alizungumza Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe. Mohammed Said, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa na Mhe. Salmin. Halafu sheria ndogo ndogo za Serikali za Mitaa, waheshimiwa wengi na walizungumza suala hili si chini ya ishirini hapa urekebishaji tunachelewa tunakubali, lakini tayari zimeshafikia pahala zile *by law* ninafikiri karibu zitatoka.

Halafu uharibifu wa mazingira pamoja na usafi katika maeneo ya mji, hili nalo kama nilivyosema waheshimiwa wengi sana wamelichangia tunashukuru sana kwa mawazo yenu na inshaalla tutayafanyia kazi.

Mishahara kwa watumishi wa Idara maalum za SMZ. Mhe. Makame Mshimba naye aliuliza Mhe. Jaku, Mhe. Rashid Seif, Mhe. Salmin Mhe. Asha Bakari, Mhe. Mbarouk, Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kwa ufupi nataka kusema kwamba hakuna lengo la kuwakandamiza askari wa chini, lakini ninachoomba kwamba unajua wakati mwengine wanasema kweli, wakati mwengine labda wengine wanaficha. Kuna mikato wanakopa wale wakikatwa kisu hafatilii lakini anaona kakatwa tu. Sasa utaratibu wa kutoa zile *salary slip* kwa kweli haupo lakini sisi tutauanzisha alau siku anakwenda kupokea mshahara aone pale mwenyewe *growth* yake ipi, *net income* yake ipi aone moja kwa moja. Na wengi hawa wanachukulia benki sasa ninashukuru kwa *observation* zenu na hili tutalifanyia kazi.

Suala la michezo nalo wamesema wasikatwe tumesikia, lakini ninachosema kwa taratibu za kiaskari kwamba madhali umejiunga wewe kama mwana KMKM yaani askari wa KMKM basi wewe ni *automatic member* wa KMKM *Sports Club* halkadhalika Mafunzo, halkadhalika Zimamoto. Lakini hiyo mikato mengine haipo mikato ile michango ya kawaida tu yaku-*maintain* hiyo klabu iende, kama si hivyo itakuwa haiendi tutazitoa wapi hizo fedha. Sasa lazima hilo wafatilie utaratibu hatuwezi kuliepuka, kwa sababu michezo tunaihimiza.

Mhe. Spika, suala jengine limezungumzwa suala la chelezo, upekuzi kwa wafanyakazi wa kigeni katika sekta binafsi, migogoro ya ardhi nayo imezungumzwa sana tunashukuru hiyo niseme kwamba juzi tulikuwa na semina elekezi kwa viongozi wa *level* ya Mikuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani na Masheha. Na walipata dozi nzuri sana ya mambo ya kuyazingatia na moja ilikuwa ajenda hiyo ya masuala ya ardhi, watu ardhi timu nzima walikuja wakawaelezea taratibu ziliopo na mambo ya kufuata na nini wajibu wao. Na nikiri kwamba wengi walikuwa wanasema sisi tunasimamia uuzwaji wa mashamba, uuzwaji wa ardhi, wakaambiwa hata hiyo kusimamiwa ni kosa, hata hiyo kusimamia hampaswi msimamie. Kwa hivyo niseme semina hii tumeifanya juzi Unguja na tutakwenda Pemba tutaifanya hiyo hiyo.

Masuala ya vitambulisho, yalizungumzwa kwa urefu, masuala yote sisemi kama hayafanywi walikuwa wakifanya lakini walikuwa hawajijui. Kuna wajibu wao upo wa kuhaulisha, yale wanapaswa lakini sio mengine. Sasa hii dozi wameipata vizuri kabisa juzi tumemaliza saa saba usiku, kulikuwa na agenda ya siku mbili pale ninashukuru sana na waheshimiwa wengi tu akiwemo Mhe. Mwanasheria Mkuu walipata wasaa wa kuwapiga lecture watu wetu. Kama nilivyosema nikimaliza hapa baadae tutakwenda na Pemba kutoa dozi kama hii.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la vikosi cha KVZ na JKU vichanganyishwe baadae nitazungumzia Mhe. Rashid Seif alizungumza hilo. Usajili wa askari ZSSF Mhe. Ismail alizungumza hilo. Ziara za Mhe. Rais anapofanya nchi za nje, namshukuru Mhe. Haroun kwa kujibu Waziri wa Kazi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hili nalo kwa kweli kila nafasi inapopatikana tunajitahidi nao wanaingizwa.

Mradi wa hospitali ya KMKM tokea kuanzishwa kwake hadi sasa ni kiasi gani zimeingizwa. Mhe. Makame Mshimba tunakushukuru tutakujibu, makusanyo ya *parking* za Forodhani na mgao wake nalo umeliuliza Mhe. Mshimba fedha za likizo kwa maaskari hizi sasa zimeanza kutolewa lakini kwa wamewekwa kwa laki moja kwa kila askari kwa kipindi kile wanachokwenda, hizi zimeanza kutolewa zamani kweli zilikuwa hazipo.

Mafanikio ya ziara za Afisa Tawala Mkoa wa Mjini Magharibi Mhe. Makame Mshimba ninakushukuru kwa uoni wako kuhusu suala hili. Machinjio ya kuku katika soko la Darajani Mhe. Jaku, njia ya Shangani imefungwa *authority* ya kufungua njia hii ni Mamlaka ya Mji Mkongwe. Hapa masuala haya ya mji mkongwe niseme kuna utatu, Baraza la Manispaa, Mji mkongwe na Wizara ya Mawasiliano kwa njia. Sasa hili nalisema sana tunajaribu kukaa lakini wenzetu wengine kuna wataalamu, na wataalamu wengine kuna wataalamu na wataalamu kuna taratibu zake ambazo UNESCO wamezimeweka kwa mji mkongwe.

Sasa pale ambapo sisi tuna uwezo kwa upande wetu ambao tunaona mimi hautoathiri ndio tunatengeneza. Ndipo pale mnaona mnaponihimiza siku zote fanya hivi fanya hivi nikakwambieni hebu ngoja nikashauriane. Lakini baada ya kushauriana nimeona linalowezekana basi tumefanya kile kinachowezekana. Sasa mengine tunawaachia wenzetu wa mji mkongwe kwa sababu ndio *authority* yao. Mimi kama Baraza la Manispaa dhamana siwezi kuliingia hilo. Lakini nitawashawishi tukaeni pamoja tusikilize maoni yenu, ushauri wenu, maelekezo yenu hakuna kisichowezekana na hakuna kisichozungumzika.

Uimarishaji wa huduma za zimamoto Mhe. Jaku ulizungumza hilo, mji mkongwe hakupitiki, sasa tumeanza utaratibu wa kununua vifaa vidogo. Jengo la zimamoto *airport* Pemba kweli ninakubali tutaomba nafasi ili japo tujenge nyuma pale kwa sababu pale nafasi tena hapana na vijana pale kukaa mbele ya uso na magodoro ya haipendezi.

Bajeti ya Chuo cha Mafunzo ni ndogo mlo mmoja kwa wanafunzi na mahabusu bajeti ya mwaka ujao tumeshaiongeza mataiona tumeiongeza marudufu hasa kwa chakula, Mhe. Jussa kazungumza hivyo, kwa hivyo mtanona tofauti. Mkurugenzi wa Manispaa kumhamisha mtu kumpa jamaa yake katika ile aliyosema Michenzani pale haitokuwa hiyo tu, tunamhakikishia tutakwenda kitaratibu. Mikato kwa maskari nimeshaizungumza hiyo.

Halafu suala jengine kubwa sana waheshimiwa mlilolizungumza suala la vitambusho, wamesema kunyimwa vitambulisho kwa upande wa Pemba, Ofisi ya Usajili ilifanya juhudi za makusudi kupitia kila jimbo ili kuwasaidia wananchi kuweza kusajiliwa. Serikali inafanya kazi za ziada katika zoezi zima la usajili kimsingi kumekuwa na udanganyifu mkubwa wa vyeti vya kuzaliwa, lazima tukwambieni jamani. Nilikuwa nataka nitoe *photo copy* hasa nikuonesheni vyeti watu wanavyo ghushi mpaka wanaghushi vyeti vya skuli mpaka vya kuzaliwa wanaghushi nilikuwa *specimen example* nataka nivilete.

Halafu watu kadhaa wamehusishwa na kughushi vyeti vya kuzaliwa kama nilivyosema. Aidha kumekuwepo na wimbi la udanganyifu kughushi hati za kiapo za mahkama. Haya yote yanayopelekea Ofisi ya Vitambulisho wawe waangalifu zaidi. Lakini pale ambapo tumewakamata kwamba hawastahiki basi tumewashtaki na ile orodha Mhe. Jussa aliioonesha na mimi ninayo nyengine na tumewanyan'ganya vitambulisho. Kwa hivyo yote tunayafanya tunamshtaki kwanza na tunamnyan'ganya kitambulisho. Hili limezungumzwa na *almost* waheshimiwa wote. Ninachosema waheshimiwa ni muhimu ni haki yake Mzanzibari yoyote suali ni taratibu tu za kufuata. Na nitatoa takwimu baadae hapa kuonesha vile vitambulisho ambavyo vipo na havijachukuliwa, sijui kwa nini nitatoa takwimu hapa.

Halafu Mhe. Omar Ali Shehe, na Mhe. Saleh wanataka kufahamu mpango wa kuendeleza barabara za ndani za mji wa Chake Chake na kuondoa uchafu katika mji. Mhe. Omar barabara ya Chake Chake imeshajengwa tena kwa kiwango cha lami kabisa wameshaziba matundu yale baada ya kushirikiana na mfuko wa barabara. Hizo ni taarifa kamili nilizozipata mimi mwenyewe sijenda hivi majuzi, lakini hiyo kazi nimeambiwa imefanywa.

Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kupatiwa fursa kupiga kura Mhe. Saleh aliuliza hili, hili bado hatujafikia huko lakini tunatizama lile suala la *dual citizenship* kama litakubalika basi hilo litakuja kufatia baadae.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa na waheshimiwa wengi ni shamba la kilimo Bambi lina tija? Mbona kila siku mapesa mengi tu hili nalo tutalitolea maelezo lakini ninachosema lina tija. Lakini siku zote tujuwe madhumuni yake lile shamba kwanza ni utafiti na uzalishaji wa mbegu au mboga mboga. Na siku zote kwenye uzalishaji kuna matatizo yake, hasa ardhi ya Bambi. Lazima tujuwe ardhi yenyewe una-*deal* nayo, ardhi ya Bambi na ile kazi yake *doctor* alilisema hili kwa urefu baadae nitakuja kueleza.

Mhe. Spika, kama nilivyosema suala jengine ni ziara za watendaji wa *Daforum emiret* juzi tu walikwenda Mhe. Ali Abdalla Mohammed aliuliza na faida zilizopatikana tutazielezea. Pia ujenzi wa matengenezo ya nyumba za Ikulu fedha tushaingiziwa nyingi tu, lakini kila siku matengenezo tu, matengenezo tu si bora tukajenga kasri nyengine. Lakini ninachosema jamani hizo nyumba za Ikulu nyengine ni kongwe tumezirithi sasa tuziache tu. Chukulia Kibweni au nyumba ya Migombani anayokaa Mhe. Rais, nyumba ya Ikulu yenyewe ile itanataka *constant maintenance* na nyinyi ndio mnatushauri yende na hadhi ya Ikulu haya ni masuala ya msingi kabisa. Kwa hivyo lazima tunapoona panahitajika marekebisho tunafanya. Lakini tuseme tulivunje lile haiwezekani. Lakini cha kufurahisha tu kwamba majengo yote haya sasa tuko katika *process* ya kuwapatia hati miliki Mhe. Omar Ali Shehe aliuliza hili. Tumeshayapima mengine na hatimiliki tayari ziko mbioni sasa kutengenezwa, yote haya yatapatiwa hatimiliki. Bwefum na kwengine kote.

Mhe. Mohammed Haji naye aliulia alitaka Waziri abadilishe sentensi katika maelezo ya utekelezaji malengo ya halmashauri ya Wilaya ya Mkoani. Tunakiri tutayabadilisha hayo marekebisho, tumeona kweli ulipochangia Mhe. Tunakushukuru tulipitikiwa tu kumradhi kidogo kwamba tulikusahau kama na wewe ulichangia, lakini tunakushuru kwa kutuunga mkono, hili ni letu na wewe pia ni jimbo lako lile.

Matumizi ya mihadharani ndani ya Chuo cha Mafunzo hili kweli ni tatizo waheshimiwa wengi mmelizungumza tena kwa hamasa. Vipi ndani ya Chuo cha Mafunzo yanatokezea haya? Kwa kweli hata sisi linatuumisha kichwa, lakini sisi tumeshasema tukimbaini askari anafanya haya, ofisa anayafanya haya huyo hatumwachii na yeye tutamtia adabu. Kwa sababu mtindo huu utokomee, kama kule wanakwenda kufunzwa tena sio kufanya uovu yeye atasaidia kupeleka madawa kule kuvuta bangi sio lengo letu la kuwarekebisha watu kule.

Mhe. Mohammed Said uanzishwaji wa Taasisi ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki aliulizia hilo. Maslahi ya wafanyakazi wa Baraza Pemba hili kweli ni tatizo lilitokezea lakini taarifa niliyopata kwamba Wizara ya Fedha wamesharekebisha na vocha zimeshapigwa. Ilikuwa mwezi uliopita hizi area ilikuwa zote walipwe lakini kwa bahati mbaya tu walikuwa wanalipa mishahara mapema lakini vocha ziko tayari zimeshapigwa na mwezi huu inshaalla na mimi nitalifatilia nisimamie kwamba area zao zinalipwa. Tunaomba radhi wenzetu kwa kucheleweshewa area zao.

Halafu nasema kutokuwepo na umuhimu wa kitengo cha usalama kwa sasa Mhe. Abdalla Mohammed alizungumza. Kitengo cha Usalama nchi yoyote lazima kiwepo, hatuwezi kukiondoa. Waingereza na *Scotland*, Wamerakani, FBI ni lazima usalama wa nchi tena unafatiliwa, unachunguzwa kila kitu. Kama Uswisi kule tokea unatua *airport* mpaka unaondoka wanaku-*monitor*. Hii waheshimiwa lazima tukubaliane ni suala muhimu sana.

Sasa naomba niende kwa urefu ile ilikuwa *summary* tu ya michango yote. Sasa naomba nigusie kwa haraka haraka Mhe. Spika, hii michango ambayo imezungumzwa. Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena ninachukua fursa hii kumpongeza Kaimu Mwenyekiti Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishiwa Jimbo la Kwahani, kwa pongezi, ushauri, maelekezo na maoni aliyoyatoa. Ushauri wake tunaupokea pamoja na ushauri wa Kamati. Mhe. Ali alielezea uimarishaji wa nyumba za Ikulu na akataka ufafanuzi kuhusu Ikulu ndogo ya Kibweni pamoja na kusisitiza ujenzi wa Ikulu ya Dodoma, Mkoani, Mkokotoni na Bwefum.

Mhe. Spika, ziara za Mhe. Rais zimechangiwa na Mhe. Ali Suleiman wengi hawa nimeshawataja. Lakini ninamshukuru Mhe. Haroun kwa kutoa ufafanuzi na yale ambayo wamekubaliana. Niseme tu kwa upande wa sekta ya afya Serikali yetu na Serikali ya *Ras-al-Khaimah* walikubaliana mambo kadhaa yanayohusu afya yakiwemo kwenda kutibiwa katika hospitali kuu ya *Ras-al-Khaimah* pia wataalamu wa Zanzibar kwenda kufanya ziara ya kitaalam huko *Ras-al-Khaimah*. Aidha wataalam wa Zanzibar kwenda kujifunza ambako vijana wawili tayari wako nchini humo kwa masomo ya udaktari.

Mhe. Spika, ujenzi wa majengo ya Ikulu nayo kama nilivyosema imechangiwa na waheshimiwa kadhaa lakini suala la msingi kwamba wazo la mradi wa uendeshaji wa Ikulu liliasisiwa mwaka 2009 na kamati iliyokuwa ya Katiba, Utawala na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Haji Omar Kheri wa Jimbo la Tumbatu. Kwa wakati huo ziara ya Kamati hiyo katika nyumba hizo ilitokana na bajeti ndogo iliyokuwa ikitengwa ambayo haikukidhi matengenezo yaliyokusudiwa, na iliamuliwa kuanzishwa mradi maalumu wa ujenzi wa nyumba za Ikulu.

Nyumba zenyewe ni Ikulu ya Mnazi mmoja, Ikulu ya Migombani, Nyumba ya wageni Kikwajuni yaani *Bosnia*, nyumba ya Mazizini namba 1, nyumba ya wageni Mazizini namba 2, nyumba aliyokuwa anaishi Mhe. Waziri Kiongozi, nyumba ya Bwefum. Nyumba ya Kibweni, nyumba ya Mkokotni, nyumba ya Mkoani, nyumba ya Chake Chake, nyumba ya Wete, nyumba ya Laibon Dar es Salaam, nyumba ya Haileselassie Dar es Salaam, nyumba ya Dodoma namba 1, Dodoma namba 2, Dodoma namba 3 jumla 17 hizi.

Mhe. Spika, mradi huu kwa wakati huu ulikusudiwa kutumia shilingi bilioni kumi unaotekelezwa kwa muda wa miaka 5, ilikuwa mkakati nyumba zote viongozi wetu wakilalamika wanakwenda Dodoma, wanakwenda Dar es Salaam hawakai pazuri. Sasa lengo lake ni hilo twende kidogo kidogo lakini tuzitengeneze. Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha uliopita nyumba ya Haileselassie, nyumba anayoishi Makamo wa Pili wa Rais, na nyumba ya Dodoma namba 3 iliondolewa na kuwekwa katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Serikali imeweka muda wa miaka 5 kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba hizo.

Mhe. Spika, matengenezo ya nyumba ya Migombani yamekamilika. Hivyo namuomba Mhe. Omar Ali Shehe kuwa Ofisi yangu iko tayari kwa kamati yake kuitembelea nyumba hiyo wakati wowote, siku ile ilikuwa bahati mbaya tu. Kwa hivyo tuko tayari tupange miadi na hivi sasa Mhe. Rais hayupo basi itakuwa vizuri tutakutembeza nyumba yote kabisa.

Mhe. Spika, ninakubaliana na maoni ya Mhe. Rashid Seif kwamba Serikali itafute eneo la kujenga nyumba za viongozi na kamati maalumu imeshaundwa chini ya mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kulisimamia suala hili kutafuta eneo la ujenzi wa nyumba hizo. Lakini pia kamati hii imeshapitia eneo la mazizini, walitembea kwa miguu eneo lote la Mazizini pamoja na nyumba anayokaa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na nyumba anayokaa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na nyumba anayokaa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani na nyumba nyenginezo walitembea na kuona mpango ambao wenyewe tufanyeje Mazizini iweje?

Pili kuhusu hati za nyumba kama nilivyosema suala hili limeshakamilika na lengo kama Fumba kule kuzuia mmong'onyoko na tunaambiwa kule kunahitajika kama shilingi milioni 1.1 kwa ukarabati wa ile nyumba ya Fumba. Lakini tunashukuru alau tumeiezeka ile kuvujiwa kidogo imeacha tunashughulikia haya mengine. Bado dhamira tunayo kuifanyia matengenezo nyumba hiyo ambayo kwa sasa kama nilivyosema tumeshaiezeka ili tuihifadhi isiendelee kuharibika.

Mhe. Spika, waheshimiwa wawakilishi waliochangia mishahara ya askari na chakula cha askari kama nilivyowataja Mhe. Ali Salum, Mhe. Salmin, Mhe. Jussa Mhe. Mtando, Mhe. Wanu. Serikali imerejesha miundo ya kiutumishi kwa lengo la kuweka tofauti ya mishahara kati ya wafanyakazi wenye uzoefu wa muda mrefu na wale wenye uzoefu wa muda mfupi kwamba uzingatiwe upandishaji wa daraja kwa watumishi wa kawaida na vyeo kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ. Mpango huo unatarajiwa kutumika baada kupitishwa katika Tume ya Utumishi ya Idara Maalumu ya SMZ.

Aidha Serikali inaahidi kwamba watumishi wa Idara Maalumu za SMZ hawatakatwa mishahara yao kwa ajili ya kuchangia pesa ya chakula cha wapiganaji, hili jukumu sasa linachukuliwa na Serikali na ndio maana utaona bajeti ya chakula kwenye vikosi imekuwa kubwa sana, suala hili moja kwa moja tunalichukua Serikali. Hii inatokana na mazingatio makubwa yamefanywa ya kuongeza bajeti ya kula kwa Idara Maalumu za SMZ katika mwaka wa fedha ujao. Kwa wastani bajeti ya chakula imeongezeka kutoka shilingi milioni 400 mwaka jana hadi kufikia shilingi milioni 750 kwa mwaka wa fedha 2012/13.

Kwa mujibu wa katiba za michezo katika vikosi kila askari ni mwanachama hili nimeshalielezea kwa urefu. Nakiri kwamba yapo malalamiko katika eneo linalotaka kujengwa Chuo Hanyegwa mchana ambacho waliazimwa kulima mazao ya muda mfupi, kama vile muhogo, viazi, majimbi na hatukuorodhesha mazao hayo kupitia kwa Sheha eneo

husika limechukuliwa na tathmini ya mazao haya yamefanywa na Wizara ya Kilimo kwa hivyo mazao hayo yanatarajiwa kuvunwa hivi karibuni kabla ya ujenzi wa Chuo kuanza. Hili tutalimaliza tushafanya tathmini wameorodheshwa tutachukua hatua ipasavyo za kiserikali kuona wanalipwa ili kutoa nafasi kwa ujenzi.

Niseme tu kwamba hakuna malimbikizo yoyote ya malipo ya wastaafu wa KMKM. Naomba nimjulishe jukumu la kulipa wastaafu wote ni la Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Sisi huku tunaorodhesha akimaliza faili lake tunalipeleka kule mambo yote yanamalizwa kule, huo ndio utaratibu uliopo.

Mhe. Ali Salum alitanabahisha juu ya askari wa Chuo cha Mafunzo kujisafirisha wenyewe kutoka Pemba wanapopewa uhamisho. Ni kweli askari wa Chuo cha Mafunzo wanaosafirishwa pamoja na vifaa vyao, hali hii inasababisha Idara kushindwa kuwagharamia askari na familia zao kwa pamoja, askari wenyewe hujikubalisha wao wenyewe kurudi Unguja kwa gharama zao mara tu wanapomaliza ile ngwe yao ya kukaa Pemba. Ikifika tu hawangoji na baadae huwa wanarejeshewa fedha zao. Lakini hapa tunapompa *transfer* nenda Pemba inakuwa shida hata umpe pesa haendi. Lakini utaratibu unafanywa ninashukuru wengine wanajitolea wanakwenda zao lakini wengine inakuwa shida kidogo. Sasa kutokana na matatizo ya fedha tunakubali kwamba hili lipo lakini tutalirekebisha.

Mhe. Spika, ninampongeza sana rafiki Mhe. Saleh Nassor kwa kuwa karibu na Ofisi yetu. Kimsingi wanafunzi wanaoletwa Chuo cha Mafunzo baadhi yao ni wateja wa matumizi ya dawa za kulevya, na huwa wameathirika na dawa hizo hali ambayo inaweza kusababisha kuonekana kama wanatumia wanapokuwa chuoni, bado ile *hang over* wanayo wanakwenda nayo. Wanapobainika kuingiza dawa hizo basi tunawadhibiti, kwa mujibu wa sheria pindipo mwanafunzi au askari atakayebainika kuingiza au kutumia dawa za kulevya, akiwa yupo chuoni huwa kama ninavyosema anachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kumfukuza kazi kabisa.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Saleh Nassor Juma kuwa baadhi ya kambi za chuo cha mafunzo miundombinu yake sio ya kuridhisha. Kimsingi vyuo vyetu vya mafunzo vyote vimejengwa wakati wa ukoloni kwa lengo la kuwaadhibu wahalifu na pia vyuo hivyo itakuwa vigumu kufanya marekebisho ya miundombinu, ndio yale aliyozungumza habari ya mtondoo na mengineyo. Kwa vile vyuo ambavyo imewezekana tayari marekebisho yameshafanyika, tumefanya Kangagani, Tungamaa, lakini kwengine kunakuwa kugumu kidogo kama pale Wete.

Katika kukabiliana na tatizo hilo serikali imeamua kujenga chuo kipya cha kisasa kitakachozingatia haki za binadamu na miundombinu iliyo bora. Aidha katika kipindi hiki idara imeanza kuchukua hatua ya kukarabati na kujenga majengo hayo kwa kambi za Unguja na Pemba kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mhe. Spika, naomba kumjuilisha Mhe. Rashid Seif kwamba jina la Chuo cha Mafunzo linatokana na Katiba ya Zanzibar na kama kutakuwa na ulazima wa kubadilishwa basi Katiba yenyewe ya Zanzibar ifanyiwe mapitio. Hata hivyo, kwa mujibu wa nchi nyingi duniani hivi sasa jina la Magereza halipendezi na halitumiki tena na badala yake hutumika jina la *department of correctional services*. Hili ndilo jina sahihi linaloendana na haki za binadamu.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kwa umuhimu wa Kikosi cha KMKM kutumia chelezo chake kwa ajili ya matengenezo ya boti zake na hasa ikizingatia kanuni za kiusalama. Katika kufanikisha hilo serikali imelipa umuhimu mkubwa wa kukijenga upya chelezo cha KMKM. Tayari jitihada kubwa katika kufufua chelezo hicho zinaendelea na chelezo hicho kilijengwa katika miaka ya 1970 kwa msaada wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ujerumani. Aidha, mawasiliano ya awali yamefanyika na mkandarasi kama nilivyowahi kujibu swali kutoka *Damian Shipping* ya nchini Uholanzi kwa kuangalia gharama za matengenezo ya chelezo hicho. Mbali na hilo jitihada zinafanyika ili kufanya upembuzi yakinifu utakaotoa muono halisi ya ujenzi wa chelezo hicho.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/12 serikali ilianza kufanya juhudi za makusudi za kukiimarisha kituo cha uzamiaji cha KMKM kiliopo Kibweni. Katika awamu hii ya kwanza askari 30 wa kitengo hicho wamepatiwa mafunzo ya mwenzi mmoja yaliyoendeshwa na wataalamu kutoka Uingereza. Aidha vifaa mbali mbali vimenunuliwa vikiwemo vifaa kamilifu vya wazamiaji 15, *life jacket* 200, mtambo wa kuhifadhia hewa mmoja na vifaa vyengine muhimu.

Mafunzo ya hatua ya pili yaliyoshirikisha askari 22 yanaendelea. Katika awamu ya pili ya mpango huu wa kuimarisha vitengo vya uzamiaji ambayo itaanza katika mwaka wa fedha wa 2012/13 serikali itaanzisha kitengo cha

uzamiaji katika kituo cha KMKM kiliopo Mkoani. Vifaa vitakavyonunuliwa katika awamu hii ya pili baadhi yake vitapelekwa huko na sehemu ya wale ya askari watatupa mafunzo katika mwaka huu wa 2012.

Mhe. Spika, hakuna sintafahamu kati ya Baraza la Manispaa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hasa ukitilia maanani kwamba chombo hiki cha Manispaa kiko chini ya ofisi hii. Ndio maana jambo lolote linalohusu Manispaa msemaji wake katika Baraza hili na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, kwa mujibu wa sheria Nam.3 ya mwaka 1995 inampa mamlaka waziri anayesimamia Baraza la Manispaa kujua miradi mikubwa inayotaka kuendeshwa na inayoendeshwa na Baraza namna itakavyotekelezwa. Hapa jambo kubwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inasisitiza kufuatwa kwa sheria ya mikataba na utaratibu uliopo, hasa ukitilia maanani kwamba mmoja kati ya anayepatumia ni Shirika la Umeme.

Lile ni eneo la serikali, jumba la *Diplomatic Super Market* ni la serikali na msimamizi wa serikali katika wizara hii ni waziri anayesimamia Manispaa. Hili jambo lifuate taratibu tu, haiwezekani kwamba twende pale muhusika au mkuu wa Manispaa aseme mwenye duka funga duka kesho unikabidhi, wizara haijui, utaratibu hauwendi hivyo. Sasa tunachosema sisi muhimu zile taratibu za kiwizara tuzifuate tu hakuna tatizo lolote, sisi ndio wasimamizi, yeye ndiye mwenye mali tutampa kwa mujibu wa mipango yetu iliyopo hakuna tatizo lolote.

Mhe. Spika, Mhe. Saleh Nassor wa Jimbo la Wawi tunampongeza sana kwa mchango wake, napenda kumthibitishia kwamba Baraza la Mji Chake Chake linajitahidi katika kudumisha usafi. Utaratibu unaotumika katika kusafisha eneo la mji wa Chake Chake kwanza jaa la sokoni lipo, kanisani na Machomane huwa taka zinazolewa siku zote isipokuwa siku ya Jumapili tu. Majaa madogo madogo ya mitaani kama vile Msingini, Kichungwani na Mtoni huwa wanazolewa si zaidi ya siku mbili hadi tatu katika hali ya kawaida. Jaa kubwa la sokoni tayari limeshafungwa na halitumiki tena, hakuna jaa hata moja lenye sura mbaya kwa sasa. Fedha zinazokusanywa na Baraza la Mji huwa zinatumika kwa usafi na kuchangia miradi ya maendeleo. Hali itakuwa nzuri zaidi baada ya kuwasili kwa gari kupitia mradi wa *ZUSP* hivi karibuni.

Kama nilivyosema kwa kweli jamaa wanajitahidi, bahati mbaya hizi zana ndio tatizo lao. Kwa hivyo, kwa kweli mradi wa *ZUSP* ni imani yetu kwamba utapokuja utaweka sawa na kutusaidia sana kuyafanya mambo yawe bora zaidi.

Nampongeza Mhe. Farida kwa michango yake, yapo mengi ambayo tumeyachukua na tutayafanyia kazi. Ni kweli Ofisi ya Baraza la Mji Wete ni ndogo na inatokana na kwamba jengo la awali halikuwa ofisi lilikuwa ni soko la samaki, baada ya kufanyiwa ukarabati likabadilishwa na kuwa ofisi ya Baraza la Mji. Kimsingi jengo hilo haliwezi kutosheleza mahitaji yetu, jengo lile huwa linafanyiwa matengenezo mara kwa mara ili liendane na hadhi ya ofisi ya Baraza la Mji. Aidha, kupitia Mradi wa *ZUSP* pia jengo la ofisi ya Baraza la Mji Wete litatengenezwa upya kwa gharama ya dola za Kimarekani zipatazo 40,000.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Mohammed Haji Khalid ambaye ni Mjumbe wa Kamati inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu kwa michango yake. Nafikiri nimpongeze sana na naomba nimjuilishe tu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imechangia ujenzi wa banda la madarasa katika Skuli ya Sekondari Kengeja na kutaoa bati 23 zenye thamani ya shilingi laki nne na nusu. Hivi sasa banda hilo limeshaezekwa na limeshafunguliwa.

Katika Madrasatul Kadiria ya Kengeja imechangiwa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi laki sita, daraja la mto mkuu limechangiwa vifaa vya ujenzi wa thamani ya shilingi laki nne na nusu. Aidha, Skuli ya msingi Makhuduthi imechangiwa matofali yenye thamani ya shilingi laki mbili ishirini na tano elfu.

Mhe. Spika, Kikosi cha Kujenga Uchumi (JKU) na Kikosi cha Valantia haviwezi kuunganishwa na hii inatokana na dhamira ya kuanzishwa vikosi hivi. Dhamira hii ilikuwa ni tofauti na bado ni tofauti, vikosi hivi vyote vilianzishwa kwa mujibu wa sheria zilizopitishwa na Baraza hili tukufu Mhe. Spika. Kikosi cha JKU kimeanzishwa kwa Sheria Nam. 6 ya mwaka 2003, wakati Kikosi cha Valantia kimeanzishwa kwa Sheria Nam. 5 ya mwaka 2004. Ndani ya sheria hizi yameelezwa wazi wazi majukumu ya kila kikosi. Kwa mfano, jukumu kubwa la JKU ni kuwalea vijana wakati jukumu la Valantia ni kufanya kazi kama jeshi kwa madhumuni ya kuzuia hali inayohatarisha amani na usalama wa nchi yetu.

Mhe. Spika, mradi wa Shamba la Mfano Bambi umeasisiwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Misri. Utaratibu wa uendeshaji wa mradi huu umeelezwa waziwazi katika MOU ambapo yaliainishwa malengo matatu makuu ambayo ni kufanya utafiti kwa wasomi wa Vyuo Vikuu, Kutoa elimu kwa wakulima wadogo wadogo na kutoa mbegu bora ambazo husambazwa kwa wakulima kwa bei nafuu. Faida ambazo zimepatikana hadi sasa ni kwamba haya malengo matatu yote yanaendelea kutekelezwa. Hadi sasa jumla ya wanfaunzi 12 kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Morogoro walikuja kufanya tafiti za aina mbali mbali. Aidha, wananchi wa Bambi wanafaidika kupata elimu ya kilimo cha mbogamboga.

Sambamba na hilo shamba hili limeweza kutoa mbegu bora za mahindi na mtama na kusambazwa kwa wananchi. Kwa mfano, mwaka 2010/11 jumla ya tani tatu za mahindi na tani moja na nusu ya mtama zimevunwa. Kwa mwaka 2011/12 zimeweza kulimwa mbegu za mahindi ekari 15, mtama ekari 10 na mpunga mbegu ile mpya na Nerika ekari 40.

Mhe. Spika, shughuli zinazofanywa na Kikosi cha Zimamoto zimechangiwa na Waheshimiwa Ali Salim, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Rashid Seif, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Mohammed Said Dimwa. Nakubaliana na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba mazingira ya askari wa Zimamoto katika uwanja wa ndege wa Pemba sio ya kuridhisha. Lile eneo linalotumika si eneo la Kikosi cha Zimamoto na Zimamoto haina mamlaka ya kufanya marekebisho yoyote kwa sehemu hiyo. Hata hivyo, mazungumzo yanaendelea baina ya kikosi hicho na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, endapo itakubalika ujenzi wa ofisi au bweni utafanyika katika mwaka huu wa fedha basi tutaanza ili kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Spika, kuhusu uwezekano wa kupitisha magari ya Zimamoto katika Mji Mkongwe wakati wa ajali. Tatizo ni usimamiaji mbovu wa ujenzi katika mji huo uliokuwepo hapo zamani ambapo umekuwa hautowi kipaumbele cha kuwepo kwa barabara za uhakika kuweza kupitisha magari ya Zimamoto inapotokea ajali. Kukosekana kwa visima ndani ya mji huo nalo ni tatizo jengine. Katika kukabiliana na hali hiyo Kikosi cha Zimamoto kimechukua hatua za dharura za kufanya mazungumzo na Kampuni ya ***IFECS*** ya Ujerumani kuhusu uwezekano wa kukipatia kikosi magari madogo *land rover pick up*. Vile vile kununua vifaa vya kisasa vya *DSPA* ambavyo vinaweza kuzima moto mkubwa kwa kutumia maji kidogo. Vifaa tayari vishafanyiwa maonesho kwa taasisi za serikali na watu binafsi na vimeonesha kuwa vinaweza kutusaidia katika kutoa huduma za kikosi hicho kwa ufanisi.

Kimsingi Kikosi cha Zimamoto kina vifaa vya kutosha kwa sasa, lakini tatizo lililopo ni uchimbaji wa visima ni vyembamba na ujenzi holela usiokuwa wa mpango. Serikali inatoa wito kwa yoyote anayetaka kuchimba kisima ni vyema awasiliane na Kikosi cha Zimamoto ili apate ushauri. Aidha, tayari tumeshawasiliana na Shirika la Bandari kwa ajili ya kupata eneo la kujenga kituo cha Zimamoto, kituo hiki kitakapokamilika tayari tumeshatayarisha gari la Zimamoto kwa ajili ya Bandarini.

Mchakato wa upatikanaji wa boti ya kuzimia moto unaendelea kwa kushirikiana na Idara ya Maafa. Kikosi cha Zimamoto kimeshawasiliana na Kampuni ya ***IFECS*** ya Ujerumani kwa ajili ya upatikanaji wa gari ndogo ya kuzimia moto ambazo zitaweza kukidhi haja ya kupita katika baadhi ya njia za Mji Mkongwe. Pia tuna lengo la kuweka Kituo cha Zimamoto katika kila wilaya kote Unguja na Pemba, hii ni kutekeleza ahadi ambayo Mhe. Rais aliitoa wakati wa kampeni yake ya uchaguzi.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Mtando kwa michango yake aliyoitoa, naomba nimjuilishe kwamba jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja hadi sasa limeshawekwa baadhi ya milango, madirisha yote, sakafu vyumba vyote na plasta jengo lote. Hivi sasa kilichobaki ni kuunganishwa umeme na kumalizia matengenezo madogo madogo. Jengo litamalizika ndani ya bajeti ya mwaka huu wa fedha, namuomba sisi tuko tayari na yeye akenda Mkwajuni kule jimboni basi apite pale twende tukakague tumuoneshe atupe ushauri najua yeye kidogo ni mjenzi mzuri sana na mambo ya umaliziaji majumba haya anayafahamu.

Mhe. Spika, kwa upande wa kushajihisha wazee juu ya elimu Mkoa wa Kaskazini kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya pamoja na taasisi zisizokuwa za serikali kuliandaliwa seminza zenye lengo la kuangalia matatizo ya kunyanyua kiwango cha elimu ndani ya mkoa kwa Walimu Wakuu wote wa Mkoa. Kamati za skuli zote, viongozi wa ngazi zote, wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge na Madiwani. Adiha, ziara za kuonana na wazazi, walimu na wanafunzi ziliendelea kufanywa katika skuli zote za Mkoa. Ziara hizo zinaongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Bodi za Elimu; jumla ya wafanyakazi 22 waliajiriwa katika kipindi cha mwaka 2010/11, kati ya

hao watatu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, sita katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’, watano katika Wilaya ya Kaskazini ‘B’ na wanane katika Wilaya ndogo ya Tumbatu.

Eneo linalotakiwa kujengwa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini ‘A’ lipo Moga Biboni, eneo hilo lilikuwa likitumiwa na wananchi kwa kilimo, Afisi ya Wilaya imewalipa fidia wananchi ambao walikuwa wakitumia eneo hilo sio kama kununua *in such.*

Mhe. Spika, Mkoa wa Kaskazini ulikuwa na jumla ya migogoro 15 ya ardhi, kati ya hiyo migogoro saba tayari imeshatatuliwa na migogoro minane ipo Mahakamani. Katika Mkoa wa Mjini Magharibi kuna jumla ya migogoro 479 ambapo hatua ya kwanza ni kuitambua idadi halisi ya migogoro yenyewe. Katika kutekeleza hatua hii, Mkoa umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Mei mwaka huu kuna migogoro hiyo au mizozo hiyo ya ardhi. Hatua ya pili ni kuichambua katika makundi kama ifuatavyo:

a) Migogoro inayowahusu wananchi wenyewe kwa wenyewe. Migogoro ya aina hii itatatuliwa kwa utaratibu wa kazi za kawaida za wilaya, shehia, halmashauri pamoja na manispaa, wilaya na mkoa. Hadi kufikia mwezi Mei mwaka huu jumla ya migogoro 15 imebainika katika *category* hii.
b) Migogoro inayowahusisha watendaji katika ngazi ya shehia, halmashauri au Manispaa, wilaya na mkoa. Hadi kufikia mwezi Mei mwaka huu jumla ya migogoro mitano imeripotiwa. Kutakuwa na utaratibu maalum wa kutatua aina hii ya migogoro kwani itahusisha utendaji katika utumishi pamoja na sheria za ardhi.
c) Migogoro inayotokana na sekta na wananchi. Mkoa utashirikiana na sekta husika ikiwa ni kilimo na ardhi katika utatuzi wake. Jumla ya migogoro tisa imeripotiwa na
d) Migogoro iliyokuwa katika hatua ya Mahakamani. Mkoa umefuatilia kesi hizo na utaratibu mzima juu ya mwenendo wake ili kuweza kutathmini kiutendaji. Hadi kufikia mwezi Mei mwaka huu tumearifiwa kuwa kuna kesi 450 zimeshafunguliwa katika Mahakama ya Ardhi ambazo zinafanya asilimia 30 ya jumla ya kesi za ardhi nchini.

Mhe. Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi umejipanga kutekeleza mpango wa kutoa elimu juu ya uchimbaji holela wa mchanga kwa wananchi kupitia kamati za mazingira za shehia. Aidha, Mkoa katika mpango wake wa kuondoa wanyama wanaozurura ovyo barabarani kwa kushirikiana na Manispaa. Halmashauri za Wilaya wamejipangia kuyasajili magari yote ya ng’ombe na punda ili kuwezesha kuyatambua na baadae kuwaelimisha wachunga punda na ng’ombe na hatimaye kuanzisha utaratibu wa kuyaondoa kwa kuyabadilisha kwa pikipiki za maringi matatu.

Mhe. Spika, napenda kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba kiwanja cha Mkoa wa Mjini Magharibi kiliopo Amani ni cha Mkoa kwa mujibu wa hati Nam. 2 iliyopo Unit NiU 20. Aidha, kimsingi kiwanja hicho hakina mgogoro kama kinavyofikiriwa na wengi, kinachoonekana katika kiwanja hicho ni kutokufahamu kulikokuwepo kwa kiongozi wa Uwanja wa Amani ambaye anadhani kuwa eneo hilo ni sehemu ya eneo lake la uwanja uhalisia wake hauko hivyo. Mkoa unaendelea na hatua za mazungumzo baina ya taasisi zetu mbili yaani Mkoa na Uwanja wa Amani juu ya namna ya kuwaondoa wauza magari yaani yadi ile ya kuuza magari iliyoanzishwa katika eneo lile.

Mhe. Spika, kuhusu juhudi za wizara za kuwashirikisha wananchi katika mradi wa mageuzi Serikali za Mitaa. Suala hili limeelezwa vizuri katika ukurasa wa 21 wa hotuba yangu ambapo vikao kumi vya wadau mbali mbali viliitishwa kwa lengo la kupata maoni yao wakati wa mchakato maandalizi ya Serikali za Mitaa. Sera ya Serikali za Mitaa sasa imekamilika na kinachoendelea ni kuandaa mazingira bora ya utekelezaji wa sera hii ikiwa ni pamoja na utungaji wa sheria, sio kama hakukufanyika chochote mwaka jana na mwaka huu na mwaka keshokutwa, tatizo kwamba hii kazi sio nyepesi na kuna modeli nyingi, kuna modeli za Tanzania Bara na kwengineko. Sasa tutafute modeli ambayo inafaa kwa nchi yetu, na kwa kweli vikao vingi vimefanywa tumewashirikisha watu wengi na tunashukuru sasa tumefika pazuri tumeshahitimisha tena. Kwa hivyo, mwakani hatutokuja tukasema tena kwamba tunatayarisha vikao kutayarisha sera aa, tutakuja kwenye utungaji wa sheria za kutekeleza hizo Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, kuhusu boti ya KMKM Kojani na mashine imechangiwa na Mhe. Hassan Hamad Omar. Kimsingi boti iliyoelezwa ipo pamoja na mashine yake, labda wakati mwegine tu inazimwa kufanya kazi nyengine hizo zilizozungumzwa za kuwasaidia kuwavusha viongozi.

Mhe. Spika, Ofisi ya Usajili na Kadi za Mzanzibari ilichangiwa na waheshimiwa wengi tu kama nilivyowataja sitaki kurejea tena, isipokuwa nataka kusema kwamba Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho Zanzibar inafanya kazi

kwa kuzingatia sheria nambari 7 ya mwaka 2005. Kanuni pamoja na sheria nyengine zinahusiana na usajili huo, usajili hufanyika bila ya ubaguzi wala masharti magumu. Masharti yaliyopo hivi sasa ni ya kisheria na naomba niwakumbushe tu Waheshimiwa, masharti kimsingi ni manne.

Kwanza tumesema awe Mzanzibari ambaye makaazi yake ya kudumu ni Zanzibar, hilo ni sharti la kwanza. Sharti la pili awe na umri wa miaka 18 au zaidi. Sharti la tatu awe amefika mwenyewe kwa Sheha wa Shehia anayoaishi na kupatiwa barua ya uthibitisho kama anaishi katika shehia hiyo na sharti la nne awe na cheti za kuzaliwa, kama hana cheti cha kuzaliwa basi ende Mahakamani akale kiapo.

Mhe. Spika, watu wenye umri zaidi ya miaka 48 yaani wale waliozaliwa chini ya mwaka 1964 ambao hawana vyeti vya kuzaliwa, Ofisi ya Usajili na Kadi ya Utambulisho Zanzibar imetoa muongozo tangu mwaka 2009 kwamba watu wa aina hiyo wanaruhusiwa kujisajili kwa kutumia hati ya kiapo kutoka Mahakamani. Aidha, vitambulivyo vilivyokuwepo katika ofisi za wilaya na havijachukuliwa na wenyewe, ni kweli katika Wilaya ya Chake Chake pekee kuna vitambulisho 8,242, idadi kamili vitambulisho vilivyokuwa havijachukuliwa kwa kila wilaya ni kama ifuatavyo:

Wilaya ya Wete vitambulisho ambavyo havijachukuliwa na wenyewe 9,002; Wilaya ya Micheweni vitambulisho 6,939; Wilaya ya Chake Chake vitambulisho 8,242; Wilaya ya Mkoani vitambulisho 7,059; Wilaya ya Mjini vitambulisho 28,713; Wilaya ya Magharibi vitambulisho 22,193; Wilaya ya Kati vitambulisho 7,579; Wilaya ya Kusini vitambulisho 2,375; Wilaya ya Kaskazini 'A' vitambulisho 13,230; Wilaya ya Kaskazini 'B' vitambulisho 7,088. Jumla Mhe. Spika, vitambulisho ambavyo havijachukuliwa na wenyewe mpaka hii leo ni 112,420. Hiyo ndio hesabu halisi ya vitambulisho ambavyo vipo havijachukuliwa na wenyewe.

Mhe. Spika, kutokana na tuhuma za kuwapatia vitambuliso wageni ofisi inafanya juhudi za makusudi katika kufanyia kazi suala hilo kwa kufuatilia taarifa za watu hao katika ofisi za Uhamiaji Zanzibar na Jeshi la Polisi na kwamba keso tatu zipo Makamo Makuu ya Polisi Zanzibar katika kitengo cha udhibiti wa mali za serikali na kesi tano zipo Ofisi ya Uhamiaji kwa upelelezi wa uraia wao.

Mhe. Spika, Sheria Nam. ya mwaka 2005 imetungwa na Baraza la Wawakishi Zanzibar, sidhani kama ina matatizo ila utekelezaji wake ndio una matatizo. Kwanza ni kwa baadhi ya wananchi wenyewe kutofuata utaratibu wa sheria, ili mwananchi aweze kusajiliwa anapaswa kuwasilisha vielelezo vya uthibitisho wa Uzanzibari wake, ukaazi wake na umri wake, vielelezo hivyo ni cheti cha kuzaliwa na barua ya sheha na shehia yake. Hata hivyo, baadhi ya wananchi wanakwenda kinyume na sheria kwa kutowasajili watoto wao na hivyo kutokuwa na cheti za kuzaliwa kinyume na sheria nambari 10 ya mwaka 2006 ya vizazi na vifo.

Aidha, baadhi ya wananchi wanapohama kutoka shehia moja kuhamia shehia nyengine wanakwepa utaratibu wa kuchukua barua kutoka kwa sheha wa shehia anayohama ili aiwasilishe kwa sheha wa shehia anayohamia ili asajiliwe katika daftari la shehia na atambuliwe kuwa mkaazi wa shehia hiyo mpya kwa mujibu wa sheria nambari 1 ya mwaka 1998 iliyoanzishwa ya Mamlaka ya Masheha.

Mhe. Spika, ukiukaji huu wa sheria unasababisha mazingira magumu kwa masheha kuweza kutimiza majukumu yao kikamilifu kwa kushindwa kutoa barua kwa watu ambao hawawatambui. Aidha, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho haiwezi kumsajili mtu bila ya kuthibitisha umri wake. Hata hivyo, kama nilivyosema hapo awali kuwa watu wenye umri wa zaidi ya 48 yaani wale waliozaliwa chini ya mwaka 1964 ambao hawana vyeti vya kuzaliwa, Ofisi ya Usajili imetoa muongozo tangu mwaka 2009 kuwa watu wa aina hiyo wanaruhusiwa kujisajili kwa kutumia hati ya kiapo kutoka Mahakamani.

Mhe. Spika, kwa yoyote ambaye anahisi ananyimwa barua na sheha au cheti za kuzaliwa anatakiwa afike Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho ya wilaya yake na atapewa fomu nambari 4 ili akate furaa kwa Mkurugenzi, rufaa hiyo itashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni na iwapo mwananchi huyo hatoridhika na maamuzi ya Mkurugenzi basi anayo haki ya kukata rufaa kwa waziri, iwapo bado hataridhika na maamuzi ya waziri basi anaweza kwenda kudai haki yake Mahakamani. Huo ndio utaratibu uliopo.

Mhe. Spika, ni kweli kitambulisho kimeandikwa Kitambulisho cha Mzanzibari kwani hiyo ndio sifa kuu ya kuweza kusajiliwa na kupata kitambulisho hicho. Suala la ukaazi ni sifa kisheria iliyoainishwa kwa Mzanzibari anayestahiki

kupatiwa kitambulisho hicho. Aidha, kucheleweshwa kwa kutoa kitambulisho ofisi imetoa muongozo tangu mwaka 2008 kwa upande wa Pemba ni wiki mbili tangu siku aliyosajili na kwa Unguja ni wiki moja.

Mhe. Spika, mwaka jana lengo la kuwasajili Wazanzibari ikuwa ni 10,578 na mwaka huu ni 10,500; kigezo kilichotumika katika kupata kiwango hicho cha makadirio ni kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na kuangalia takwimu za miaka iliyopita katika *data base* yetu pamoja na taarifa za mtakwimu.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Ofisi ya Usajili haitambui hati ya kiapo ambayo haina nembo ya serikali au ya Mahakama. Muhuri wa Mahakama husika na sahihi ya hakimu au jaji aliyeapisha, hati za viapo zenye vigezo vilivyotajwa zinakubalika bila ya pingamizi na kuwa zile zenye kasoro mwananchi anaelekezwa utaratibu wa kufuata ili apate hati ya kiapo iliyo halali. Aidha, mikataba kuombewa shilingi 337,500/-, Ofisi ya Usajili inafanya kazi zake kwa kutumia kompyuta ambayo inajumuisha *hard ware and soft ware.*

Kulikuwa na suala la malipo ya kila mwaka, ili kuhakikisha kuwa shughuli za ofisi hii haziathiriwi na mabadiliko ya teknolojia au uharibifu, serikali imeingia mkataba na Kampuni ya *OTI* kwa ajili ya kutoa msaada wa kiufundi pamoja na *guarantee* ya mitambo na programu zake zinazotumika. Aidha, serikali imeingia mkataba na mshauri mwelekezi ambaye anatoa ushauri kuhusu mambo yanayohusu teknolojia ya habari. Mikataba hiyo hulipwa kila mwaka, aidha katika mwaka wa fedha uliopita Ofisi ya Usajili na Vitambulisho imebadilisha mitambo yote ya kuhifadhia taarifa na kutengenezea vitambulisho vilivyopo Makao Makuu ya ofisi hiyo.

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti haikuweza kubadilisha mitambo ya usajili iliyopo katika vituo kumi vya wilaya ambayo kwa hivi sasa ni chakavu na imeshapitwa na muda wake wa matumizi. Hivyo basi, ofisi inakusudia kuingia mkataba wa manunuzi ya mitambo ya usajili kwa ajili ya vituo vya wilaya. Fedha hizo zilizoombwa zinakusudiwa kutumika kwa ajili hiyo.

Mhe. Spika, shilingi thamanini milioni (80,000,000/=) zinazoombwa kwa ujenzi wa majengo ni kwa ajili ya Ofisi za Wilaya za Chake-Chake na Wilaya ya Kati hazina kabisa majengo ya kufanyia kazi. Kwa sasa wafanyakazi wa Ofisi ya Wilaya ya Chake-Chake na huduma za usajili zinafanyika katika kujibana kwenye ofisi ndogo ya Pemba, na kwa upande wa Wilaya ya Kati shughuli hiyo inafanyika ofisi ya vyumba viwili tulivyoazima katika majengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kati. Kutokana na hali hiyo ofisi inakusudia tuanze mchakato wa kujenga ofisi zake katika wilaya hizo.

Mhe. Spika, serikali haina nia ya kumnyima Mzanzibari yeyote haki yake kisheria. Taratibu zake zilizowekwa ni kwa nia ya kudhibiti udanganyifu, na kuhakikisha vitambulisho haviingii mikononi mwa watu wasiostahiki kila inapoyumkinika.

Ni vyema tusaidiane kuwaelimisha wananchi wetu ili wafuate taratibu zilizoekwa ili wapate haki yao kisheria. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane kulinda vitambulisho vyetu kwa mtu yeyote, ya kwamba kuna mgeni amepenya na kupata vitambulisho, tutoe taarifa mara moja kwa Mkurugenzi au Waziri ili ufanyike uchunguzi na hatua za kisheria zichuliwe mara moja.

Mhe. Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote kuhusu utendaji wa Baraza la Manispaa, nao ndio niliowaorodhesha pale mwanzo sitaki tena kuzungumza kwa urefu.

Ni kweli nje ya soko ya sehemu ya mbele ya njia kuingia kwa Doctor Haji kumekuwa na tope na hasa kwa siku za mvua. Manispaa imezingatia matatizo hayo na kutengeneza msingi wa maji ya mvua kwa kutia zege sehemu ya mbele, na hivi sasa inatumika kwa maegesho mbali mbali.

Aidha, Baraza la Manispaa limewasiliana na Idara ya Udhibiti wa Baraza kwa ajili ya kufanya matengenezo kwa kiwango cha kifusi tu, na matarajio yetu kwamba tope zitamalizika na kubakia historia tu.

Mhe. Spika, katika kuimarisha soko la Darajani na maeneo ya wazi, Baraza litashirikiana na vikundi vya jamii katika kufanya usafi nyakati za mchana, jioni hata usiku. Tunakubaliana na wazo kwamba tufanye kazi usiku kusafisha mji wetu kufuatana na hali halisi ya mazingira.

Mhe. Spika, wafanyabiashara wanaofanya biashara kinyume na utaratibu katika soko la Darajani, Malindi na Mwanakwerekwe, katika kuimarisha mazingira ya usafi wa maeneo hayo, Manispaa haina nia ya kuwanyanyasa au kuwasumbua bali inatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria ndogo ndogo za kuimarisha usafi wa mji wa maeneo ya wazi pamoja na masoko.

Manispaa itaendelea na juhudi zake za kuelimisha jamii pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa amani na utulivu. Tusingependelea malumbano haidhuru watu wetu wakienda kuwafahamisha wanapigwa mawe, wengine wanajeruhiwa, tukiwakamata ng'ombe wanapigwa na kufika kung'olewa meno. Sasa inakuwa vigumu kabisa. Ule wajibu wao askari wa Manispaa inakuwa haufanyiki, na matokeo yake ndio hayo Waheshimiwa munayozungumza biashara zinafanywa kiholela njiani, kila mtu zile sheria zilizoekwa hataki kuzifuata.

Hivi sasa zabuni ya ujenzi wa eneo hilo imeshatolewa tokea mwezi wa Mei mwaka jana. Hatua ya awali ilikuwa ni kutayarisha michoro na kibali cha ujenzi kimeshapatikana kutoka Mji Mkongwe. Wakati wa ujenzi huo wafanyabiashara watahamishiwa katika eneo la kuchinja kuku kwenye soko la mbogamboga Mombasa kwa dharura.

Mhe. Spika, hali ya usafi wa mji itaimarika kama nilivyosema awali baada ya kupatikana nyenzo na vifaa mbali mbali, ikiwemo gari tisa kwa Unguja na tatu kwa Pemba, na vizimba vya taka 193, *dust bins* 1500, mikokoteni ya taka 75 kupitia mradi wa uimarishaji wa huduma za mji.

Maelezo haya ya kina tumeeleza katika hotuba yangu kwenye ukurasa wa 43 hadi 45. Tumeonesha yale yaliyofanywa mwaka jana na yanayotarajiwa kufanywa mwaka ujao.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa mipango miji, eneo lililokuwepo kibanda ni eneo la matumizi ya wazi wala hapastahiki kujengwa kibanda cha kufanya biashara ya aina yoyote. Baraza la Manispaa limechukua hatua ya kuondosha kibanda hicho baada ya kubainika kuwa eneo hilo linatumika kinyume na matumizi ya mipango miji kwa kujenga kibanda cha nyumba ya kuishi, jambo ambalo limesababisha uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limekaa kikao tarehe 28 Juni, mwaka huu. Na ninakubaliana na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Rahaleo ya kujenga vyoo maalum vya kisasa (*movable toilet*) vitakavyoendana na hali halisi ya matumizi ya eneo lile. Na si busara kujenga vyoo vya kudumu katika eneo lile la Michenzani.

Mhe. Spika, bustani ya Forodhani inayosimamiwa na kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa maelekezo ya Bodi ya Kusimamia Bustani ya Forodhani ambayo inajumuisha Jumuia ya Agakhan, Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa katika uendeshaji wa shughuli zake.

Bodi imefungua akaunti maalum ambayo makusanyo yote yanayokusanywa hapo huingizwa katika akaunti hiyo kwa ajili ya matumizi. Fedha zinazokusanywa katika bustani hizo zinatumika katika matumizi ya umeme, upandaji na utunzaji wa bustani, ununuzi wa vifaa vya bustani, malipo ya maji ya kumwagilia bustani na malipo ya motisha kwa wafanyakazi, pamoja na malipo ya umeme ambapo maji na umeme peke yake kwa wastani hutumika shilingi milioni sita kwa mwaka.

Na ufuatao ni muhtasari wa mapato na matumizi kwa kipindi cha miaka mitatu. Kwa mwaka 2009/2010 mapato yalikuwa ni shilingi arobaini na tisa milioni, laki mbili mia saba na thalathini, matumizi yalikuwa ni arobaini na tano milioni laki nne na tisa, mia tano na thalathini na nne.

Mwaka 2010/2011 mapato yalikuwa ni shilingi milioni thalathini na saba, laki nne thalathini, matumizi yalikuwa ni shilingi milioni thalathini na mbili, laki nne tisini na sita elfu mia mbili na kumi na sita.
Mwaka 2011/2012 mapato yalikuwa ni shilingi milioni thalathini na nane, laki tano tisini na sita elfu, matumizi ni shilingi thalathini tatu milioni, laki nne na sabini na moja mia nne na tisini na nne.

Mhe. Spika, fedha zote hizo zinakusanywa na kusaidiwa na wafanyakazi wa Baraza la Manispaa na kuingizwa kwenye akaunti ya Bodi. Hata hivyo gharama za ziada kwa usafishaji, wahudumu wa bustani, walinzi pamoja na uchapaji wa risiti huchangiwa na Baraza la Manispaa pamoja na kupelekwa wafanyakazi 17 wa usafi na walinzi 6.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa halina nia ya kuleta usumbufu kwa utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara. Utoaji wa leseni unategemea mfumo wa kompyuta na taarifa sahihi za muombaji. Baraza linahakikisha muombaji

anapatiwa leseni si ya siku mbili isipokuwa pale panapotokezea matatizo ya umeme, kuharibika kwa mtambo wa kompyuta au kukosekana taarifa sahihi. Aidha, Baraza linaomba mfanyabiashara anayeomba leseni afike mwenyewe badala ya kutumia wakala, ili kurahisha upatikanaji wa taarifa sahihi.

Mhe. Spika, usafi wa mji na misingi ni jukumu la wananchi sote na sio Baraza la Manispaa peke yake. Baraza la Manispaa katika kukabiliana na hali hii limeanzisha utaratibu wa ushirikishwaji wa vikundi vya jamii na mazingira kwa mashirikiano ya Masheha na Madiwani.

Aidha, ninawaomba wananchi kuacha tabia ya kutupa taka ovyo hasa nyakati za mvua katika misingi ya maji machafu na kusababisha misingi kuziba na kuleta mafuruko yasiyokuwa ya lazima. Ufanisi wa usafi wa mji ni pamoja na usafi wa misingi na unategemea zaidi mashirikiano zaidi ya Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge katika kuielimisha jamii na kuitaka kubadilisha tabia na kuongeza ari ya kujitolea na kuheshimu taratibu na kanuni.

Mhe. Spika, tunamshukuru Mhe. Dimwa kwa ule msingi wake au mtaro wake wa Mpendae kwa ile sehemu aliyochangia. Tunamshukuru na sehemu hii huku nyengine tumeimaliza sisi, na tunamuahidi kwamba mradi huo utaweka sawa suala lake la maji, kuanzia huko kwa Binti Amrani mpaka Kilimani.

Mhe. Spika, mradi wa huduma za ZUSP, ni mradi ambao umepangwa kutekelezwa kuanzia 2011 mpaka 2016. Kwa mujibu wa utaratibu wa mpango huo mradi umegawika katika awamu tatu. Awamu tuliyonayo hivi sasa ni utaratibu wa matayarisho ya kuwatafuta washauri kitaalamu pamoja na wakandarasi wa ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua kuanzia Magomeni Mzalendo, kupitia kwa Binti Amrani unatarajia kuanza mwishoni mwa mwaka huu.

Mhe. Spika, tunaomba Mheshimiwa kuwa na uvumilivu tusubiri utekelezaji wa mradi huu na una muda wa miaka mitano. Ni vyema kuona serikali ina nia ya kudanganya, wala haina nia hiyo. Wananchi tuwe karibu tuwafahamishe malengo ya serikali.

Mhe. Spika, mtaro wa Mpendae Wawi umetengenezwa kufuatia kusuluhisha mzozo baina ya wadi mbili za Mpendae na Meya ili kupata suluhisho la muda kwa Waheshimiwa Madiwani. Katika suluhu hiyo Mhe. Mwakilishi alishiriki kikamilifu kama nilivyosema kuchangia wazo hilo na kuahidi kuchangia gharama kwa thamani itakayofikiwa ya matengenezo.

Gharama ya matengenezo imefikiwa shilingi milioni 18 na Mhe. Mwakilishi kuahidi kuchangia nusu ya gharama hizo. Juhudi za Mhe. Waziri kufanikisha baadhi ya vifaa vya mtaro na Afisi Kuu ya Kisiwandui kupitia kampuni za wafadhili zimefanikisha kazi hiyo, pamoja na fedha za Baraza la Manispaa baada ya kukosekana msaada huo kwa Mhe. Mwakilishi wa Mpendae.

Vile vile nisisitize mitaro ya maji ya mvua kutoka Mwanakwerekwe *round about* kwendea Kiembesamaki, kupitia kwa Binti Amrani unatengenezwa na Idara ya UUB kwa hifadhi ya barabara inayoharibika kwa kutumia maji ya mvua, na sio ujenzi wa mradi wa Manispaa badala yake mradi utakapoanza Baraza la Manispaa utaunganisha msingi huo na mradi mkuu ZUSP.

Mhe. Spika, serikali kupitia Baraza la Manispaa haishindwa kuendeleza eneo la biashara la Saateni. Juhudi zinaendelea kuimarishwa kwa awamu kwa mujibu wa fedha za Baraza la Manispaa. Manispaa imejenga mtaro wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 160. tumesambaza umeme, tumetengeneza maegesho kwa kiwango cha kifusi katika bajeti ya mwaka huu 2012/2013, na tunaendeleza ujenzi wa uzio wa ukuta wa kuimarisha usalama wa eneo hilo na kituo kidogo cha Polisi kwa ajili ya kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao.

Vile vile utaratibu wa kuwashirikisha wadau kama Idara ya Usafiri na Leseni, Vyama vya wamiliki wa daladala, magari ya shamba, Polisi, Afisi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya, ili kuhakikisha magari ya abiria yanashusha abiria eneo la Saateni badala ya Darajani, ili kuchochea biashara katika eneo hilo kwa mujibu wa wafanyabiashara.

Mhe. Spika, ni kweli mradi wa bustani wa Forodhani ulikuwa ujenzi wake ufanyike sambamba na uzio wa Forodhani, lakini utekelezaji wake haukufanyika kutokana na sababu ambazo Agakhan wenyewe wanazijua, na ilikuwa ni maamuzi sio kwa mradi huo tu bali ilikuwa kwa miradi yote ya Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, serikali imeamua kuendeleza mradi huo kupitia mradi wa huduma za jamii (ZUSP).

Kwa hivyo hadidu rejea kwa ajili ya kutafuta wataalamu wa kuendeleza mradi huo tayari zimeshatayarishwa na kuthibitishwa na World Bank kwa kuajiri mshauri wa kitaalamu kwa ajili ya ubunifu wa uhandisi na usimamizi wa kazi za ujenzi. Mradi wa huduma za mji umeelezwa katika hotuba ya bajeti ya mwaka huu katika Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye ukurasa wa 43 hadi 45.

Mhe. Spika, tulipoainisha wazi michoro ya jengo la mapato la Manispaa ni kwa ajili ya jengo la mapato liliomo ndani ya Afisi Kuu Darajani, na sio kwamba itajengwa eneo la makontena Darajani kama alivyofahamu Mhe. Hija Hassan Hija.

Ni sahihi barua ya tatu kwa wawekezaji mbali mbali waliomba kuendeleza eneo hilo la kujenga uchumi kwa Manispaa, wakiwemo wazalendo kama Omar Babu pamoja na kampuni ya *Kiboko limited* kupitia jumuia ya makontena wazalendo na kampuni ya *Hot Property limited* ya wazalendo iliyosajiliwa Zanzibar yenye makao makuu nchini Uingereza.

Hata hivyo barua zimetolewa kwa misingi ya kuwakubalia maombi yao, ili wajiandae na mchakato wa taratibu zinazofuata ikiwemo Bodi ya Zabuni kupitia Kamati za Madiwani na Kamati ya Zabuni ya Manispaa, ambapo wote tayari wameshawasilisha michoro yao si Wataliana peke yake. Zingatio kwamba tangazo lilivyotoka maombi yanakubaliwa na barua za majibu zinatolewa kila zinapopokea maombi yao kama wanavyowasilisha wenziwao, na pale hatua zinapokamilika za kumpata mwekezaji halisi wa kufanya hiyo kwa sheria na taratibu za Manispaa, tutazingatia uwezekano wote wa kuwezesha kutoa kipaumbele kwa wafanyabiashara wazalendo waliopo hivi sasa kwa taratibu za kisheria za Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi inaendelea na jitihada ya kusafisha majaa ikiwemo jaa la Kwamchina kwa kuondosha taka taka katika majaa hayo kila siku asubuhi, na kufanya operesheni zoezi la kuondosha taka kwa kutumia *grader* na kijiko kila baada ya miezi mitatu.

Hata hivyo changamoto kubwa inayotukabili ni watu au vikundi binafsi vinavyokusanya taka katika maeneo mbali mbali na kuzitupa na kuzichoma moto wakati wa usiku muda sio wa kazi, hivyo kusababisha kero ya moshi kwa wakaazi wa eneo hilo. Ninamuhakikishia Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi itaendeleza juhudi zake hizo za kutoa elimu itakayosaidia kutatua tatizo lililokuwepo la wananchi au vikundi vya kijamii.

Mhe. Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi waliochangia suala la Wazanzibari wanaoishi nchi za nje. Wazanzibari wanaoishi nchi za nje wanachangia katika uchumi wa nchi kupitia fedha wanazozituma na kusaidia katika sekta za jamii. Aidha mpango mkakati wa Wazanzibari hao ambao tayari umeshatayarishwa unatoa dira ni kwa namna gani Wazanzibari wanaoishi nchi za nje watahamasishwa kuwekeza na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mhe. Spika, uraia wa nchi mbili ni jambo la Kikatiba na bado halijatolewa uamuzi. Jambo hili litaweza kujadiliwa na kupatiwa uamuzi wakati wa hotuba ya maoni ya Katiba mpya. Aidha kuwashirikisha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje na kutoa maamuzi ya kuchagua viongozi Watanzania ni jambo la Kikatiba.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 cha sheria Na. 12 ya 1992 kinasema kwamba, “Kila nyumba, ardhi iliyochukuliwa na serikali baada ya mwaka 1964 itakuwa imetaifishwa na kuwa ni mali ya serikali”.

Mhe. Spika, ziara za Falme za Kiarabu ninafikiri na ninamshukuru sana Mhe. Haroun hii ametusaidia, amejaribu kueleza yale makubaliano yaliyofikiwa kule.

Mhe. Spika, ziara za Falme za Kiarabu zimeshirikisha Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Benki ya Watu wa Zanzibar, hivi majuzi tu Mamlaka ya Vitega Uchumi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Shirika la Bima la Zanzibar. Katika ziara hiyo makubaliano yaliyofikiwa baina ya Benki ya Muscat na Benki ya Watu wa Zanzibar kushirikiana katika shughuli za kibenki pamoja na kuwajengea uwezo maofisa wa Benki ya Watu wa Zanzibar.

Pili kutafunguliwa *collection account* katika Benki ya Muscat ambayo itatumiwa na Wazanzibari wanaoishi maeneo hayo kwa ajili ya kutuma fedha zao Zanzibar. Na mwisho kuandaliwa ziara ya kiserikali itakayowahusisha viongozi wakuu wa serikali ambao itawakutanisha Jumuia ya Wafanyabiashara wa Oman, Jumuia ya Wafanyabiashara wa

Zanzibar, Mamlaka ya Vitega Uchumi ya Oman katika kipindi kifupi kijacho. Aidha fursa hii itatumika kwa ajili ya kukutana na Waoman wenye asili ya Kizanzibari.

Mhe. Spika, nipo mwishoni mwishoni. Sheria Na. 5 ya mwaka 1983 ya Usalama wa Taifa inayosimamia uendeshaji wa kazi za ukaguzi na upekuzi haina mapungufu (GSO). Aidha sheria imeweka adhabu kwa wale wanaopatikana na makosa ya utumishi hususan makosa ya kughushi vyeti, ambapo mtu atakapopatikana na kosa la kudanganya katika taarifa zake anatakiwa ashushwe cheo, afukuzwe kazi au asimamishwe kazi. Aidha utaratibu unaopeleka maombi ndio inayotumiwa wajibu, na wala sio mtu aliyepekuliwa kupewa majibu ya upekuzi.

Mhe. Spika, Kitengo cha GSO kipo kabla ya Afisi ya Rais ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sheria ya Utumishi ya mwaka 2011 imesisitiza tu majukumu ya kitengo kusimamia utumishi lakini kutokana na maadili ya kutunza siri za serikali, kitengo hakiwezi kuunganishwa na taasisi nyengine. Aidha kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma Na. 2 ya mwaka 2011 kitengo kinawajibika moja kwa moja kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe. Spika, sheria ya uhaulishaji imempa uwezo Sheha kukusanya shilingi ishirini elfu kwa ajili ya matumizi ya ofisi ikiwemo vifaa vya kuandikia. Sheria nyengine za usajili ya Mzanzibari Mkaazi imempa uwezo kupokea shilingi mia tano kwa ajili ya mchango, vifaa vya kuandikia pamoja na utoaji wa kopi.

Mhe. Spika, ninamjuulisha Mhe. Farida kwamba jumla ya semina nne ambazo zimewashirikisha Waheshimiwa Sheha na Madiwani, Unguja mbili na Pemba mbili, juu ya majukumu ya kiutendaji kwa shughuli zao za kazi za kila siku katika mwaka 2011/2012.

Aidha semina elekezi ya siku mbili kwa watendaji hao kwa upande wa Unguja kama nilivyosema awali ilifanyika chini ya Mwenyekiti Rais wa Zanzibar hivi majuzi tu. Semina kama hiyo inatarajiwa kufanyika Pemba baada ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Spika, Mhe. Asaa ninamjuulisha kuwa Baraza la Mji Mkoani limetenga jumla ya shilingi kumi na tatu kufanya matengenezo soko la Mkoani. Aidha soko la Baraza la Mji la Wete liliopo pwani ya Wete limefanyiwa matengenezo na limegharimu jumla ya shilingi milioni tano.

Vile vile mradi wa ZUSP katika vipaumbele vyake vimeazimia kujenga soko la Baraza la Mji Chake-Chake na ujenzi wa soko jipya katika eneo la Machomanne. Soko la samaki la Chake-Chake litafanyiwa matengenezo pia. Pia Baraza linategemea kujenga soko la matunda litakalogharimu shilingi milioni mia nne kupitia mradi wa kilimo.

Mhe. Spika, soko la Micheweni limefanyiwa matengenezo katika sehemu ya Afisi ya soko kwa azma ya kuwapatia vijana ushauri nasaha pamoja na kupima virusi vya Ukimwi, pia kutumika kufanyia mikutano ya viongozi mbali mbali. Ghala ya chakula imeanzishwa na Tume ya Uchaguzi na ambamo wanatumia kwa kuwekea vifaa vyao baada ya kufanyiwa ukarabati.

Pia miradi ya maendeleo iliyolikamilika ni mradi wa ujenzi wa tangi la maji Gongoni ambao upo Shehia ya Kiuyu Minungwini na Maziwa Ng'ombe. Mradi wa skuli ya sekondari Sheria za Chwaka, Tumbe na Konde. Mradi wa ujenzi wa kuzuia maji chumvi uliopo bonde la Ukele.

Miradi ambayo haijakamilika ni mradi wa ujenzi wa njia ya Mapofu Finya hadi Kinyasini, mradi wa njia ya Konde/Wete, ujenzi wa skuli ya msingi ya Sinai, mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Kifundi, ujenzi wa soko la samaki Tumbe, Micheweni na ujenzi wa maabara Micheweni.

Mhe. Spika, ninachukua fursa hii kumjuulisha Mhe. Mohamed Haji ajira kwa Halmashauri za Wilaya. Kimsingi shughuli za Mabaraza ya Miji za Halmashauri Pemba zinaratibiwa na kusimamiwa na Afisi ya Afisa Mdhamini. Wakuu wa taasisi hizo, Makatibu wa Mabaraza ya Miji na Makatibu wa Halmashauri za Wilaya waliowasilisha maombi yao ya ajira Afisini kwa Afisa Mdhamini, na walichelewa kuwasilisha maombi yao kwa ajira Afisini kwa Afisa Mdhamini. Hatua za maombi hayo zilipokelewa taratibu za uajiri zimeshabadilika, yapo maombi yamepokelewa.

Kwa mujibu wa sheria Na. 11 ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi Serikalini imepewa mamlaka ya kuajiri na sheria hiyo badala ya Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa taratibu mpya za uajiri ndizo

zinazopelekea hadi leo kuwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya Pemba hazijaweza kuajiri wataalamu wa kada hizo. Hata hivyo hatua za maombi za ajira zimeshatumwa Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa hatua, na tunasubiri kauli ya serikali juu ya uajiri na kujaza nafasi hizo. Na alhamdullahi Mhe. Waziri na wizara kwa jumla na hili linafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, Asha Bakari Makame na yeye alitaka maelezo ya kujua sababu gani zilizopelekea kutolipwa tofauti za mishahara kwa wafanyakazi wa Baraza la Miji na hili nimeshalieleza. Afisi imechukua hatua ya kuomba tofauti hizo Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, na hatua juu ya majibu ya tofauti hizo imeshatolewa. Hatua iliyobaki ni juu ya kulipwa tofauti hizo na vocha za maombi hayo zimeshawasilishwa Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kunatarajiwa kulipwa mwezi huu wa Julai mwishoni mwa mwezi.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Asaa walitaka ufafanuzi kwa baadhi ya vifungu vya fungu Na. 8 la Afisi ya Baraza la Mapinduzi kuongezeka. Mafuta yameongezeka kutokana na kuongezeka shughuli ambazo zinalazimilika kutumika mafuta. Vikao vya Baraza la Mapinduzi pamoja na kamati zake zimeongezeka kwa zaidi ya marudufu ambapo sekeretarieti ina wajibu wa kuwasambazia nyaraka Wajumbe wote wa Baraza, wajumbe wote wa Kamati ya Makatibu Wakuu na kamati nyenginezo za BLM, ikiwemo kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Jamii.

Pia gharama hizo zimeongezeka kutokana na matarajio ya kupokea wageni wengi kwa ajili ya mkutano mkuu wa *African Association for Public Administration and Management* unaotarajiwa kufanyika katika mwezi wa Novemba mwaka huu hapa Zanzibar.

Aidha gharama za matumizi madogo madogo ya Afisi ya Baraza la Mapinduzi yameongezeka kutokana na kujumuisha kimakosa malipo ya *political vote* za Waheshimiwa Mawaziri wasio na Wizara Maalum ambapo Afisi ya Baraza la Mapinduzi imebahatika kuwa na Mawaziri watatu kwa wakati mmoja.

Gharama hizo za *political vote* zilipaswa ziende kwenye kasma 272100 kinachohusu misaada ya kijamii. Jumla ya shilingi milioni kumi na nane zilizokuwepo zinapaswa kuwepo kasma ndogo 272108 inayohusu kushughulikia shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri jitahidi ufikie angalau saa sita tumalize.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, *interruption* yako imekuja kwa wakati na niseme tu kwamba baada ya maelezo haya mengi na ningependa niongeze zaidi lakini muda hautoshi, basi naomba niwashukuru sana Waheshimiwa kwa kunisikiliza. Tumejitahidi kwa upande wetu, kwa niaba ya wenzangu kwa kufanikisha haya majumuisho.

Lakini ninarudia tena masuali yenu ni mengi, maelezo tumeyachukua na tutayafanyia kazi. Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuweza kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 17 JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja shs.22, 500,000,000/=
Jumla ya Fungu **shs.22, 500,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 Idara ya Vyuo vya Mafunzo shs.41, 000,000,000/=
Jumla ya Fungu **shs.41.000,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 07 OFISI YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NCHI ZA NJE

Kifungu 0601 Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa

Mhe. Ismail Jussa Ladhu:Naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu na ufafanuzi wa hoja zetu mbali mbali tulizozitoa hapa, ametoa ufafanuzi wa kina tunamshukuru. Lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo bado labda kwa sababu ya kumuhimiza alikuwa hakuyafikia, hasa pale mwisho.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba katika hoja zangu Mhe. Mwenyekiti, nilizozitoa kwenye vifungu mbali mbali ambavyo nilihoji uhalisia wa kasma zilizowekwa. Pia nilihoji fungu linalohusu manunuzi ya TV katika maeneo mbali mbali, na hapa pia lipo katika ukurasa wa 104 *vote* – 311200 kuhusu ununuzi wa mashine na zana, *sub vote* 311214 ununuzi wa televisheni shilingi 40,000,000/-. Sasa nilikuwa naomba hili lisimuhangaishe huko mbele, alijibu kwa pamoja kwamba hizi hesabu za TV za shilingi 40,000,000/- ambazo zinazojitokeza mara nyingi katika Idara zake mbali mbali, atuambie ni TV gani iliyokuwa ya thamani hiyo ya shilingi 40,000,000/-. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. vote

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hapa sio ununuzi wa TV peke yake, ni vifaa vile vyote vya kurikodia, *printing* na hiyo TV ni *item* moja tu. Hilo ni kosa la *printing error* kusema TV, ni vile vitu vyote vya kurikodia na vyenginevyo, sio TV peke yake hapana, ni kosa hilo. Kweli limeonekana kwengine sio hapa. Lakini hasa sio ununuzi wa TV peke yake, ni ununuzi wa vile vifaa vyote kamili vya mambo haya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nasikitika kwamba sikubaliani na maelezo ya Mhe. Waziri kwa sababu bahati mbaya sikushiriki mafunzo ya juzi, lakini naambiwa moja katika yale mafunzo ni kwamba *vote* hizi hasa katika ile *sub item*, kile kilichoandikwa pake ndicho ambacho kimekusudiwa sio zaidi ya hapo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, fungu hili au *vote* hii inazungumzia ununuzi wa mashine na zana, halafu zimechambuliwa moja moja. Kuna ununuzi wa gari, kuna ununuzi wa kompyuta na halafu kuna hiyo ninayoisema 311214 ununuzi wa televisheni, basi imeishia hapo, kwa Kiingereza imeandikwa *purchases of television* 40,000,000/-. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hili sitaki kumsumbua sana, linajirejea pia katika Idara zake mbali mbali, unakuta televisheni shilingi 25,000,000/- na nyengine televisheni shilingi 40,000,000/-. Najiuliza ni TV gani inayogharimu shilingi 40,000,000/-, hata kama itaambatana na *plug* na waya zake bado siamini kama kuna TV ya shilingi 40,000,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atupe maelezo ya kina, kwa sababu hizi ni fedha za walipa kodi wa Zanzibar, hivyo zinahitajika ziwe na mahesabu mazuri hapa, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kutaka ufafanuzi. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hiyo ilikuwa ni *printing mistake*, hasa kilichokusudiwa hapa ni ununuzi wa *generator* kwa hizo shilingi 40,000,000/-.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu haya maelezo yanabadilika badilika, na hatujui hasa Waziri anatuomba kitu gani. Kwa hivyo, mimi naomba atukubalie kifungu hiki tumzuilie, kwa sababu hajui hasa kifungu cha 40,000,000/- kinataka nini. Kwa hivyo, hatuwezi kupitisha hapa kama Wawakilishi wa wananchi tunaosimamia kodi zao na fedha zao, fedha ambazo Waziri mwenyewe mwenye dhamana hazijui. Katuambia mara anataka kununua kompyuta na vifaa vyengine, na sasa hivi anatuambia *generator*. Kama ni *printing error,* nadhani utaratibu Mhe. Mwenyekiti, kama kuna *printing error* tunaletewa marekebisho. Hatuwezi kupitisha vifungu chini ya maelezo ya jumla jumla kama haya.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri hajajiandaa basi kifungu hiki, kutokana na mafunzo mazuri uliyowapa Wajumbe wenzangu, na mimi sikushiriki, lakini wamenisaidia, hivyo kifungu hiki cha milioni 40 tukifute mpaka hapo atakapokuwa kapata maelezo, mwakani atuletee tutampitishia kununua TV. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alitaka maelezo ya vifungu mbali mbali, na katika kifungu hiki hasa kwenye utoaji wa zawadi, safari za nje, ada ya washauri, gharama za huduma za malazi. Hapa na utoaji wa zawadi ni milioni 53 jumla ya kifungu na ununuzi wa gari 104, hilo ni jenereta tu.

Mhe. Mwenyekiti, nimekiona hapa. Naomba kumfahamisha Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba hili ni kosa hapa, hii sio ununuzi wa TV. Hizi 40,000,000/- zilizowekwa hapa ni ununuzi wa jenereta hiyo ni hakika. Sasa kama anafahamu vyengine, mimi sijui. Lakini ninachosema, hiyo *printing* iliyoandikwa hapa ni *wrong*, sio ununuzi wa TV. Imeandikwa *purchasing of television* ni *wrong* ni *purchasing of generator* hiyo ndio sahihi. Sasa ni ununuzi wa *generator*, hiyo ndio sahihi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kinachozungumzwa ni kwamba kulikuwa kuna koseo juu ya *sub vote* hii, kwamba makusudio hasa ni ununuzi wa jenereta na sio televisheni.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hili utusaidie wewe. Kwa sababu hapa tuko katika Kamati ya matumizi hivi sasa na kamati ya matumizi inachojadili ni kile ambacho serikali imekileta hapa. Sasa hatuwezi kupitisha marekebisho ambayo yanafanywa kwa mdomo saa hizi Mhe. Mwenyekiti, sio utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua, utaratibu ni kwamba na hata kwenye *briefing* tuliletewa, ingawa tulilalamika, lakini angalau tuliletewa marekebisho. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii haikuwa *trained.* Tulipopitisha Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza kulikuwa kuna marekebisho hivyo hivyo ambayo sisi hatukugaiwa, tukasomewa na tukakubali. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea na utaratibu kama huu.

Pili, hata katika Kamati naambiwa na Wajumbe wa kamati suala hili hakulisema, halikujitokeza. Fungu lililojitokeza hapa ni kama lilivyojieleza hapa kwamba hii ni matumizi ya televisheni.

Kwa hivyo, nasema kama anataka kununua jenereta, basi mimi nadhani tukubaliane tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hilo atatuletea mwakani tutampitishia, kwa mwaka huu akubali hizo milioni 40 tuziondowe. Kwa hivyo, katika bajeti hii ya 884,000,000/- ya Ofisi ya Ushirikiano wa Kimataifa tupunguze 40 milioni za televisheni, kisha mwakani tutampitishia atakuja kununua jenereta tukijaaliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi naiona *concern* ya Mhe. Ismail Jussa, lakini nataka nimwambie kwamba hili buku zima akilisoma katika ukurasa wa mbele, ataona kwamba tumezungumzia *draft* buku zima hili. Kwa hivyo, makosa ambayo yanaonekana hapa ndio pahala pake pa kurekebishwa, halafu baadae tunakuja kumuuliza Mhe. Waziri kwa kupitia kamati ya PAC kwamba kifungu hiki ulituambia kuna milioni 40 ya jenereta, jenereta iko wapi. Lakini hapa ndio pahala pake pa kurekebisha. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Jussa akubali hayo marekebisho, ili kifungu kiweze kuendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namuheshimu na najua kuwa ni kaka yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, lakini nasikitika kusema au kwa lugha ya Mji Mkongwe *nataasaf* kusema huo sio utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, buku hili na mara nyingi tumekuwa tukisema hata ukiliandika *draft estimate,* hili linapaswa liwe *draft estimate* mpaka litakapopitishwa ndani ya Kamati. Mara nyingi tunasema, kwamba linapofikia kiwango cha kuletwa hapa, basi halipaswi tena kuwa ni *draft.* Haya baada ya kuwa kamati zimepitia na zimeridhika. Ndio maana kwa wenzetu wana mabuku matatu Bungeni, lakini yanarekebishwa na inapofika kwenye bajeti, kwa sababu hiki ndio kiongozi chetu kama wasimamizi wa walipa kodi, kupitishia fedha za wananchi hapa na kwenda kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba kama tungekuwa makini, basi tungefanya marekebisho. Nitatoa mfano. Sisi katika kamati yetu ya Katiba, Sheria na Utawala, tulikuwa na matatizo na Kamisheni ya Utumishi, lakini Mhe. Waziri anayehusika tulipokwenda kwenye kamati, akatoa marekebisho na mimi ninayo hapa ya Kamisheni ya Utumishi, naamini itakapokuja hapa tutagaiwa ili tufanye marekebisho.

Vile vile siku ya kuchangia bajeti kuu hapa, nilihoji mimi Mhe. Mwenyekiti, kwamba vile vifungu vya matumizi katika kasma moja moja havikutimia katika buku. Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alipokuja kufanya majumuisho, kabla hajaja mbele pale alitugaia, kwa hivyo tulipopitisha tulipitisha kitu tunachokielewa.

Kwa hivyo, hatuwezi Mhe. Mwenyekiti, halafu sio utaratibu kwa dunia nzima chini ya Mabunge ya Jumuia ya Madola, kuwa na *estimate* ambazo Waziri anakuja kurekebisha hapa tukasema tunapitisha, huo sio utaratibu wala sio usimamizi mzuri kwa walipa kodi wanyonge wa nchi hii, maskini wanakamuliwa halafu fedha zao zinatumiwa vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema tukubali kabisa, kwamba hili kama ni kompyuta au jenereta kwa mwaka huu hajajiandaa, basi tuzipunguze hizo shilingi 40 milioni, kisha mwakani atatuletea bajeti ya jenereta tutakuja kumpitishia Mhe. Waziri. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tufuate utaratibu, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa hebu tuangalie hali halisi. Hali halisi Waziri anasema kwamba wamekosea, haikuwa ununuzi wa televisheni, isipokuwa ni ununuzi wa jenereta ndicho anachokizungumza. Ni kweli tulitegemea kwamba kama kuna makoseo, nadhani hii iwe ni muongozo pia kwa wizara nyengine, tuende kwenye hili buku tuwe tunapitia mapema, ili tukija hapa tuwe na uhakika wa kitu gani tunakiomba. Ni suala muhimu sana hilo. Kwa sababu hapa kamati hii ya matumizi ina uwezo wa kupunguza fungu kwa mujibu wa kanuni zetu, ilichokuwa haina uwezo ni kuongeza fungu kwa mujibu wa kanuni hizo.

Sasa busara iko kwenu Waheshimiwa Wajumbe, kuona je hii anayosema kwamba ni sahihi, kuna haja ya kununuliwa jenereta ndio anachokisema hapa, tunakubali akanunue jenereta tuje tumdai huko siku za usoni, au tunafanyaje, au asinunue kabisa. Kwa sababu hapa haja ni kitu hiki anachosema sasa ndio sahihi kinahitajika. Kwa hivyo, ni kwetu sisi kumpa ruhusa akanunue hilo jenereta aje tumdai, au tumwambie mara hii ndio imekwenda ajuari usinunue, tukimwambia usinunue maana yake fungu hili ndio linapungua hili. Utendaji wa huko utakuaje, hilo sasa ndio tunaweza tukazingatia na Mawaziri mnaweza mkasema, tutapungukiwa nini kama jenereta halikununuliwa mwaka huu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninavyoelewa mimi ni kwamba kunakuwa na fungu la gharama nyenginezo. Kwa hivyo, kama kuna kitu walichokuwa hawajakiona watatumia fungu hilo, lakini kwa fungu hili mimi naomba kwa leo tutumie utaratibu huu kuweka nidhamu katika matumizi. Nasema kwa kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, niwaombe Wajumbe wenzangu, tuweke fundisho kwa matumizi na nidhamu zake kwa fedha za walipa kodi, shilingi milioni 40 ziondolewe katika fungu hili Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka wakati Mhe. Ismail Jussa alipochangia katika hotuba ya Makamo wa Pili au Makamo wa Kwanza, tulifikia pahala tukasema hili buku mwaka huu limekosewa sana, nakumbuka. Sasa na tukasema litarekebishwa na wenyewe wakasema tutalirekebisha. Kwa hivyo, ninachotaka kusema kwamba utakuta humu hili buku bado liko Ofisi ya Waziri Kiongozi na mengineyo, yaani kuna marekebisho mengi ambayo yanataka kufanywa kwenye hilo buku.

Mhe. Mwenyekiti, hata kwenye huu ukurasa wa kwanza hapo wa 101, imeandikwa vifungu vya fungu hili vinavyooneshwa hapa chini matumizi yake yatatumiwa na Katibu mkuu Ofisi ya Ushirikiano wa Kimataifa wa Kuratibu Wazanzibari. Hii ni ya mwaka jana haipo hii, huyu Katibu mkuu wa ushirikiano wa kimataifa kuratibu Wazanzibari hayupo. Kwa hivyo, ndio nasema bado kuna marekebisho mengi katika buku hili, kwenye *set up* yake

Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tuliwatanabahisha, wakasema wao wanaangalia kuanzia mwakani yote wataya-*clear*.

Kwa hivyo, huyu ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ndiye atakayesimamia kifungu hiki tunachokipitisha. Sasa nataka kusema makosa bado yamo, lakini kama ulivyosema Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio mahala pale kabla hatujapitisha tuna *pin point* makosa kwa kurekebisha, halafu hapa tena kinachopita ndio kimepita. Sasa mimi namshauri tu na ninakubali hayo mawazo yake Mhe. Ismail Jussa kwamba kweli, nafikiri niliisahihisha sehemu nyengine lakini hii sikuiona, hatuwezi kununua televisheni kwa shilingi milioni 40, hiyo ninayomuambia mimi ndio mwenye Wizara na nimeshahakikishiwa kuwa hili ni kosa. Ni ununuzi wa jenereta, iwe ni asilimia mia juu ya moja.

Kwa hivyo, wacha Mhe. Mjumbe atuachie tukaone, kamati ipo ya PAC itatumika wapi hii fedha, tutanunua jenereta aje afuatilie aone, lakini kuzuia kifungu kuwa tusitumie nafikiri ningeomba busara tu atumie Mhe. Mjumbe, ningemuomba sana Mhe. Ismail Jussa.

Mhe. Mwenyekiti: Baada ya maombi hayo Mhe. Ismail Jussa, kwa sababu kiti kazi yake baadae ni kusema tu kwamba je, tumruhusu akanunue jenereta kama alivyotaka marekebisho au kuna maombi mengine ya serikali. Kiti kazi yake ni kusema kwamba haya wale wanaosema tumruhusu wanyanyue mkono na wale wanaosema tusimruhusu wanyanyue mkono.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema, kabla sijatoa kauli yangu ya mwisho, nataka kusema *observation* moja. Mhe. Waziri ni waziri mzoefu sana katika Baraza hili, sasa akilitia dosari buku hili akasema lina majumuisho ya Ofisi ya Waziri Kiongozi, mimi ambaye ni mwanagenzi katika Baraza hili nitapata tabu sana, kwa sababu suala hili niliwahi kuliuliza mimi niliyekuwa mwanagenzi, nikasaidiwa kwamba hizi *vote* huwa mpaka zifikie miaka mitatu ndio zinaondoka *automatic*. Sasa kwa Waziri ambaye keshakuwa Waziri wa Fedha na Uchumi, ikiwa hilo halifahamu, leo anatumia kama ndio kutetea hoja yake, inatusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, buku hili halikuandaliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi *back benchers*, hili limeandaliwa na serikali, na serikali iliyowajibika hapa kwa pamoja, *collectively responsible.* Sasa kama wametuletea buku lenye makosa ni kwamba wao wanataka kulipotosha Baraza hili lipitishe mafungu kimakosa, jambo ambalo sisi hatuwezi kulifanya Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema mengi tunaridhia kama nilivyosema, lakini kwa hili nasema 40 milioni kama kuna sehemu nyengine wataweza kuzipata, kila Idara ina fungu lake la matumizi mengineyo. Lakini kwa hili Mhe. Mwenyekiti nasema, kamati ya matumizi iache itekeleze wajibu wake kwa mujibu wa kanuni, ipunguze fungu hili la 40 milioni. Kwa mawazo mengine itakuwa ndio fundisho, kwamba kama kuna marekebisho au kama kuna sehemu imekosewa, wakati watakapowasilisha bajeti zao watatuwasilishia marekebisho hayo, wakati tunakaa kama kamati ya kupitisha vifungu, tutakuwa tunapitisha na marekebisho tuliyoletewa, lakini hatuwezi tukafanya marekebisho hapa saa hizi, wakati ameondoka sasa hivi kufanya majumuisho hakutufanyia marekebisho hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba *concern* katika hili, tupunguze 40 milioni, tuweke fundisho kwa serikali katika matumizi.

Mhe. Mwenyekiti: Haya. Kuna maombi yoyote kwa serikali. Niwaulize basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubali. Hee haya Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi. Kuna waraka huu ulitolewa na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kujaribu kusahihisha hili. Sasa katika kuupitia na tutizame kuna fungu hili hili ambalo huku, limeandikwa kweli ni jenereta, kama hivyo anavyosema Mheshimiwa. Lakini kinachotoa uzito ni kwamba na hiyo *data* ya huku nayo imekosewa, lakini kweli ni jenereta. Katika ukurasa wa 12 wa hii aliyoisahihisha.

Samahani, sasa hii inaonesha kwamba kweli kuna makosa, kwa sababu hata hii iliyosahihishwa nayo inasema ununuzi wa televisheni, lakini huku 141 milioni ambayo haiwezekani, kwa hivyo bila shaka kuna kosa la msingi, tumefahamu. Kwa hivyo, anachokisema Mhe. Waziri kwamba imekosewa ni kweli imekosewa. Sijui nimeeleweka.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Afya, unatuchukua kwenye

Mhe. Waziri wa Afya: Samahani. Nilichotaka kuthibitisha kwamba anachosema Mhe. Waziri kwamba hii imekosewa ni kwamba imekosewa kweli, kwa sababu hata hii waliosahihisha wenzetu ambayo ni hii, huku bado wameandika ununuzi wa televisheni. Hivi kuna televisheni inayonunuliwa kwa milioni 141. Kwa hivyo hii ni kuthibitisha kwamba imekosewa. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tumefahamiana. Waheshimiwa Wajumbe, kasma inayozungumziwa kwamba imekosewa ni kasma nambari 311214, ambayo maelezo ya matumizi ya kasma hiyo ni ununuzi wa televisheni, ndivyo ilivyo kwenye hii karatasi ya marekebisho na pia ndivyo ilivyo huku kwenye buku letu.

Tatizo jengine lililojitokeza ni kwamba huku kuna milioni 40, lakini huku kuna milioni 141. *(Makofi/Vicheko).*

Hebu tupeni ufafanuzi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuingilia yale maelezo ya Waziri na maelezo ya Mhe. Ismail Jussa, ninachotaka kusema ni hiki alichokisema Mhe. Waziri wa Afya, ni kwamba kama tumemsikia vizuri Mhe. Ismail Jussa, kwamba kifungu hiki kimejitokeza katika taasisi nyingi. Kwa hivyo, hii 141 ni kwa ajili ya mafungu yote yaliyo chini ya Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, haina mnasaba wa moja kwa moja na fungu hili tunalopitisha hapa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa nataka kusema hivyo hivyo kwamba maelezo ya Mhe. Waziri wa Afya, yalikuwa yanatutoa *from the frying pan to the fire*, lakini Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ameliweka sahihi, kwamba hii ni *summary* ya kila fungu vote ile katika bajeti nzima. Kwa hivyo, kama nilivyosema hata hii. Ndio maana nataka kukiuka kanuni, hatujafika katika mafungu hayo, lakini hili fungu la kuwa na milioni 40 kwa TV haliko hapa tu, liko kwengine vile vile katika bajeti ya ofisi hii hii ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ndio maana nikasema ujumla wake ndio hiyo 141 inawezekana. Kwa hivyo, katika hii sio sahihi kufanya marekebisho haya.

Lakini bado kwa kuthibitisha hoja yetu iko sahihi Mhe. Mwenyekiti, iangaliwe *sub vote* iliyokuwepo hapa na nambari yake na maelezo yake, na *sub vote* ile iliyokuwepo katika maelezo haya, ni nambari ile ile na maelezo ni yale yale. Kwa hivyo, ukisema kwamba inahusu jenereta haiwezekani, kwa sababu haiwezekani ukakosea kuanzia nambari ya *sub vote* mpaka *description* ya *sub vote*.

Hizi ni fedha kwa ajili ya televisheni Mhe. Mwenyekiti, na hatuwezi kuruhusu televisheni kununuliwa kwa shilingi 40 milioni, fungu hili tuliondowe sasa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Haya, tunafanyaje sasa. Hapa suala lililobaki ni kwamba tupige kura kama fungu hili tunalipunguza au tunamwachia tuje tuone wakati wa utekelezaji kama hilo jenereta amenunua kweli. Maana marekebisho yake yeye ni kwamba huu ni ununuzi wa jenereta.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba Mhe. Waziri kwamba tusilazimishe kwenda kwenye kura kwa suala kama hili, kwa sababu kwa kuwa ushauri umeutoa, mimi nafikiri Mhe. Waziri kama kuna makoseo akubali tu hii tuipunguze, ili tuendelee mbele. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hata kama kuna marekebisho kwenye Kamati hayakuja. Sasa kamati yetu ndio kamati ambayo inayotakiwa hayo marekebisho ifanye kwanza, sasa marekebisho kuja kufanywa hapa hapa moja kwa moja, wakati mwengine inakuja kutuletea tabu.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa haya maelezo yameshakuwa na utata, kwa sababu mwanzo Mhe. Waziri alieleza vizuri. Bora angejenga ile ile hoja yake ya televisheni, kusema kuna na vifaa vyengine, lakini baadae akaja kusema jenereta.
Mhe. Mwenyekiti, hili lilikuja kumchanganya baada ya kuletewa karatasi kutoka juu. Wakati mwengine wanawachanganya Mawaziri. Mimi naomba watendaji wetu wajitahidi wawasaidie mawaziri tokea huko ofisini, kuliko kuja kuwachanganya hapa. Mhe. Mwenyekiti, kila siku tutawaumbua Mawaziri wetu kutokana na uzembe wa

watendaji. Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati hii, suala halikuja labda kama kulifanyia marekebisho.

Mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, hili liwe funzo kwa watendaji wetu, sio kwa mawaziri wetu, kwa watendaji wetu. Mimi nafikiri hii milioni 40 tuisamehe, tuipunguze ili tubakiwe na hizo nyengine watatumia kufanya *re-allocation* kama wanataka kununua jenereta, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, baada ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Wenyeviti na Mwenyekiti wa Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali, kwa ushauri wake na nasaha zake na mimi nimekubali. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, sasa fungu hili linapungua, maana yake jumla ya fungu itakuwa pungufu ya fedha hizi kama hakuna jengine litakalotokezea.

Jumla ya Fungu kasoro milioni 40 (**814,000/=)**

FUNGU 08 - OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu 0501 - Baraza la Mapinduzi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na katika fungu hili nilitoa *queries* mbali mbali katika maelezo yangu na ninamshukuru Mhe. Waziri nyingi amezijibu na alizijibu vizuri na maelezo ya kina kabisa. Kwa mfano, lile fungu na *items* na vitu vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka ulimkatisha pale mwisho kwa hivyo pengine hakuwahi kufika eneo lile, basi naomba anisaidie hilo, kwamba katika mafungu yaliyokuwepo hapa na fungu nililolizungumza ilikuwa ni matengenezo ya majengo, ambapo hapa kuna *vote* 200700 Matengenezo ya Ofisi Nyumba iko kwenye ukurasa wa 107 Mhe. Mwenyekiti. Katika *sub vote* 200702 Matengenezo Makubwa ya Majengo kumetengwa shilingi milioni 185/=.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidiwe tu, kwa sababu kwenye bajeti yake Mhe. Waziri ameshatwambia kwamba mwaka jana Ofisi ya Baraza la Mapinduzi *Peoples' Palace* tayari imeshafanyiwa matengenezo makubwa. Kwa hivyo, haya matengenezo mengine makubwa ya shilingi milioni 185/= ni yepi. Naomba anisaidie maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Ofisi ya Baraza la Mapinduzi mwaka jana ilitengenezwa, lakini ujenzi wa ofisi haukumalizika na sasa tunaendelea tena. Kwa mfano, kuna makabati ya *files* za siri, ofisi, vipoza hewa, kwa ujumla ule ujenzi haukukamilika. Kwa hiyo, tumeomba tena kwa ajili ya kuendelea na mwaka huu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi kwa sababu ni Mwakilishi wa Mji Mkongwe karibuni nilitembelea jengo la kasri na sikuwahi kuyaona haya matengenezo makubwa ambayo anayaeleza Mhe. Waziri. Lakini nasema kwamba shilingi milioni 185 kwa ajili za makabati na *furniture* nyengine zinanitia mashaka na wala sitaki kuzuia fungu hili.

Kwa hivyo, tuendelee lakini nimuombe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na wajumbe wake waende wakafanya ukaguzi wa kina, ili wajiridhishe na *value for money* kama Kanuni zetu zinavyotaka, kwamba je haya matengenezo ya mwaka jana ya ofisi ile ambayo ofisi ndogo tu.

Baraza la Mapinduzi haitumii jengo zima la kasri ni sehemu ndogo tu ya jengo la kasri pale Forodhani, ijiridhishe na halafu kweli tuone kwamba zinahitajika shilingi milioni 185/= kwa mwaka huu. Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nadhani kamati yetu itafanyakazi vizuri naomba tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Mwenyekiti anakubali kwa kazi uliyompa. Tunaendelea.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hicho wakati nilipokuwa nikichangia nilitaka maelezo kwa Mhe. Waziri kuhusu matengenezo ya majengo ya Ikulu.

Kwa hivyo, nilimuomba aje anipe ufafanuzi mzuri kuhusu jengo la Micheweni, kwa sababu hii itakuwa ni mara ya pili, kwani mara ya kwanza aliniambia kwamba suala hili litashughulikia na kwa bahati nzuri alinipa ahadi ya miaka miwili na sasa imeshatimia, lakini bado hakuna kilichofanyika. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo kwa ajili ya kunisaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Subeit Khamis Faki mara nyingi alikuwa anatupa hamasa tumalize ule ujenzi wa *Rest House* ya Micheweni.

Tatizo lililokuwa linatukabili ni fedha, lakini mwaka huu na sentensi ipo kwenye mradi wa matengenezo ya Ikulu kwamba nyumba ile mwaka huu tunaimaliza kwa fedha zile shilingi milioni 400/= zilizowekwa kwa *State Lodges* zote pamoja na *Rest House* ya Micheweni.

Kwa kweli tunapata tabu wakati Mhe. Rais anapofanya ziara Micheweni inabidi aje Chake Chake, kwa ajili ya kupumzika au kwenda Uwani, sijambo zuri sana. Kwa hivyo, tumeazimia mwaka huu kuimaliza tena namuahidi Mhe. Mjumbe kwamba tushirikiane na yeye yupo kule na tutamaliza ujenzi ule mwaka huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kabla Mhe. Subeit Khamis Faki hajasema ndio au sio ni *sub vote* hii au hiyo ni nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: sasa kimsingi maelezo yameshatoka. Lakini *sub vote* yenyewe sio hii iko nyengine. Mhe. Subeit Khamis Faki nakusudia huko usije kusimama tena.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwanza, kwa sababu kuna kifungu chengine.

Kifungu 0501	-	Baraza la Mapinduzi	1,362,000,000/=
		Jumla ya Fungu	**1,362,000,000/=**

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kabla hatujaingia kwenye fungu hili nataka kutoa tahadhari moja tu, ili utusaidie muongozo wako. Katika eneo hili kawaida tungetegemea pawepo fungu linalokwenda Baraza la Manispaa, lakini mwaka huu halionekani hapa. Kwa hivyo, kabla hatujaingia kwenye mafungu katika kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri, kwenye *summary* yake kule nafikiri 110 liko hilo fungu.
Kwa maana hiyo, tunaomba utupe muongozo kabisa kabla hatujafika huko kwa sababu palikuwa na hoja nyingi zinazohusu Manispaa. Lakini lile fungu la ruzuku hapa na nafikiri hata Mhe. Wanu Hafidh Ameir aliwahi kulitaja kwenye mchango wake kwamba halionekani kwenye buku hili. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba muongozo wako utusaidie kabla ya kufika huko.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, labda tupate maelezo kabla ya muongozo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, Ruzuku ya Manispaa ipo lakini halikuandikwa hilo jina la Manispaa ndio hayo unayosema kwamba kidogo buku hili lina lugha nyengine na yale tuliyoyazoea. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia ukurasa wa 132 buku hilo kifungu 263100 Ruzuku *Transfers to other General Government Units, Programs* na Ruzuku kwa ajili ya mishahara, *subvention for support* ipo hapo 1291 ndio mishahara ya Baraza la Manispaa na hapo ndipo ilipo.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, ruzuku ipo hapa. Waheshimiwa Wajumbe, basi huko tutaendelea nadhani tuendelee. Lakini kimsingi maelezo yake ndio hayo. Nafikiri Mhe. Ismail Jussa Ladhu wasi wasi wake ni kwamba hapa tupo kwenye Kamati ya Matumzi na kuna baadhi ya taasisi kama hiyo Manispaa inapata ruzuku na haioni iko wapi, ili isijekushindwa kufanya shughuli zake, nadhani hayo ndio madhumuni makuu. Tunaendelea.

FUNGU 10 - OFISI YA RAIS IKULU

Kifungu 0301	-	Ofisi Kuu Pemba	462,406,000/=
Kifungu 0401	-		

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wakati nilipokuwa nikichangia hiki kifungu cha mipango na sera, kwa hiyo tunazungumzia sera. Nilipokuwa nikuzungumzia kuhusu uundwaji wa Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sikuridhika na majibu aliyotoa Mhe. Waziri kuhusiana na Kitengo cha *GSO* kubakia katika ofisi hii, sababu zote alizotoa hazikulingana na hali ilivyotokezea.

Kwa mfano, Tume ya Utumishi Serikalini, Idara ya Utumishi Serikalini na Chuo cha Utawala wa Umma vyote vilikuwa na vote huku na ushahidi ni buku hili kama vilikuwa na vote katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais na vyote vimehamishiwa katika Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa hivyo, ni sababu gani nzito zaidi *GSO* ibakie katika Ofisi ya Rais wakati tayari tumeshaunda Ofisi ya Utumishi wa Umma, hebu atupe sababu nzito zaidi, lakini naona sababu zake hazikuwa za msingi. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, tusaidie maelezo, Mhe. Mjumbe yeye hazuii fungu, lakini anataka ajue tu imewekwa *position* ndipo au vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana ni kweli Mhe. Rashid Seif Suleiman alieleza sana kuhusu suala la *GSO* na akasema kutokana na ukubwa wa wizara hii, basi tuondoshe kitengo hiki na mimi nilimwambia aa! Pale nafikiri pale ndipo mahala pake. Kwa kweli suala la *GSO* kazi yao kubwa ni upekuzi na usalama wa watendaji, siri za serikali.

Sasa nafikiri kwa Ikulu au Ofisi ya Rais Ikulu ndipo mahala pake zaidi na hiyo wizara nyengine anayoisema yende huko pia ni Ofisi ya Rais, lakini Utumishi wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, *proper place* ni hapa kwa ile *nature* ya kazi zao, nafikiri ni vizuri ikae hapa. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Waziri anajizonga tu. Kwa kweli angetueleza tu kwa sababu Mawaziri wote akeshaitwa waziri basi anahadhi sawa na waziri mwengine ndivyo tunavyoelewa na wala hakuna waziri mmoja mwenye hadhi iliyokuwa chini ya waziri mwengine.

Sasa hii wizara kwa sababu ya ufanisi na kuendelea katika mipangilio ya kisheria, iliundwa kwa ajili ya kushughulikia Utumishi wa Umma na ikapewa na masuala ya Utawala Bora. Lakini Kitengo hiki cha *GSO* bado kimebakia kule na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yeye mwenyewe alisema wizara yake ni kubwa sana.

Kwa hivyo, leo baada ya kusema katika Baraza hili kwamba moja ya changamoto kuwa wizara ni kubwa bado anang'ang'ania kukibakisha kitengo kile katika wizara yake. Mhe. Mwenyekiti, wakati huo Wizara ya Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetueleza humu kwamba na wao wanafanya utafiti wao kwa wafanyakazi pamoja na wale ambao bado hawajaajiriwa pia wanachunguza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa watu hawa wanaotaka kuajiriwa na wale ambao tayari wameshaajiriwa watachunguzwa na wizara ngapi na wakigongana je watu hawa.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema akatueleza kinaga ubaga ni kitu gani hasa kilichofanya hii *GSO* isipelekwe katika Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili utumishi wote wa umma uwe katika *umbrella* moja au kuna siri inafichwa, atuambie basi, kwa sababu kuna dalili ya ubaguzi katika kitengo hiki maswali yanayoulizwa na wala hataki kusema Mhe. Waziri, haya tuambie basi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa sababu nilitaka kutoa *ruling*, lakini Mhe. Mwanasheria Mkuu atanisaidia.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, tumesikia *concern* za Mhe. Rashid Seif Suleiman. Lakini kwanza naomba nimkumbushe kidogo historia ya *GSO*, mwaka 1983 tulitunga Sheria ya Siri za Serikali, baadae ikaja fikra kwamba hii haina utaratibu (*Institutional Structure*) ya kuisimamia na ndio maana mwaka 1994 ikaundwa Idara hii ya *GSO*.

Kazi ya *GSO* ikiachia upekuzi wa wafanyakazi, kwa ujumla usalama wa serikali kwa maana ya majengo na wanatakiwa wafanye upekuzi wa majengo usalama wake na wawashauri watendaji namna ya kuimarisha usalama wa majengo.

Jambo jengine *GSO* wanatakiwa wafanye ni usalama wa nyaraka za serikali, wanafanya kazi hiyo ukihitaji unaweza kuwaita na wakakufanyia kazi hiyo na wakakushauri, baadhi ya wengine tulifanya ombi hilo na wakatufanyia kazi hiyo na wakatushauri. Lakini na usalama kwa maana ya *hazards* nyengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, *GSO* ni zaidi ya upekuzi kama katika utendaji kulitokea tatizo nasema hilo ni *dynamic* za mwenendo mzima tulivyokuwa tunakwenda na *origin* kazi yao ni hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimtanabahishe Mhe. Rashid Seif Suleiman ni kwamba ukeshakuitwa Waziri wa Nchi, maana yake hawa wote ni mawaziri wa nchi, Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Vikosi, Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Uchumi, Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hasa *substantively* Waziri anakuwa ni mwenyewe Rais. *(Makofi)*

Kwa hivyo, popote ambapo Idara au Kitengo kitawekwa ni sawa kwa mujibu wa busara ambazo mwenyewe waziri au Msimamizi Mkuu Rais mwenyewe atakapoona ni sawa. Kwa maana hiyo, ukitizama kwa sababu kazi hizo za *GSO* na *status* mawaziri wote kilipowekwa na sote tunajua kwamba *Security Briefing* za kwanza dunia nzima zinakwenda kwa Rais mwenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu, kutoa maelezo ni sawa kwa faida ya kila Mhe. Mjumbe, lakini *ruling* hasa haya ni mamlaka ya Rais imekwisha. Kwa mfano, anaweza kusema kesho anaiweka kwengine au vyenginevyo na kusema anaiundia wizara ama vyovyote vile na haya ni mamlaka ya Rais. Tunaendelea. *(Makofi)*

Kifungu 0401 -

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa busara zako na umakini. Naomba kutoa hoja kwenye fungu hili la mipango na sera ambalo ni fungu la wizara nzima.

Wakati nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri nilihoji kuhusu suala zima la wafanyabiashara pale Darajani na Mhe. Waziri alisema kwamba kwa kadri ya ufahamu wake ni kuwa wizara yake inaendelea kulishughulikia suala hili na kwamba tayari wamechukua maombi ya wazalendo na wawekezaji wan je.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilibahatika kupata barua mbili, barua moja ya Katibu wa Rais ambayo imeandikwa na Bi Mariam H. Mrisho na nyengine ya Rashid A. Juma Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa. Barua ya Rais iliwataka waendelee kuvuta subira na wanashughulikiwa mwezi wa Aprili, lakini mwezi wa Juni kwa mujibu wa barua hii ya Manispaa tayari Kampuni ya *Hot Properties* umekubaliwa kupewa eneo hilo.

Sasa naomba anisaidie tu je, wanaendelea kuzungumza au hii Kampuni ya *Hot Properties* tayari imeshapewa eneo hili, naomba kujua.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri. Kwa kweli kama ingekuwa hili jibu nimelisikia mimi, basi ningesema Mhe. Hija Hassan Hija kaa kitako kwa sababu muda mrefu ulikuwa haupo. Lakini kwa kuwa hata mimi pale sikulisikia, basi tupatie maelezo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza ninashukuru na nimshukuru Mhe. Hija Hassan Hija kwa utafutaji wa takwimu au hizo *facts*.

Mhe. Mwenyekiti, hizo barua mimi sijaziona na kama waziri ingepaswa kidogo ile *hierarchy*, Baraza la Manispaa zipite huko na baadae zinifike mimi, kutokana na *hierarchy* nasema na hilo sio tatizo.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba mipango ya wafanyabiashara wa pale kweli ipo na walimuandikia Mhe. Rais moja kwa moja kwa ajili ya kupaendeleza pale. Sasa Mhe. Rais akatushushia sisi kwa ajili ya kulifanyiakazi kimaoni, tunapaonaje pale.

Kwa hivyo, kukawa kidogo kuna mawasiliano ya kiofisi na bado yanaendelea, nafikiri ndio maana akajibiwa kwamba waendelee au wasubiri. Mhe. Mwenyekiti, hicho ndicho ninachokijua mimi kilichotendeka kwa upande wangu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kukushukuru kwa kutukumbusha na nakuthibitishia kwamba Mhe. Waziri wakati alipojibu nilikuwapo na nimefahamu.

Kwa kweli ninachosema mimi hii Idara ya Mipango na Sera ya wizara nzima kubwa barua ya Katibu wa Rais inawaomba wawekezaji wazalendo wavumilie na kushughulikiwa, barua ya Mkurugenzi anamwambia Kampuni tayari umebarikiwa.

Sasa hapa tusaidie kwamba wazalendo wasubiri ipi hii ya Rais ambayo inashughulikiwa au waendelee kukata tamaa, kwa sababu Mkurugenzi tayari ameshaibariki Kampuni ya *Hot Properties*. Mhe. Waziri naomba utusaidie hilo tu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote Rais mkubwa kuliko Mkurugenzi wa Manispaa. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Hija Hassan Hija aiheshimu barua iliyotoka kwa Katibu wa Rais. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naheshimu sana barua ya Mhe. Rais na ndio maana nikapata kigugumizi hivi ni mkubwa nani, najua mkubwa ni Rais ndio maana barua ikenda hivi.

Sasa kama hivyo ndivyo, basi na yeye ajifunze kuona kwamba watendaji wanakiuka maagizo ya ofisi kubwa na wanafanya kwa maamuzi yao. Kwa kweli hili ni jukumu lake la kuamua je, huu ndio utaratibu au utawala.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, jitahidini muwe na *communication network* yetu iwe nzuri, ili serikali moja isiwe na maamuzi tofauti.

Hii hoja ya ngapi, kwa sababu ya kwanza ilitoka pale, pili na sasa tunaingia ya tatu nimpe Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru pamoja na mjumbe wangu kwa kusoma ripoti yetu ya kamati kwa ufasaha mkubwa na ninaamini mwakani na yeye atakuwa mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi ukiacha ile ripoti, kwa ajili ya kumkumbusha Mhe. Waziri na kwa kuwa kamati yako Mhe. Mwenyekiti tunatumia fedha za wananchi kwenda kutekeleza majukumu kwa wananchi.

Sasa kuna swali moja tu ambalo namuomba Mhe. Waziri alitolee kauli kwa kuwaelekeza Wakuu wao wa Mikoa kupitia kwa masheha kufungua njia zote zinazoendea baharini katika yale maeneo ya uwekezaji utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na kero kubwa wawekezaji wanaunganisha kuta zao na wananchi wanapotaka kwenda kwenye shughuli zao baharini inabidi wazunguke masafa marefu. Suala hili tumelitolea maagizo katika kamati tumefuatilia na tumegundua kwamba halikufanyiwa kazi.

Kwa hivyo, naomba suala hili alitolee kauli Mhe. Waziri angalau kuagizwa Wakuu wa Mikoa, ili kuhakikisha wale wawekezaji katika maeneo yetu hasa katika ukanda wa baharini wanafungua njia zote ambazo wananchi wanatakiwa wapite kama sera ya serikali inavyotaka. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma kwa *concern* yake hii. Kwa hivyo, ninachotaka kusema sio kulitolea kauli tu, lakini tunawapa maelekezo kwa sababu hili jambo ni la uwekezaji na hatujui huko makubaliano yako vipi, lakini taratibu za kiserikali zipo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachomuomba Mhe. Hamza Hassan Juma tushirikiane kwa pamoja kwa nafasi yake kama Mhe. Mwenyekiti ambaye anasimamia ofisi hii, basi tutakwenda huko kwa Wakuu wa Mikoa tutakaa nao kwa ajili ya

kuwaelekea, yaani *field* ili tuone, kwa sababu tusijetuka- *contravene* ile mikataba ya mahoteli na kutoa kauli na maamuzi hapa na kule kunapingana na mambo mengine. Kwa hivyo, ningemuomba sana kwa hili tushirikiane kwa pamoja na tutakwenda huko *field* na tuone tunafanya vipi. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, suala hili sio kubwa ni dogo sana, kwa sababu wawekezaji wanapopewa maeneo wanakuwa na ile mipaka yao. Vile vile kuna *beckon* moja na nyengine, yaani baina ya muekezaji mmoja na mwengine, yale maeneo yanatakiwa yawe *free* kwa wananchi, kwa ajili ya kutumia kwenda kwenye shughuli zao kama vile baharini.

Mhe. Mwenyekiti, miradi yetu imo katika maeneo ambayo wananchi wetu wanakaa. Kwa hiyo, wakati mwengine wanaunganisha hizo kuta bila ya utaratibu. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, tumeshalitolea maelezo katika kamati na wala si mambo ya kukaa na kupoteza muda mwingi.
Nadhani Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane na yeye kwamba tukimaliza hiki kikao basi tukae na Wakuu wa Mikoa wote tuwape maagizo katika yale maeneo ambayo tayari wawekezaji wamezuia wananchi kwenda baharini, basi wafunge yale maeneo ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tumefikia pahala pa zuri, kwamba jambo hili si vyema kulitolea kauli katika chombo hiki, kwa sababu kuna wahusika wengi katika masuala ya uwekezaji. Kwa hiyo, tukija kutoa *ruling* iliyotolewa na chombo hiki, kwa sababu akitoa ndio chombo hiki kimefanyakazi hiyo na itakuja kuleta migongano kati maamuzi yaliyofanywa na taasisi zinazohusika na chombo hiki kikubwa, kwani chombo hiki ni kizito tena ni kikubwa kweli.

Sasa muongozo huu na ule muongozo niliotoa kwamba kuwe na *communication network*, iwe ni vizuri ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na uamuzi mmoja ambao ni thabiti. Tunaendelea.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Spika: Muda unakaribia kwisha na shughuli haijamaliza. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli zilizopo mbele yetu bado hazijamalizika na kwa kuwa muda wa Baraza lako wa kipindi cha asubuhi unakaribia kumalizika. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Spika tuweke Kanuni kando ya muda, ili tuweze kumalisha shughuli zilizopo mbele yetu. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri ya kuongeza muda wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Kifungu 0701	Huduma za Rais Unguja	1,908,266,000
Kifungu 0801		

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuweza kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri juu ya swali ambalo nilimuuliza kuhusiana na *Supermarket*. Alisema tu Mhe. Mshimba kachangia lakini hakunipa hoja iliyokuwa nzito.

Madhumuni yangu kuwa wenyewe Madiwani walisema kuwa walimpa *notice* ya mwezi mmoja ukimaliza iwe mkataba basi ili waweze kuleta kitu cha maendeleo kiweze kuwasaidia. Vile vile huyu muwekezaji kwa zana tu akapitia chini ya mgongo akaja kwako inavyosemekana, toba sikio. Wewe ukatoa ruhusa kuwa aendelee. Nataka sasa unipe jibu sahihi je, hili suala ni kweli? Kama ni kweli Mheshimiwa waruhusiwe mara moja Madiwani watoe kauli ili waendeshe mradi kama wanavyoendesha Mawizara mengine.

Mhe. Mwenyekiti: Inawezekana ikawa hapa sio pahala pake, pahala pake ilikuwa ni kule nyuma. Lakini kwa sababu hili jambo linakugusa Mhe. Waziri, nadhani upate nafasi ya kujisafisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mshimba kwa kunikumbusha. Mimi kama wiki mbili zilizopita, walikuja wajumbe wawili Waheshimiwa Madiwani, Mhe. Shara pamoja na Diwani wa Rahaleo. Wao walinifuata wakanambia Mhe. Waziri tunakuomba uje, kwenye Kikao chetu cha Madiwani kuna mambo tunataka tuyazungumze kwa Mustakbal wa Wizara yetu. Nikawambia sawa nimesikia lakini tutapanga kwa sababu sasa hivi tupo kwenye Bajeti.

Suala moja kubwa hilo la *diplomatic supermarket*. Nikawambia sawa basi tutatafuta wakati tutakuja, tutazungumza tatizo tuweze kujua tatizo ni nini. Ndio akanieleza, mimi nilikuwa hata sijui hayo mambo ya kiutendaji wala hayajanifikia bado. Uwamuzi ulikuwepo kwamba yule bwana anafurushwa hilo mimi nililisikia kwenye TV. Nikaona Madiwani walipokwenda pale na kumwambia kwamba bwana wewe Jumatatu uondoke.

Mimi kama waziri ni lazima nitumie busara. Nikamwambia kwanza mwambie huyu bwana abaki, waje watu wa Manispaa tuzungumze nini haja yao, wanataka kufanya nini, wayalete Wizarani. Hatuwezi kufanya kazi kwa nje nje, hichi ni chombo chetu. Ndiyo yale uliyoyazungumza Mhe. Spika. Lazima Manispaa wajue kwamba kuna Wizara ambayo ndio baba. Hawawezi kuchukua *conflict statement* wakenda kwenye TV kwamba wewe uhame tu. Yule bwana ana mkataba na analipa, sasa kama akenda Mahakamani utafanya nini, tutakosa mwana na maji ya moto.

Pili pale kuna kituo cha Umeme, halafuu unamwambia kile kituo tufunge pale, unasababisha matatizo kwa wananchi wengine. Kwa hivyo kama mimi ni Mkuu wa Wizara, nikatumia busara, nikawambia njooni tuzungumze. Sasa huo wasaa wa kuzungumza hatujaupata *Inshallah* baada ya kumaliza Kikao tutazungumza na naamini tutaelewana hakuna matatizo yoyote.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani maelezo haya yatoshe juu ya hili.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi nipo katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aliponijibu Mhe. Waziri nilikuwepo, kanijibu juu juu tu, hakunijibu hasa vile ambavyo masuala niliyoyauliza. Namuomba sana Mhe. Waziri anihakikishie hapa kwenye kikao hichi.
Serikali za Mitaa, Wilaya ya Wete, Wilaya ya Chake, kwa Pemba kwa ujumla kwamba walipwe pesa zao za *arrears* hilo moja.

La pili wameambiwa kwamba ile mishahara nyongeza waongezwe kwenye makusanyo yao. Kwa hivyo mimi sitokubali nataka anihakikishie hapa kwamba yeye ndiye muhusika Mkuu, atoe fedha hizo awape haki zao na nitakizuia kifungu hichi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Asha asikizuie kifungu. Kwanza kuhusu *arrears* nafikiri tulisema labda alikuwa nje. Tulisema kwamba *arrears* zote ziko tayari zimeshapigwa hesabu bahati mbaya, baada ya kufatilia na mimi nimeambiwa kwamba vocha zimeshapigwa. Mwezi huu wa Juni ilikuwa walipwe, hazikulipwa. Lakini zipo tayari, tukijaaliwa mwisho wa mwezi huu wa Julai watalipwa mishahara na *arrears* zao zote.

Kuhusu mishahara hiyo ndiyo nia ya serikali yetu kila mfanyakazi apandishwe mshahara na wao madhali ni wafanyakazi watalipwa. Kulikuwa kuna matatizo ya wapi kwamba utokee ule mshahara, kwa sababu wao wanapata ruzuku. Lakini tumeshakaa na Wizara ya Fedha pamoja na Utumishi wa Umma tumeshakubaliana, haki yao ya nyongeza na wao watalipwa kama wafanyakazi wengine wa serikali. Hilo namuhakikishia, hakuna tatizo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Fedha hizi zitatoka wapi na humu hazimo Mhe. Waziri?

Mhe. Waziri wa Fedha akisema atazitoa yeye tutampa makisio yetu ambayo sasa hivi umeme uko juu atufanyie kwa *units* na baadhi ya mambo mengine. Atatizotoa wapi Mhe. Waziri fedha hizi. Naomba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mwenyekiti, nilieleza wakati ule labda kwa vile kizungu kwa vile wengine kizungu hapa na Mhe. Bi Asha sijui alisoma Romania vile au Yugoslavia kidogo kingereza hapa. Samahani namtania tu, kumradhi.

Kile kifungu nilichosema pale kwamba ruzuku *transfers to others general government units programmes and* Manispaa pamoja na Mabaraza ya Miji. Imo *inclusive 32 millions* kwa Mabaraza ya Miji ya Pemba, imo kifungu cha 263100 na wao wamo humu *inclusive*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mie Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani na Mhe. Waziri kutokana na majibu yake. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kama zilikuwepo hizi pesa kwanini asizitowe akawapa watu haki yao.
Mhe. Mwenyekiti, mie nimesoma chini ya Miembe, lakini nakuhakikishia nawashinda wale waliochukua ma- PhD na ma – Diploma. Mimi ni matunda ya Mhe. Mzee Karume, Mwenyezi Mungu amrehemu, sasa sina PhD wala Masters. Lakini wenye ma- Masters na ma- PhD ndio wanaotudhalilishia baadhi ya mambo. Kwanza namuomba Mhe. Waziri afute kauli yake kama nimesoma Czecho-Slovakia, Bulgaria au wapi. Naomba kwanza anitake radhi. Hatukuja hapa kuoneshana visomo, tumekuja hapa kwa maslahi ya wananchi na nchi yetu. Namuomba anitake radhi ndio niweze kukipitisha kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Unajua shughuli hizi zinakwenda pamoja na *lobbing* yenye heshma kubwa ndio kawaida ya vyombo hivi. Sasa unapoteleza kidogo usione tabu kuomba radhi Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Asha Bakari Makame, mwenyewe alisema jirani yangu, ndugu yangu, katumia *adjectives* tatu, sasa mimi nimvunjie heshima leo Bi Asha. Yeye mwenyewe kazungumza jana hapa vizuri kabisa, hata siku moja Mheshimiwa sithubutu. Mimi namuona kama dada yangu, ndugu yangu, mpenzi wangu, yote hayo. Mheshimiwa kama mdomo umeteleza namuomba radhi.

Mhe. Mwenyekiti: Tupe kauli ya kupitisha kifungu sasa kumuachia.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nijigambe mimi ni Mapinduzi ya Karume najigamba. Sisi ndio wale *form six* wa Marehemu Mzee Karume ndio sisi tuliokuwa Mawaziri, mmoja wapo nikiwa miye Mhe. Mwenyekiti.
Ahsante sana ndugu yangu umeniwekea maneno wazi, umenistahi, nakubali, umetaka radhi pia nakukubalia. Lakini ahakikishe nitamuandama kuhusu fedha za Pemba nitakuwa nae bega kwa bega kuhakikisha watu wanapata haki yao, kasema kwamba vocha zimeshapigwa kwa hiyo nasuburi, nakiachia kifungu. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nakiachia kifungu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwa muda mrefu nilichangia njia ya Forodhani kwa muda mrefu Waziri swali hili hajalipatia ufumbuzi. Vile vile nikamueleza nataka maelezo njia ya Mkunazini lini itajengwa baada ya Mhe. Mbunge kukabidhi milioni 40.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya sikuitolea maelezo. Lakini tuliwahi kujibu swali hapa kwamba kuna mpango wa Mheshimiwa wa Mjimkongwe takriban fedha ameshatoa itajengwa ile njia. Ni suala la kufuatilia na kuliweka sawa kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na kitengo chake cha UUB, tuone ile njia inajengwa. Mimi nitalichukua nitakaa Manispaa na mwenzangu Mhe. Waziri Hamad Masoud tuone na kitengo chake UUB ili kuona ile kazi inafanyika. Mhe. Mbunge wa Mjimkongwe ameshatupatia fedha kwa kazi hiyo. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, njia ya kuelekea Forodhai kwa miaka miwili hivi sasa bado imekuwa kizungumkuti. Kimsingi suala hili Mhe. Waziri unalikubali lakini inapofika wakati wa utekelezaji unakuwa haupo. Hebu tupe kauli moja isijekuwa umeondosha yale madude ili tupitishe Bajeti, ikisha baadaye yakarudia tena. Nataka kauli yako Mhe. Waziri kwa hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya serikali na mimi ningetoa ufafanuzi kidogo tu, kuhusiana na maswali mawili aliyoyauliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Kwanza kama maelezo aliyotoa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu. Lakini la pili kuhusiana na hii barabara anayoizungumzia *round about* ya Malindi kuelekea upande wa Forodhani. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na lile swali lake mama alilolizungumzia suala la barabara ya Forodhani. Suala hili kwa msingi ni kwamba serikali kunako mwaka wa 1994 iliingia katika utaratibu wa uhifadhi wa Mjimkongwe.

Kwa mujibu wa sheria ile ya Mjimkongwe inaeleza wazi kwamba miji Mikongwe inakuwa ni *traffic free zone.* Kwa msingi ule ule katika *Zanzibar Master Plan* ya mwaka 2008 ilielekeza wazi kwamba eneo la Mjimkongwe litaendana na mahitaji ya uhifadhi wa Mji Mkongwe. Sisi pamoja na Manispaa tukakubaliana kwamba katika eneo la Mjimkongwe tuanze kudhibiti uingiaji wa magari. Katika hatua ya kwanza tumekubaliana kwamba kuwe na *one way*. Ndio maana kutoka *round about* ya Malindi mpaka ilipo Wizara yetu tukasema pale tutaruhusu magari mpaka ya tani 4 au tani 5 kwa kuweza kupata *access* ya kuingia Bandarini, zaidi ya hapo hakuna ruhusa ya kwenda mbele.

Suala la ujenzi wa barabara kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba sisi tutakaa na wenzetu wa Manispaa. Mchango wa Fedha uliotolewa na Mhe. Mbunge ili kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika katika kipindi cha mwaka huu cha 2012 kabla ya kumalizika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naomba utumike utaratibu wako Mhe. Spika, kifungu Nam.37. Waziri au Mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo anatakiwa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa na usahihi, kwa ufupi, isipokuwa swali alilouliza Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine na Mwanasheria Mkuu. Wajibu wa kujibu swali sio Naibu Waziri kwa mujibu wa kifungu hichi. Naibu Waziri hana uwezo wa kunijibu mimi na ameshazoea kujibu.

Mhe. Mwenyekiti: Anachokusudia Mhe. Jaku ni kwamba mamlaka ya kujibu maswali haikuwa sahihi yajibiwe na Naibu Waziri. Isipokuwa yajibiwe na Mhe. Waziri mwenyewe. Lakini kwa madhumuni ya kujibu maswali jambo hili ni utamaduni wetu hapa. Hoja ndio tuliokubaliana katika Kanuni hizi kwamba hiyo ni Waziri, kama Waziri hayupo Kaimu kama hayupo huyo badi Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo labda kama Waziri mwenyewe atasema kwamba maelezo ya Naibu wake siyo sawa, lakini kwa kuwa hajasema jambo pale inaonekana maelezo haya ni sawa sawa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi kama yupo Waziri anijibu Waziri, Mhe. Naibu Waziri siku zote majibu yake yanakuwa hayashikiki wala hayafahamiki Mhe. Naibu Waziri huyu.

Mhe. Mwenyekiti: Tufate lile alilozungumza kama itakuwa kuna hoja kwamba hakufanya hivyo hilo ni suala jengine litakuja hapo baadaye. Lakini tukubaliane kwamba utekelezaji utakwenda kwa mujibu wa majibu aliyotoa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Waziri kuhusu Baraza la Manispaa, sikupata majibu ya kuniridhisha ambayo yangesaidia. Mimi nampa ushauri Mhe. Waziri kwamba masoko yetu yote ya sehemu ya Mjini tukianzia la Darajani, Malindi, Saateni, Mwanakwerekwe pamoja na Mombasa, hivi ni vioo vya mji.

Nitamuomba Mhe. Waziri, fedha ambazo zimetiwa humu kwa kipindi hichi cha mwaka mmoja tu cha fedha tunazopitisha, tuchukue masoko mawili tuyatengeneze vizuri ili kipindi cha mwakani tuchukue tena mawili tuyatengeneze tena vizuri na mwakani tuchukue mawili. Nimetoa mifano Mhe. Mwenyekiti, sitaki nirejee kwamba tunasafiri sana na tunaona. Nikamtaja Mstahiki Meya na nikamtaja na Mkurugenzi wake, kwa hivyo mimi najitolea Mtoto wa Karume kama watanishirikisha sitaki kulipwa, sitaki chochote lakini katika kupanga mipango ya masoko yetu yaweje na yawe vipi. Maana na sisi pamoja na kuwa hatuna PhD lakini tumesafiri nchi nyingi. Miye bado nchi chache Mhe. Mwenyekiti kuzimaliza, kwa hivyo naona mambo mengi.

Namuomba Mhe. Waziri anihakikishie hapa, miye nipo tayari nijitolee ili nishirikiane na Manispaa pamoja na wizara yake kuweka hali ya mji wetu, kuwa msafi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakubali na nimeipokea kwa nia safi kabisa mchango wa Mhe. Asha Bakari Makame, tutashirikiana na nitamfuata.

Mhe. Asha Bakari Makame: Naipitisha, ajue nitamuandama kwa madhumuni yale yale uliyoyasema kwa madhumuni ya wananchi na sio kwa kumuandama vyengine.
Kifungu 0801 1,992,409,000
Kifungu 0901

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu kuhusiana na Idara hii ya Uratibu wa Idara maalum ilitoa hoja mbali mbali kuhusiana na watendaji narejea kusema kwamba vikosi vya SMZ ni fahari kwetu Wazanzibari kwa sababu hivi ni vikosi vya Zanzibar. Lakini nilitoa baadhi ya mambo ambayo niliomba Wakuu wa Vikosi hivi wakishirikiana na Mhe. Waziri warekebishe hasa malalamiko yanayotoka kwa askari wa vikosi hivi.

Mikato ya aina mbali mbali, kutopatiwa posho zao wanaposafiri, wanapotakiwa kuchangia katika majengo, michezo ambayo yote na vifungu mbali mbali Mhe. Mwenyekiti. Katika maelezo yake Mhe. Waziri amezijibu nyingi ya hoja hizi na amesema kwamba mikato imepungua. Lakini katika maelezo yake alisema inawezekana Waheshimiwa Wawakilishi wamepokea malalamiko haya kipindi ambacho kabla marekebisho yalikuwa hayajafanyika.

Nataka nimuhakikishie kwamba baadhi ya malalamiko hayo Mhe. Mwenyekiti, tumeletewa siku tatu zilizopita. Mimi nilikuwa nataka kumuomba kitu kimoja tu hapa. Atuhakikishie Baraza hili kwamba badala ya kuridhika na taarifa anazoletewa na wasaidizi wake ikiwa ni Makamanda ikiwa ni Mkurugenzi wa Idara hii. Mhe. Waziri atupe kauli hapa kwamba haya atayafatilia na tumuombe kwamba atoe kauli na atakwenda kukaa na askari wenyewe katika mazingira ambayo yataruhusu kusema. Kwa sababu kuna mazingira akiwaita mbele ya wakubwa wao na nidhamu ya kijeshi hawawezi kusema wanayotwambia sisi.

Nimuombe Waziri haya ayafatilie ili kama alivyotoa kauli yake, basi kauli yake isimame kwamba kauli ya Waziri hapa ni kauli ya Sera kwamba Mikato yote ikiwa ya michezo, ikiwa ya majengo, ikiwa ya kukatwa ZSSF zao, haya ayafatilie Mhe. Waziri ili yapatiwe ufumbuzi. Naomba kauli yake hiyo tu baada ya hapo Mheshimiwa nitamruhusu tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimepokea na nakubali ushauri wa Mhe. Jussa wa kukaa kwanza na Maofisa halafu na askari wa kawaida au watendaji wa chini kuzungumzia masuala haya. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nilivyochangia hoja hii jana na kwa kuwa Wawakilishi wengi walisifu sana kwenye vikosi, nilihoji kwa wale vijana wetu ambao ni 150 ambao serikali iliwapatia mafunzo hapa Zanzibar na hata JKT Tanzania Bara. Hatimaye tukawatumia kwenye ulinzi wa majumbani mwetu na Afisi zetu. Hatimaye wasiajiriwe, badala yake wakaajiriwa vijana ambao ni nje ya *intake* ile. Mhe. Waziri amejaribu kujibu lakini nataka atwambie hasa ili Wazanzibari wafaidike ni sababu zipi za msingi hasa ambazo zimepelekea, vijana ambao tumewatumia kwa mafunzo, na tumewatumia maofisini mwetu na tulikuwa tukiwalipa Sh 25,000/-, lakini hatukuwaajiri na tumewaajiri watu wengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti kweli Mhe. Hija alipokuwa akichangia alitoa hoja hii ya vijana wale ambao walipata mafunzo ya JKT. Nataka kusema tu kwamba baada ya mafunzo yale ya JKT au ya JKU sio maana yake lazima wasubiri ajira za serikali au za Vikosi. Zikitokea ajira zozote huwa wanafanyiwa mpango, lakini kwa kipindi kirefu kwenye KVZ hazijatokea ajira bado.

Kwa hiyo kama zikitokezea basi na umri wao unaruhusu tutafanya mpango, hakuna tatizo, tutakwenda. Nakubali matatizo yapo na ajira sasa hivi ni *hot cake* kila mtu anazungumzia ajira, itabidi tulisimamie tuone kama bado umri unakubalika kwa sababu sasa hivi mwisho ni miaka 25 kama umepindukia kwa ajira za kiaskari basi tutawasaidia kwa upande mwengine. Jengine ndio lile alilozungumza Mhe. Waziri wa Kazi tujaribu mbinu za kuwawezesha na wao wajitegemee sio ajira ya kungoja Serikalini tu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti sikusudii kupingana na Mhe. Waziri lakini ninamuhakikishia kwamba kipindi hicho ambacho vijana wetu tumewatuma tayari ajira imetokezea na nimkumbushe kwamba wameajiri katika *intake* ya 55 wanaita *intake* tano, tano na mmeajiri na nimebahatika kunusa orodha ambao mmeajiri wapya na tunawajua mpaka nyumba zao na shehia zao. Sasa hoja yangu kwa nini mkawachukua wapya wakaanza mwanzo

mafunzo mkaacha wale wakongwe, hoja ya kwamba hamna ajira si sahihi. Na hata majibu ya Serikali ambayo wamejibiwa wale vijana tunasema kwamba vijana walijali makosa wengine walipewa sare bado ni hoja ya kuwatoa tu.

Sasa nikuombe Mhe. Waziri, kwa busara zako wale vijana uwaite na uwape angalau matumaini ya kuwaajiri mwakani. Kwa sababu mlitwambia kwamba mmewajazia mkataba wa muda lakini mkataba wa muda hakuna mkataba mliowajazia. Sasa wale vijana labda unambie utawaita na baadae pengine sisi kama wawakilishi turidhike kwamba kweli umewaita na kuwapatia ajira zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti mimi nimeupokea ushauri wa Mhe. Hija kawaita na namuomba orodha aliyonayo yeye anipe nikaufanyie kazi pamoja na makamanda wangu tutakaa pamoja tuone vipi tunaweza tukawasaidia. Lakini hapo tutapofanya ajira maana yake siku mbili hizi hazipo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru kwa kunipa nafasi mimi nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo hapa kwenye hii ada ya ushauri maana nimeziona zimekuwa nyingi na mafungu yake yamenona kweli kweli, kidogo nilikuwa nataka maelezo juu ya hii ada ya ushauri ya kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti: Tuelekeze iko kwenye kasma gani.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Iko kwenye 220509 kasma hii ya 220500 vifaa na huduma za ofisi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti kama anazungumzia ada ya ushauri tulizungumza ile *consultance fee* ndio hasa unaju bado kuna wasimamizi wetu wa mambo ya vitambulisho na kuna *fee* pia za kila mwaka kama ada tunalipa ndio hiyo hasa iliyokusudiwa washauri wale kila mwaka wanakuja wanahakikisha bado tuko kwenye *standard* zinayotakiwa lazima tuwalipe.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijamfaham Mhe. Waziri maana naona tunazungumzia kwenye Idara ya Uratibu au Idara Maalum, anazungumzia kwenye vitambulisho sasa sijui vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo *sub heading* yake inasema vifaa na huduma vya Ofisi, *Office supplies and services*. Kasma 220509 ukurasa wa 134.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimeiona nimechanganya na ile ya vitambulisho, lakini hasa ninafikiri kwa kizungu inajieleza zaidi *consaltance fees* na niseme tu kwamba unajua mara nyingi kuna washauri wanakuja kutushauri hasa kwenye mambo ya uchumi, kuja kutupa labda semina elekezi ndio yote yanaingia humu kwenye *consaltance fees*. Ni ada ya ushauri, washauri wanataka kulipwa na ni ghali kweli kweli hawa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti hii ninafikiri iko wazi kabisa mimi kizungu sijui na Baraza lako hapa ninajua lugha rasmi ni Kiswahili. Ada ya Ushauri mimi nataka ufafanuzi wa hii ada ya ushauri ya kitu gani? Hebu atufafanulie maana hizi ziko nyingi sana zina mafungu manono hizi, nimeziacha acha tu lakini naona kila tukiendelea naona nazikumba tu hebu naona tupate ufafanuzi kidogo maana tushazipitia nyuma kila kifungu zipo hizi. Sasa na hapa naona aa hebu tupate ufafanuzi katika hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Unajua Mhe. Waziri ukiitizama kasma hii hiyo *heading* hiyo hapo juu halafu kwamba ndani yake kuna ada ya ushauri maana ni kununua vifaa vya kuandikia, magazeti, sasa kinachomtatiza hii ada ya ushauri katika kununua vifaa hivi inakujaje? Kwa sababu hapa kuna vifaa vya kuandikia *stationary*, vifaa vya *computer*, vifaa vya usafishaji, ufukizaji, ununuzi wa magazeti inakuja hii ada ya ushauri kama haijakaa pahala pake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwenye hiyo *sub heading* inasema vifaa na huduma, *consultance* ni huduma, ushauri ni huduma. Kwa hivyo vifaa na huduma nadhani ni pahala pake lakini sasa labda hiyo tafsiri ada ya ushauri anaweza lakini hii ni vifaa na huduma.

Mhe. Mwenyekiti: Sijui kama kuna maelezo zaidi Mhe. Waziri ushauri wa nini ndio tatizo lake wala hadadisi pesa ngapi hapa yeye anataka maelezo tu huu ushauri wa nini?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema huo ushauri unategemea unajua hii Wizara kubwa inategemea vile tulivyopanga kama nilivyosema labda kutakuwa na semina, kutakuwa labda mafunzo elekezi, tunataka mtu kidogo labda atupe technology fulani ndio hasa hatuwezi ku-*itemize* sasa hivi ushauri huu huu huu. Lakini tafsiri hiyo yenyewe hiyo ada ya ushauri ndio *consultance*.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti mimi naona haina maelezo vizuri maana yake kama ni ada ya ushauri unahusu mafunzo ingepelekwa kwenye vifungu vya mafunzo ninafikiri wanavyo vifungu vya mafunzo. Sasa kwa hapa ilipokaa mimi ndio nimepata shaka naona kama imefichwa fichwa hapa. Sasa bado sijapata maelekezo mazuru maana nataka kujua hii imekusudiwa kitu gani watafanyia nini? Maana hiyo wameenda wamepanga tu sasa wanaomba hizi fedha kwa ajili ya matumizi ya hiyo mipango yao hebu atueleze, kama haina maelezo tulitoe hili fungu tuendelee mbele Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Una maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti labda kwa kuongezea tu nazidi kusisitiza hawa ni washauri elekezi, hawa kila Wizara lazima wafanye. Siku hizi Wizara isiwe ndogo tu lazima ujitanue, sayansi imetanuka, ushauri umetanuka na wapo wanatoa hizi taaluma maalum, si lazima wende mwaka mzima, unawaita wao unakuja kuelekeza juu ya sera, sheria mbali mbali sasa kwa hii *term* tumeweka hii.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia huku mbele kuna kasma ya 221100 ni gharama za mafunzo *capacity building* kaiandika hivyo anavyo vitu kwa nini isiingie hapa kama alikuwa ndio hao maana ndio wanaoana na hapo washauri wangekuwepo hapo. Mimi nahisi hili fungu halina matumizi yoyote Mhe. Mwenyekiti nahisi tuliondoe tuendelee mbele muda unakwenda.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri kajitahidi kueleza, nadhani kilichokuwa hawajafahamia na Mhe. Mtando ni kwamba Mhe. Waziri kajielekeza zaidi katika mafunzo. Lakini naomba nimuhakikishie Mhe. Mtando na waheshimiwa wajumbe wengine kwamba hili fungu unaliona takriban katika kila Idara kwa sababu ni jambo la kawaida.

Kwa mfano unatengeneza sera inawezekana huna wataalam wa sera ile, pengine kwenye mageuzi wakati mwengine pengine unatengeneza *work plan* huna wataalam na mambo mengi yanajitokeza si sauala tu la mafunzo, inawezekana mafunzo ni moja katika sehemu hiyo na unahitaji watu wataalam kutoka nje ya Idara na haya yanafanyika sana. Na wakati mwengine pengine unahitaji pengine ni watu wa ndani lakini katika muda wao ambao si wa kazi hiyo pia inaweza ikatokea.

Sasa fungu hili la ushauri ndipo ambapo hizi ada kwa kazi mbali mbali ambazo zinazotokea ndio zinapolipiwa si suala la mafunzo tu, naomba Mhe. Mtando afahamu kwamba mafunzo inawezekana ikatokea tu lakini ni mafunzo juu ya jambo pengine sera au kitu chochote. Lakini linatumika special kwa ushauri wa aina mbali mbali ambao unatolewa kwa Idara au kwa Wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti: Ukiangalia mantiki inayozungumzwa fungu ni muhimu liendelee kubaki.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Sijafaham Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nasema ukiangalia mantiki ya maelezo aliyotoa Mhe. Waziri hapa fungu ni muhimu kuendelea kubaki.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mimi ninakubaliana na wewe Mhe. Mwenyekiti, fungu ni muhimu lakini ndio tulikuwa tunahitaji maelezo yenyewe kujitosheleza kwake. Haya maelezo bado Mhe. Mwenyekiti bado hayajakaa sawa. Kwa sababu Mhe. Waziri hapa ameshatupa maelezo karibu mara sita lakini yote yanapishana pishana na wao ndio waliopanga hiyo bajeti. Mimi ninamuheshimu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na ninafikiri walikuwa wanataka ufafanuzi wa kisheria zaidi lakini sisi tuko katika kamati ya matumizi tunataka kujua matumizi yake zaidi.

Katika hili fungu ndio maana nataka kuona walipangia katika matumizi yepi *specific* wanakwenda kufanyia nini? Ndio ninachotaka kukijua huu ufafanuzi wa kisheria hauna matatizo naukuali lakini yeye Mhe. Waziri wa ndio alikaa na watendaji wake wakapanga ndio wanakuja kuomba hapa na sisi tunataka kuidhinisha. Sasa angalau tujuwe mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti atupe maelezo kama ni hivyo Mhe. Mwenyekiti unaona twende mimi ninaheshimu kiti chako tuendelee tu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa mwaka huu mmejipangia nini?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti hawa ni washauri elekezi wa sera na sheria mbali mbali zitakazofanywa katika Afisi yetu.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee Mhe. Mtando tupate kuendelea.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nikubaliane na mawazo yako lakini hili fungu kila Idara utaliona limo, sasa sijui kila Idara ndio washauri wa sheria na nini, tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Humu ndio mule mwahala ambamo kamati inabidi ifatilie kwa makini sana, Mhe. Hamza unapokea hii haya.

Kifungu 0901	Idara ya Uratibu wa Idara Maalum	200,000,000
Kifungu 1101	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	

Mhe. Ismail Jusa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na nirejee tena katika mchango wangu kulikuwa na vifungu vingi ambavyo niliviombea maelezo na miongoni mwa fungu ambalo nililoliombea maelezo ni fungu la viburudishaji Mhe. Mwenyekiti. Na katika Idara hii ya Utumishi na Uendeshaji ukurasa wa 136 wa buku hili vote 220200 viburudishaji fungu hili Mhe. Mwenyekiti lime-shoot kutoka milioni sita mwaka jana hadi mia moja na kumi milioni laki tisa na elfu tano kwa mwaka huu. Na *trend* hii ninaisemea hapa Mhe. Mwenyekiti, lakini ipo takriban kila Idara ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Sasa yapo maeneo hatujayahoji hapa kwa sababu yanaeleweka. *Secretariate* za Baraza la Mapinduzi tuliambiwa kuna vikao vingi siku hizi ufatiliaji mwingi, huduma za faragha za Rais tunaelewa, lakini inapokuwa kila Idara nyengine inalo fungu hili, kwa hivyo fungu hili si kama linasimamia Wizara yote. Kwa sababu kila Idara inalo na limewekwa fungu lake. Lakini kuna kuongezeka kukubwa mno kwa asilimia isiyoelezeka. Kwa hivyo nilikuwa naomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri kuhusu hilo, lakini vile vile katika mafungu hayo hayo katika vifaa na huduma za Ofisi vote 220500 ukurasa 137 tena katika ada ya ushauri kuna hamsini na tisa milioni na laki nane nilikuwa naomba vile vile anipe maelezo *consaltance* ya hapa inahusu maeneo gani. Kwa sababu kama sera kwa kweli serikali za mitaa kuna mageuzi kuna fungu lake katika fungu la maendeleo.

Kwa hivyo nilikuwa naomba ada hiyo ya ushauri na fungu hili la viburudishaji kwa nini kuna kuongezeka kwa kiasi kikubwa kama hicho au ndio fedha zimeshatoka kwa kasma kwa hivyo kila mmoja kajalizia tu apate kutumia fedha za walipa kodi bila ya maelezo. Naomba maelezo ya kina Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaruhusu mafungu haya.

Mhe. Mwenyekiti kwanza kwenye kifungu 220200 vuburudishaji, *hospitality* hasa pale Mhe. Mwenyekiti *figure* ile kutoka milioni sita kwenda laki moja mia moja na kumi milioni mia tisa na tano ile zamani ilikuwa inaitwa kwa jina jengine matumizi yaliyotazamiwa. Sasa hilo jina tumeliondoa inakuwa inclusive shughuli zote za utawala, maana haiwezekani kwamba viburudishaji tu ndio pesa hizi aa lakini hasa shughuli zote za utawala tumezipa na unajua utawala tume-*shoot* kutoka milini sita mpaka milioni mia moja na kumi.

Na kifungu cha pili alichozungumza ada ya ushauri *consultance fees* nyengine hii Mhe. Mwenyekiti, kutakuwa na kazi kubwa ya uhakika wa mahitaji na mpango wa mafunzo yaani *need assesement* pamoja na mafunzo yake na *training program* ndio maana ika-*shoot* kutoka ishirini na nne milioni mpaka tisiini na tatu. Unajua ukifanya *need assessment* inabidi watu wende field wakae masemina kwa watu nini, hayo ndio maelezo kwa vifungu alivyovieleza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika ninamuonea sana Mhe. Waziri kwa sababu kama walivyosema watanguliaji mapema nadhani haya mambo watendaji watawaungusha sana mawaziri wetu humu ndani. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hili liwe fundisho kwa mawaziri wetu kwa sababu wanaoingia humu ndani ni mawaziri watendaji wanakaa juu kule.

Mhe. Mwenyekiti, bado maelezo hayaridhishi. Ukinambia fungu la viburudhishaji linajumuisha pia matumizi yasiyotazamiwa tunapata maswali badala ya majibu Mhe. Mwenyekiti. Inakuwa kama vile paper ya Mhe. Othman Masoud kwamba yale maswali yasiyokuwa na majibu katika bajeti ya SMZ badala katika masuala ya muungano.

Mhe. Mwenyekiti fungu la matumizi yasiyotazamwa lina vote yake ambayo ni 2821000 msaidie Dr.Mhe. Mwinyihaji Makame. Na katika kila Idara ilipaswa iwekwe hapo huwezi katika fungu la viburudishaji ukaweka kitu kama hicho. Lakini kama vile vile anazungumzia ada ya ushauri kwamba inahusu mafunzo, mafunzo ina fungu lake. Na kama ni semina katika viburudishaji vile kuna ku-*subvote* pale inayozungumzia viburudishaji vya ofisi kwa mfano hapa viko thalathini milioni, lakini kuna chakula na vinywaji (*food and refreshment, seminars meeting*) ambapo hapa zimewekwa ni 27,000,000. Kwa hivyo haya yana mafungu yake Mhe. Mwenyekiti tayari. Haiwezekani ikawa fungu la consultance fees Mhe. Mwenyekiti analipwa *consultant* uliomwita kuja kukufanyia study maalum na Mhe. Mgeni wanajua mambo haya humu ndani. Unamwita anakuja kushauri labda anataka kuja kutunga sheria fulani, sera fulani, kutaka kufanya study Fulani. Hauwezekani ikawa ni fungu la mafunzo bado Mhe. Mwenyekiti tunapata wasiwasi kwa mafungu haya yamepewa katika *ceiling* hayana pa kuwekwa yamejalizwa katika mafungu haya watu wapate mwahala mwa kula.

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena maelezo niliyoyasema katika kifungu cha mwanzo kabisa, baraza hili kwa sasa haliwezi likapitisha vifungu ambavyo havina maelezo. Naomba maelezo ya kina kabla sijafikia maamuzi ya kulishauri baraza kwamba vifungu hivi tuvin'goe. Naomba maelezo ya kina.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Labda nirudie kutoa ufafanuzi tena katika kile kifungu cha viburudishaji kama nilivyosema ni shughuli za utawala, labda utawala wenyewe namna gani tuliokusudia hasa ni kwa ajili ya kamati za uongozi wa Wizara, vikao vinavyofanyika Unguja na Pemba sisi tuna kamati tendaji ya kila wiki, pia kuna vikao vya budi vya zabuni, *audit committee* ndio hizi shughulizi zenyewe za utawala nilizozikusudia.

Na pale penye *consultance fees* nakubaliana na wewe Mhe. Jussa kwamba *consultant* anakuja ni kweli lakini sasa anapokuja tunamlipa lakini huku kuna gharama zake. Kuna gharama huku tunakaa tunazifanyia hiyo hali ya kuwahutubia lazima kuwe na watu ndio wanaingia humo humo ndio hasa tunapokusudia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninasikitika kusema Mhe. Waziri hana maeleozo. Mhe. Mwenyekiti, tukizungumzia kama viburudishaji vinajumuisha vikao, mimi ninajua kuna bajeti ya Idara nzima ya Utumishi na Uendeshaji jumla yake inapatikana hapa. Kwa hivyo shughuli zote hizo zina bilioni moja na mia mbili halafu imegawiwa katika mafungu madogo madogo kila mmoja na matumizi yake. Kwa mfano kama vikao vinafanyika baina ya Unguja na Pemba hapo hapo chini ya viburudishaji kuna gharama za safari, kuna safari za ndani, kuna safari za nje ndio wanazipata katika mafungu hayo. Ukizungumzia posho la kujikimu katika fungu la mwanzo kule kuna posho la kujikimu anapokwenda katika hiyo safari kwa hivyo hapa *specifically* na tusifundishwe upya Mhe.Mwenyekiti ninasikitika, Waziri ambaye kawa Waziri wa Fedha katika serikali hii kwa muda mrefu, awe anatupa majibu ya jumla jumla kama haya.

Unaposema viburudishaji ni component ya viburudishaji katika bajeti ya jumla ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi Mhe. Mwenyekiti. Kama nilivyosema na hii haiwezekani ihudumiwe na Wizara nzima kwa sababu katika kila Idara ina fungu lake na limevimba kama lilivyovima hapa naomba maelezo Mhe. Spika, vikao vinafanyika kila mwaka haiwezekani bajeti hii ikatoka kutoka milioni sita kwa mwaka uliopita na ikafika ghafla milioni mia moja na kumi laki tisa na elfu tano tukategemea baraza hili tupitishe.

Na vile vile naendelea kurejea ada ya *consultance fees* sote tunajuana humu ndani atakuwa mtu wa ajabu sana akatwambia *consultance fees* inahusu kwenda kulipa wanaotoa semina au waliokuwa wanakwenda kuhudumia semina na vyakula haihusiani na mambo hayo. *Consultance fees* wanalipwa *consultance* Mhe. Mwenyekiti, kama hakuna maelezo Mhe. akubali kwamba fedha zimejalizwa tu tuyaondoe hapa, fedha za walipa kodi tuzinusuru Mhe. Mwenyekiti kuna hospitali zinahitaji madawa, kuna skuli zinahitaji madeski ya wanafunzi zote fedha zende huko zikahudumie mambo haya kuliko kukaa humu kukawa hakuna maelezo yoyote.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme tu kwamba maelezo ambayo anayotoa Mhe. Jussa na wasiwasi wake nataka nimtoe hofu kwamba hiki

kifungu asikitazame kwa ujumla wake wa kutoka milini sita kwenda milioni mia moja na kumi akitazame kwa vifungu vyote vitatu ambavyo ni vidogo vimo chini ya hicho kifungu kikubwa.

Kwanza kuna kifungu hapo kinazungumzia suala la ununuzi wa zawadi, tuna utaratibu sisi hapo tunapotembelewa na wageni na vile vile tuna utaratibu wakati tunakwenda kuwatembelea wenzetu, basi huwa na sisi tunachukuwa zawadi. Kwa hivyo hichi kina milioni kama hamsini na tatu, hata jana tulikuwa tuna wageni vile vile tuliwapatia zawadi. Kwa hivyo uko utaratibu huo ambao nacho vile vile kimewekwa chini ya kifungu hicho cha viburudishaji. Sasa akitazama kwa kimoja kimoja nadhani ndugu yangu Jusa ataweza kupata kimsingi hasa hiki kifungu ni cha nini.

Lakini cha pili, kuna kifungu kinazungumzia chakula na vinywaji lakini wakati wa mikutano na vikao kwa ajili ya Idara hii, wakati mwengine Mhe. Mwenyekiti, vikao vyengine vinapindukia saa za lunch, basi pale kuna huo utaratibu ambao wa kuweza ku-*provide* vitu kama hivi kwa ajili ya wale wanaokutana. Kwa hivyo nadhani vile vile akiviangalia kwa hilo ataweza kuona kwamba umuhimu wa hivi vifungu kuwepo kwa ajili ya Idara hii husika. Wingi wa fedha itategemea na wingi wa vikao vinavyotokana na Idara yenyewe. Lakini umuhimu wa kuwepo fedha hizi mimi nadhani ni muhimu sana na ninamuomba sana Mhe. Jusa awaruhusu basi hivi vifungu viweze kupita ili waweze kutekeleza.

Cha msingi ni kile kile ninachokizungumza wakati wa utekelezaji ndio muhimu kwa sababu kuwepo kwa fedha hapa haina maana kwamba ni kutumika kwa fedha fedha inakuwepo hapa incase kwamba ile dharura ya matumizi imetokea au ile haja ya matumizi imetokea. Lakini la msingi ni kwmaba usimamizi na utekelezaji katika lile lengo lililokusudiwa.Mimi Mhe. Mwenyekiti ninamuomba sana Mhe. Jussa Mwakilishi wangu wa Mjimkongwe basi aruhusu hivi vifungu viweze kupita, ili hii Idara iweze kufanya kazi zake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ufafanuzi wake, nataka nimhakikishie kabisa kwamba nimeviangalia kwa hizi subvote zake zilizokuwa zimewekwa lakini sikutaka kwenda moja moja kwa sababu nimeona ningelipotezea wakati Baraza nimezungumza kwa pamoja. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha kwamba kifungu kinapowekwa huwa si lazima kwamba zitatumika lakini ninachosema hapa ni bajeti ni makisio ya matumizi yetu kwa mwaka ujao wa fedha. Sasa kuna maeneo mengine kwa fedha hizi zinahitajika sana Mhe. Mwenyekiti. Juzi tumebishana sana hapa katika kuongeza kodi katika kuhudumia mambo maalum ambayo yametajwa. Kumbe tunatafuta fedha wakati huku fedha zinawekwa hazijulikani zinatumika vipi.

Na Mhe. Mwenyekiti naomba nifahamike hoja yangu nataka nikae sioni sababu kuendelea kuzungumza hayo kwa hayo Mhe. Mwenyekiti. Na katika ile nataka nimkumbushe kaka yangu Mhe. Omar vifungu hivi nilimwambia katika bajeti ya jumla aviangalie sana nilisema mwanzo, mimi Mhe. Mwenyekiti siamini kama bajeti ya jumla *recurrent* ni mafedha yale ambayo tumeambiwa tuyapitishe hapa na nikasema kwamba kuna mafungu mengi niliyataja siku ya bajeti ya jumla ayatizame Mhe. Waziri haya humo ndio kwenye mafichio ya watu kwenye kutafuna fedha za walipa kodi. Mhe. Mwenyekiti hebu Waziri wa Nchi anielewe, nataka alinganishe tu hivi katika kutoa zawadi Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo inamhudumia Waziri itakuwa inahitaji kununua zawadi zaidi kuliko huduma za Rais za faragha?

Hivi viburudishaji atakuwa anapoke wageni zaidi kuliko Rais sasa hebu alinganishe Mhe. Omar fungu hili na fungu ambalo tumelipitisha ambalo hakulihoji hapa vya huduma ya Rais katika ukurasa wa 128 vote 20020 viburudishaji ataona vyakula na vinywaji kwa Rais faragha Unguja kwenye makao makuu ya Serikali ukurasa 128 ni shilingi ishirini na nne milioni laki moja tisiini na tisa elfu huku kwa Waziri kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi kuna ishirini na saba milioni yaani yeye anamzidi Rais. Kwenye zawadi hapa kwa Rais kuna ishirini na moja milioni laki sita hapa kwa Waziri kuna hamsini na tatu milioni na laki tano na hamsini elfu.

Viburudishaji kwa jumla kwa Rais kuna shilingi 36 milioni, huku kuna shilingi 30 milioni. Sasa hata jumla ya Rais fungu lote hili, ni shilingi 81, 799,000. Huyu Mhe. Mwenyekiti, ndio *head of state*, ndio *symbol* yetu na ndiye anayepokea wageni wote kama zawadi ndiye anayezitoa. Yeye ana fungu ambalo jumla yake ni shilingi 81 milioni, lakini waziri katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi yeye ana milioni 110 tuipitishe mheshimiwa. Mimi siwezi kuipitisha fungu hili hata siku moja. Naomba tena fungu hili lirekebishwe au la tulipunguze au la sivyo tukubaliane hapa tutakuja kukaa na kamati tujiridhishe na kama halipo tuipe mamlaka kamati, tuwasiliane na Mhe. Waziri ana

mamlaka ya ku *reallocated* katika maeneo mengine ya juu, lakini hatuwezi Mhe. Waziri ikawa Ofis ya Rais inatumia kidogo kuliko Ofisi ya Waziri katika Ofisi ya Rais, hatuwezi kukubali hata siku moja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri naomba kusisitiza tena kwamba Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kazungumza vizuri sana na kazidi kusisitizia mkazo, kwamba kuna vikao tunafanya Kamati ya Uongozi, hii ndio inaendesha wizara na hii ndio *machinery* ya wizara. Hii Idara ya Utumishi na Uendeshaji ndio *machinery* ya wizara pamoja na sera na mipango.

Kwa hivyo, Mhe. Rais ni kweli, lakini sisi ndio wizara na sisi ndio machinery ya wizara, naomba kulisisitiza neno hilo. Kwa hivyo, ndio pale mnaposema tunashindwa kuendesha hiki na hiki, sasa watu wakae na njaa, hatwendi hivyo sasa. Lakini Mhe. mwenyekiti, ushauri wake nimeupenda alioutoa mwisho na mimi nauchukua kuwa basi tutakaa na kamati tuone hivi tunavirekebisha, lakini sio kuwa tuviondowe vifungu, hiyo wizara itakufa, itakuwa haifanyikazi. Mimi nilikuwa napenda kusisitiza hilo na nauchukua ushauri wake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, maelezo yako maana yake nini, tuendelee kamati ikusanye shughuli za kusimamia au vipi. Mhe. Jussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nataka nirudie tena kama nilivyosema kwamba tunaheshimu sana ofisi hii. Kama nilivyosema tumeletwa hapa kwa ajili ya kusimamia fedha za wananchi wa Zanzibar, nitakuja neno dogo Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipoisimamia Ofisi ya Makamu wa Kwanza watu wengi walinichokoza nje wakasema, ofisi ya bosi wako, kwa maana katika shughuli nyengine za kichama. Nikawaambia hapa hakuna chama, hapa kuna fedha za walipa kodi na sisi kama wawakilishi wa wananchi.

Kwa hivyo, nataka kusema kwamba tunaheshimu ofisi zote za viongozi hawa ikiwemo ofisi hii ya Mhe. Rais. Kwa maelezo ya Mhe. Waziri Dk. Mwinyihaji, nakubali. Lakini mwenye mamlaka baadae wa kukwamisha vifungu hivi ni Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ingawa inakuja mwisho katika bajeti yake. Mimi nataka kauli yake aniambie kwamba hili akishirikiana na kamati baada ya kujiridhisha atasimamia ili kuona kwamba ikiwa fedha hizi zilikuwa zinahitajika ziendelee, lakini kama hazihitajiki zipelekwe katika maeneo yake ambayo zinahitajika zaidi katika kuwahudumia wananchi wa Zanzibar. Nataka kauli ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana kabisa na Mhe. Jussa, nadhani kabla hata kamati haijafanya hiyo kazi yake nataka nimuhakikishie kwamba kazi hiyo nitaifanya mimi kwa kushirikiana na kamati, ili tukibaini kwamba hapa kuna fedha nyingi basi tutazihamisha kuzipeleka katika maeneo ambayo zinahitajika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee nakushukuru sana.

Kifungu 1101 Idara ya Utumishi na Uendeshaji

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, mimi nina tatizo kidogo kwenye *vote* 220700 matengenezo ya ofisi, kwenye 220701 matengenezo madogo ya ofisi *minor civil work*, nilikuwa nataka maelezo juu ya kifungu hiki, pana milioni 50 hapa. Katika ukurasa wa 137. Kasma 220700 matengenezo ya ofisi, kijifungu cha 220701 matengenezo madogo ya ofisi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kifungu kinavyojieleza haya ni matengenezo madogo madogo, sio madogo, matengenezo madogo madogo ya ofisi. Majengo yetu haya nilizungumza katika majumuisho, majengo makongwe hitilafu zinatokea mara kwa mara, isipokuwa tena mambo ya vyoo haya, ndio haya tunayokusudia humu, ni lazima kifungu hiki tuwe nacho.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi napata tatizo kidogo, maana ninavyofahamu mimi hii ofisi iko Ikulu, tuna matengenezo na tuna mradi mzima wa kuzishughulikia hizi. Tumeshaidhinisha fedha nyingi sana katika matengenezo ya Ikulu hizi. Mwaka jana pia tumeingiza matengenezo ya Ikulu na mwaka huu pia ameomba huyu, lakini bado na hapa ndani ya idara pia zinaombwa matengenezo milioni 50, mwaka jana milioni 20 na mwaka huu anaomba tena milioni 50, hebu tupewe hasa ni matengenezo gani yanayotengenezwa katika hizo nyumba

yasiyomalizika, kila siku tutakuwa tunatoa fedha kwa ajili ya matengenezo tu, si bora tukajenga nyengine kama hilo jengo halifai.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Mjumbe tumeisikia, lakini nazidi kusisitiza na unajua tunapozungumza mradi, hiyo ni miradi midogo midogo, huyatarajii na kwa ujenzi, yeye mwenyewe anajua milioni 20 kwa siku hizi kwa mambo ya ujenzi hakuna kitu, ndio tukaweka hizo milioni 50 kwa kutizamia hayo madogo madogo, sio madogo, madogo madogo. Mhe. Mtando, kama nilivyosema wakati ule huyu ni mjenzi na yeye kidogo alione hili.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anasema matengenezo madogo madogo, lakini hilo fungu la fedha ameliona, maana yake hapo uingie kwenye *tender* kufanya hayo matengenezo. Kwa mujibu wa *procurement Act*. Sasa anapotuambia matengenezo madogo madogo, fungu kama hili maana yake kungekuwa kuna milioni 5, 7 au milioni 8 tungesema kweli unahitaji vitu vidogo vidogo, kwa sababu hii ni idara tu, sio wizara nzima, matengenezo ya milioni 50 Mhe. Mwenyekiti, ni pesa nyingi sana, hizi pesa wa walipa kodi tusizifanyie mchezo Mhe. Mwenyekiti, na sisi ndio wajibu wetu hapa kuja kuziidhinisha. Tumeshamuingizia fedha huku kwa ajili ya matengenezo ya hilo jengo lote sasa ikiwa limefanyiwa *repair* halafu yeye anaomba tena ndani ya idara hii.

Mhe. Mwenyekiti, siwezi kukubaliana nayo. Nafikiri atupe maelezo ya kutosha zaidi katika hili, haya maelezo hayajajitosheleza hata kidogo. Mhe. Mwenyekiti, hizi ni fedha ndio maana niliposema kuna mafungu mengi tunayaona yameongezwa ongezwa, mimi nililipinga lile la mwanzo lakini Mhe. Ismail Jussa hilo la pili lina shilingi 59 milioni, mimi nilikwenda kwenye 30, hili hapa lina 50 tayari, wakati huku unakuta kuna matengenezo makubwa wameshayafanya sasa hii inakuwaje. Hebu atwambie kuna tatizo gani, inavuja, inafanyiwa *partition*, nini anataka kuzitumia fedha hizi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimjuilishe Mhe. Mtando kwamba hii Idara ya Utumishi na Uendeshaji haiko Ikulu peke yake, kuna jengo nje pale ndiye Mkurugenzi yuko pale na watumishi wake. Kwa hivyo, asichukulie ni Ikulu tu aa, sio jengo la Ikulu peke yake, tunaweza kuiita Ikulu pamoja na lile la nje lakini sio la Ikulu tu.

Mimi nataka kumualika kidogo nikamtembeze aone hilo jengo lilivyo na haya mambo madogo madogo ninayoyasema, *break down*, *and so on*, huzitarajii Mhe. Mwenyekiti. Haya yanatokezea, nyumbani kwako yanatokezea utatengeneza vipi, lazima vifungu hivi viwepo ndio utaratibu huo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi ndiye mwenyekiti wa kamati yake na tulipokuwa katika ukaguzi wa shughuli mbali mbali za kamati katika wizara kimsingi tulikuta kuna udhaifu mkubwa sana wamajengo yetu na kimsingi kamati haikuridhika. Kuna baadhi ya maeneo tulifika pahala tukamwambia kwamba safari hii kama hamkufanya ukarabati katika baadhi ya maeneo, kwa sababu kwa kweli kuna maeneo mengi ambayo yako dhaifu. Sasa nadhani labda Mhe. Waziri yeye hajapata muda kwa sababu katika kamati zaidi tulikuwa sisi wajumbe. Kwa hivyo, sisi tuliyaona maeneo mengi, sasa tatizo labda kwamba Mhe. Waziri kashindwa kueleza kwamba ukarabati huu utakuwa sehemu fulani na sehemu fulani, lakini kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, bado katika maeneo yetu ya Ikulu ukiangalia hata pale tunapoingilia ndani, ukiangalia ile sehemu wanayokaa askari pale sisi tunaokwenda kukaguliwa haifai.

Sasa kwa kifupi kweli hata hilo jengo lenyewe la Idara ya Utumishi kwa kweli tumewakuta vile walivyojibana bana kimsingi katika hili Mhe. Mtando mimi namuombea Mhe. Waziri, kwa sababu kamati yangu ilikwenda ikashuhudia na tunasikitika namna watendaji wetu wanavyofanya kazi katika mazingira magumu hasa wakiwa chini ya Ofisi ya Rais. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwa sababu waziri kashindwa kutoa yale maelezo ya uchambuzi lakini mimi kama mwenyekiti wa kamati wakati mwengine natakiwa nimsaidie vile vile. Kwa hivyo, mimi mwenyewe nimekwenda *physical* kuna maeneo mengi ambayo kwa kweli yanahitaji fedha kwa ajili ya ukarabati. Kwa hivyo namuomba Mhe. Mtando kwa hili atustahamilie aturuhusu hili fungu lipite ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Hamza Hassan, Mwenyekiti wa Kamati hii lakini Mhe. Mwenyekiti na mimi niko kwenye Kamati ya *PAC*, moja katika kazi zetu ni kukagua ukaguzi wa fedha. Tumekwenda pale tukaoneshwa namna ya zile fedha za ule mradi wa Ukarabati wa Ikulu, miongoni mwa majengo ambayo yalikuwa yanakarabatiwa ni hilo ambalo analizungumza Mhe. Waziri. Ikiwa fedha zile zilitumika katika ukarabati ule na tulikagua ikawa mpaka ghorofa ya kwanza tayari wanaendelea na ya

pili hilo jengo la utumishi ninalosema ambalo kama nimelifahamu ni lile nje ya Ikulu pale pembeni, limo katika mradi ule.

Sasa ikiwa fedha hizi mwaka jana aliomba shilingi 20 milioni labda kulikuwa kuna mambo ya *partition* kidogo na nini umeshafanya, mimi ndio maana nikawa nataka maelezo ya hizi shilingi 50 milioni anazoziomba sasa wakati ule mradi bado unaendelea kuombewa fedha kule na hapa anaomba tena shilingi 50 kwa matengenezo yepi, maana kama viji-*partition* vidogo vidogo hizi shilingi 20 milioni za mwaka jana alishazitumia, sasa hii 50 ambayo anaitaka mwaka huu tuiidhinishe kwa matumizi yepi ndio ninayoitaka mimi Mhe. Mwenyekiti.

Lakini pia akumbuke ule mradi kule umejenga hata lile jengo limo ndani ya ule mradi, tulikaguzwa sisi tukatembelea kama *PAC* mwenyekiti wangu nafikiri anaweza kutoa maelezo zaidi pale, tulishakagua lile tukaliona kwenye mradi ule linavyokwenda sasa ukiwa unaliombea tena na fungu jengine kwa fungu jengine dogo huku mimi ndio nakuwa sielewi. Kuziidhinisha fedha hizi Mhe. Mwenyekiti, itakuwa vigumu kidogo mpaka nipate maelezo ya kutosha. Naomba Mhe. Waziri kama ana maelezo ya ziada katika hili atusaidie.

Mhe. Mwenyekiti: Unajua mimi huwa napata maelezo humu humu ndani tunapozungumzia kuhusu habari ya Ikulu. Tumeeleza kwamba Ikulu ni pahala ambapo pana kiongozi mkuu ndio *symbol,* imezungumzwa humu ndani na nafikiri hakuna anayepinga juu ya hilo. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yeye ametueleza mpaka ukaguzi wa karibuni tu kuna maeneo tena katamka kwamba hayafai, hayaridhishi. Lakini katika Baraza hili tena kikao hiki hiki tumeulizana hivi hatutembei tukaona kwa wenzetu? Imetoka humu kwamba kwa wenzetu unakuta mambo yako *perfect* kweli kweli, ukienda Ikulu ya Dar es Salaam tu hapo kuna mambo pale ambayo kumbe ni muhimu *security-wise* petu hapana.

Mimi nadhani kama alivyoeleza waziri, kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Mwenyekiti wa Kamati. Maelezo haya yote pamoja na maelezo tuliyoyatoa humu ndani Mhe. Mtando nadhani anazingatia hayo na atasema ruhsa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa busara zako, lakini mimi nilichokuwa nakitaka Mhe. Mwenyekiti, ni kidogo sana kwa Mhe. Waziri, labda alikuwa hajanifahamu hii lugha yangu mimi unajua natoka kijijini kule Mkwajuni mbali kutoka kule mpaka huku. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kidogo atupe maelekezo ya hizi shilingi 50 milioni anazozitaka, kidogo tu atufafanulie matumizi yake ili tuseme sawa twende zetu. Sina kitu kingine mimi Mhe. Mwenyekiti, atoe tu, labda anataka kufanya vi-*partition* mule, anaongeza ngazi katika hizi, hicho tu ndicho ninachokitaka Mhe. Mwenyekiti, nikishapata hicho kwa busara zako sina tatizo tutaendelea tu. Atwambie Mhe. Waziri atafanya nini katika hizi basi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mtando mimi nadhani tukimtaka aseme misumari mingapi atanunua, saruji *packet* ngapi, nadhani hiyo tungeacha hebu turuhusu hili fungu liendelee. Maelezo mengi sana tushapewa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Jumla ya kifungu Idara ya Utumishi na Uendeshaji shilingi 1,247,264,000/-

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Makame Mshimba sasa tupumzike hapo tena, maelezo mengi yashatoka hapo.

Kifungu 1601 - Kitengo cha Ofisi ya Usalama wa SMZ

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi tofauti na wengi nilivyokuwa nikichangia katika Kitengo cha Ofisi ya Usalama wa SMZ nilisema bado naona haja ya kuendelea kwake na kinyume na huko kwengine nilikohoji matumizi makubwa hapa Mhe. Mwenyekiti, nilieleza *concern* yangu katika mchango ambao katika ufafanuzi wa Mhe. Waziri sikusikia akinisaidia, aliwajibu zaidi wale ambao walionesha *concern* ya kutaka kisiwepo. Lakini mimi nilisema kwamba hivi kilivyo na kwa kutambua umuhimu wake yale mengine naamini tutajirekebisha kama mfumo wetu wa kisiasa ulivyobadilika. Lakini nilisema ukiangalia namna ya mazingira ya wanavyofanya kazi bado ni magumu. Unajua hawa kimsingi pengine ni watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na ndio maana hata katika fungu humu hawana mishahara wana posho za *over time* na vitu vingine.

Lakini nilisema kuna kitu cha msingi Mhe. Mwenyekiti, kama vile usafiri wao. Kwa sababu bahati nzuri tunamokwenda mwingi tunawakuta hawa wanatangulia wao kwanza kabla hawajaja viongozi au hata kabla sisi tulioalikwa hatujafika. Sasa ni aibu Mhe. Mwenyekiti, kwamba watu kama hawa wanaomba *lift* kwa viongozi waliokwenda katika shughuli kama zile. Katika mchango wangu nilisema hilo, nilimuomba waziri katika hili aje atusaidie, ana mpango gani wa kuwasaidia huduma zao za msingi.

Katika bajeti hii Mhe. Mwenyekiti, ukitizama sina haja ya kusema moja moja lakini kuna vifungu kwa mfano vya mafuta na mambo mengine, lakini lile suala la msingi la kupatiwa usafiri wao wa kuweza kuwahudumia katika kazi zao za kila siku nafikiri ni suala la msingi, hasa tukizingatia mara nyengine siku moja kunaweza kuwa na shughuli moja, mbili, tatu ambazo wanazihudumia na wao wanatangulia. Kwa hivyo, nilikuwa nataka Mhe. Waziri kwa hili anisaidie wana mpango gani wa kuwasaidia kitengo cha *GSO* ili kuweza kufanya kazi zake vizuri na kitaalamu kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti, punde tu hivi kama wanavyofanya wenzao walioko Dar es Salaam kwa mfano pale. Naomba Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana kwanza kwa *concern* yake Mhe. Ismail Jussa, kwa kweli alivyosema ni vyema kabisa si vyema watu hawa wakawa wanachupia chupia *lift* tu. Na niseme tumeliona hilo serikali na tuko njia sio tuko mbioni, tuko njiani kwamba tayari maana yake nakusudia gari zimeshaagizwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Wizara ya Fedha na kuangalia hasa mahitaji kwanza ya hao wenzetu wa kitengo ili kuwasaidia. Hivyo alivyosema kweli hawa wanakuwa kama *advance part* Mhe. Rais anapokwenda watangulie mapema.

Lakini ningeomba Mhe. Jussa kidogo asiwachanganye na hawa wale aliosema *GSO*, hawa ni tofauti kidogo. Lakini *concern* yake tumeisikia na niseme iko njiani maana yake kidogo mambo yashapata mwelekeo bado kufika tu mutukari hizo na wao nafikiri shida hii tutawapunguzia, tumesikia kilio chake. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwanza Mhe. Waziri kwa kunielimisha na ndio kawaida yetu, tunapoona kwamba tumekosea tunakubali marekebisho. Kwa hivyo, nashukuru kwanza kwa ufafanuzi alionitolea kutofautisha shughuli zao na kama ikiwa malengo kama alivyosema ni kuwapatia usafiri basi nimeridhika naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 1601	Kitengo cha Ofisi ya Usalama wa SMZ	54,858,000/-
Kifungu 1801	Kitengo cha Mawasiliano na Habari	174,894,000/-
	Jumla ya Fungu:	**6,507,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 17 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri nilitaka kupata ufafanuzi juu ya shamba la mbogamboga kule Bambi, lakini Mhe. Waziri alipokuwa anajibu hapa sikumfahamu vizuri. Sasa nilikuwa naomba maelezo yale niliyokuwa nayahitaji hasa juu ya shamba la mbogamboga, nilitaka kujua maana yake ile faida ambayo Serikali inapata, mana lile shamba pale tumeshaingiza fedha nyingi, kipindi kilichopita tuna *one billion* tumeingiza pale. Sasa nataka kuona mradi ule faida tunayoipata sisi kama SMZ. Kwa sababu tuna ushirikiano baina ya Serikali ya Misri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa naona kila kitu kinakwenda Misri, maana yake mpaka kile kinachopatikana kama mapapai kumi yanayouzwa pale wanakusanya Wamisri, hebu nataka kujua sisi hasa tunafaidika na nini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, tulieleza kwa kirefu kabisa faida ambazo shamba lile linatusaidia, lakini naomba nirudie tu kwanza shamba lile linatumia kwa utafiti na uzalishaji wa mbegu na nimetaja hasa kwenye *script* mbegu ambazo za mtama, mahindi na mbegu ya mpunga ya Nerika kwa mwaka huu wa fedha uliopita ambayo tumezalisha zimepelekwa kama ilikuwa *multiplication* sisi tumepeleka. Lakini mbegu mpya pia pia zinazokuja wanazijaribu pale, wanafanya utafiti wa kwenye umwagiliaji na lile limekusudiwa kama ni *model farm* ya uzalishaji mbegu na wenzetu wa Misri.

Kwa hivyo, ni faida kubwa sana kabisa na tunashirikiana na wenzetu wa kilimo, wako maafisa wa Kilimo pale ambao wana mradi wa uzalishaji mbegu wa Bambi na tunafanya kazi kwa pamoja. Kwa kweli faida ni kubwa sana. Lakini labda niseme pale niliporudia Mhe. Mtando labda walipokwenda pengine walikwenda *off season* na unajua ukienda wakati huo kidogo ukame ule na nini utaona hakuna uzalishaji wowote. Lakini mimi namualika sasa hivi twende tuko kwenye *on season* aone hali ilivyo. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anajaribu kueleza sijui kilimo mimi nataka ile faida ambayo sisi tunapata, maana zile fedha tulizoingiza pale ni nyingi sana Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi zaidi ya mwaka wa nne au watano tunaendelea kupeleka fedha lakini faida ambayo inapatikana kwa fedha zile tunazopeleka pale, sisi tunategemea tuzalishe tupate faida, hebu niambiwe kile ambacho tunakipata kama serikali zaidi ya hiyo kufanya utafiti wa kilimo na nini, sawa tunafanya utafiti wa kilimo lakini zile pesa ambazo tunaziingiza pale tunaingia kwa ajili ya kuzalisha nini tunakipata sisi. Ndio hoja yangu nataka kujua tunachokipata pale kutokana na fedha ambazo tunaingiza, itakuwa kila siku tunaingiza fedha tu tunafaidisha wengine.

Mimi wasi wasi wangu kwamba mradi ule hautufai na bora tuuwache kuliko kuwa tunaanza kuuingizia tena fedha. Kwa sababu na hapa naona zimo fedha nyengine lakini mara hii sio nyingi sana, lakini ni nyingi milioni ishirini na moja si kidogo hizo zinatakiwa zipelekwe pale. Sasa mimi napata shaka Mhe. Mwenyekiti, hebu Mhe. Waziri ajaribu kutueleza kidogo tupate ufafanuzi zaidi katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, najaribu tena kumfahamisha na kumuelekeza Mhe. Mtando, narudia tena lile shamba linatumika kufanya utafiti, uzalishaji mbegu utafiti unatia pesa matokeo ndio faida yenyewe. Haya narudia tena tumezalisha mbegu na nimemwambia mbegu za mtama, mahindi na mbegu za mpunga tumezitawanya tukawapa wakulima. Hizo ndio faida zenyewe, sasa hazioni Mhe. Mtando hizi?

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naziona hizo, lakini mimi nataka nimuulize. Ile dhana ya kuanzisha ule mradi hasa maudhui ni nini? Kufanya utafiti au maudhui ni shamba la mbogamboga ambalo litakuwa linazalisha na kufanya ile biashara? Hebu anisaidie hili, mana pale tuna ubia baina ya Misri na Serikali ya Mapinduzi zana yake ya kuanzisha ule mradi hebu atusaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, lile jina la mradi wa mbogamboga hakuna mradi wa mbogamboga mpaka sasa hivi, hayo niliyomwambia ndio madhumuni ya shamba lile. Unajua vitu hivi Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine uone kwa macho kidogo, mimi naomba kesho au siku yoyote atakayopanga yeye lakini wakati huu wa *season* sasa hivi *field visit* nimvalishe *gumboot* kidogo mana kule kuna tope na dongo jekundu kama la jimboni kwake, twende kidogo ashuhudie kile kinachofanyika. Kumejengwa *dam* la kuzalisha maji kubwa kweli kweli sijalionapo mimi hapa, mapesa mengi sana yametumika, kuna mitandao ya umwagiliaji *sprinkle* zile zinamwagika, hiyo *invest* anayosema ni kweli ni kubwa mno.

Sasa mimi namualika yeye pamoja na kamati Mheshimiwa twende tukatembelee aone mwenyewe na matunda yanayozalishwa mabilingani na vitu vingine. Wale Wamisri wamezowea kuchezea jua wamebadilika rangi hasa baada ya ule weupe wamekuwa weusi kwa wanavyojituma. Sio wato tu na watu wetu kabisa sasa faida ndio hizo. Mimi nasema labda hili jina lina *miss lead* kidogo, lakini tushaeleza utafiti na uzalishaji mbegu pamoja na uwo ni *model farm* na tunashirikiana na wenzetu hao wa Misri.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri Mhe. Waziri hajanifahamu, kwa sababu sisi tumeshafanya ziara pale, kamati yako ya Baraza ya *PAC* Mhe. Mwenyekiti, imeshafanya ziara, palikuwa pana *query* ya Mdhibiti juu ya matumizi ya zile fedha maana zimeonekana fedha zimetumika kuliko kilichozalishwa. Value for money haipo, *one billion* Mhe. Mwenyekiti, tumeuliza kimezalishwa kitu gani hakifiki hata shilingi laki tatu si kwambii shilingi milioni tatu, lakini bado tunaingiza tena fedha kwa ajili ya mradi ule mradi ule haukuwekwa kwa ajili ya hiyo anayosema yeye Mhe. Waziri.

Sisi tumeona mpaka huo mkataba ni shamba la pamoja la mboga mboga baina ya Serikali ya Misri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao utakuwa unasimamiwa na JKU. Huko mwanzoni sijui uende Wizara ya Kilimo nafikiri wakapiga piga mateke wakapewa JKU, JKU wamepewa pale wao kama watizamaji tu imekuwa kama yule Mmisri ndiye mwenye shamba, kulikuwa kuna *query* ya Mdhibiti pale na haijajibika mpaka leo mana wameshindwa

kutoa maelezo katika hili. Sasa ndio nataka kumwambia Mhe. Waziri huu mradi hakuna haja ya kuupelekea tena fedha kwa sababu hatuuoni, ile *impact* ya ule mradi zile fedha tutakuwa tunaingiza tu, lakini sasa uzalishaji wake haupo hakuzalishi kitu. Hiyo dhana iliyokusudiwa pale sio anayosema Mhe. Waziri imekuja kubadilika sasa hivi baada ya kuona hakuzalishwi kitu wanafanyia utafiti watu wa kilimo kwa sababu halina kazi ati lile shamba. Lakini ni mapesa mengi ambayo tunayaingiza pale faida yake haionekani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri katika hili sijapata maelezo ya kutosha, Mhe. Waziri hebu atusaidie zaidi kidogo, hii kusema twende pamoja tufanye nini, sisi tumeshakwenda kama kamati sina haja ya kwenda na Mhe. Waziri tu kwa kesho. Kamati yako Mhe. Mwenyekiti, ya Baraza hili imekwenda pale imeona yale madudu na tukakubaliana kwamba hakuna haja hapa ya kuingiza fedha tena kwa sababu huu mradi hautunufaishi, ni bora tufute ule mkataba sasa na wale wa Misri na kila kitu ibakie JKU wapewe wenyewe wanaweza kuliendesha wakafanya wanavyotaka kuliko kuendelea tukawa tunafunga mikataba na wale watu lakini hakuna faida inayopatikana. Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakuwa amenielewa vizuri kidogo lile ninalolikusudia.

Mhe. Mwenyekiti: Kama ni mradi na umetengewa pesa hebu tuzungumze zaidi kwenye hizo pesa za mradi, moja. Lakini pili huwa naogopa sana kwamba Baraza hili lifute miradi, mkataba nakusudia, huwa naogopa sana. Kwa sababu mikataba ina *consequences* zake, unaweza ukafuta mkataba ukajikuta kumbe sasa wewe ndiye unayepata hasara, inapokuja *issue* ya kupelekwa Mahakamani hatimaye unajikuta wewe ndio unapata hasara. Lakini kwa kifupi nasema kwamba, kwa kuwa ni mradi tunaouzungumzia basi hebu tuone huko kwenye pesa ya miradi nadhani kumetengewa pesa huku na ndizo mnazodadisi kwamba pesa hizo zinazoingizwa kwenye mradi ule hazizalishi kile kitu kinachotegemewa kizalishwe. Hii fedha ya uendeshaji wa hapa tumalize tungoje kwenye hiyo kasma ya miradi ambayo iko kwenye ukurasa wa 700 nafikiri ndio kuna fedha za miradi tuone je, fedha hizo zinafaa, nyingi, hazitoshi au namna gani. Lakini hapa uendeshaji wa ofisi hii nadhani tungeendelea.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa busara zako tuendelee.

Jumla ya Kifungu

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na ili kuokoa muda na kuepuka kumsimamisha kila mara Mhe. Waziri kuna hoja moja niliitoa naomba hii akinijibu kwa hapa iwe imehusu vikosi vyote vitano. Nilihoji juu ya suala la bajeti iliyokuwa katika *vote* 2112100; *sub vote* 211204 ambayo hiyo inajirejea kila pahala katika vikosi vyote, huduma za chakula cha askari.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi nataka niseme sina tatizo la kuongezwa bajeti ili askari wetu wale vizuri, wawe na utulivu waweze kufanya kazi ya kutulinda vizuri, sina tatizo na hilo. Lakini nilihoji kile kima cha uongezekaji na nikasema kwamba mfano, Kikosi cha Mafunzo naelewa kwa sababu waziri alitwambia wanakusudia kuongeza milo mitatu kwa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo pamoja na askari wao. Lakini sasa niliomba maelezo kwa jumla na naomba katika hili anisaidie kwa yote kwa pamoja, kwamba fedha hii kwa mfano katika JKU hapo ilipozungumzwa imetoka shilingi 38 milioni mwaka jana hadi 380 milioni, hilo ni ongezeko la asilimia 1000.

Sasa nilikuwa naomba waziri anisaidie tu kwamba huko nyuma kilikuwa chakula hiki kinatolewa vipi na hivi sasa kinategemewa kutolewa vipi ili ku *justify* ongezeko hili. Nikiridhika na hilo Mhe. Mwenyekiti, sina tatizo nitaruhusu bajeti iende naomba anipatie maelezo. Kama nilivyosema si kwa hili tu kwa vikosi vyote ili nisiendelee kumsimamisha katika kila kikosi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa kwa kutaka kufahamu zaidi juu ya hili ongezeko. Tulikuwa na matatizo ya maaskari wetu kwanza wakiwa mafunzoni lakini hawapati chakula, walikuwa wanajigharamia chakula. Sasa tumeliondoa hilo wakiwa mafunzoni wakati wote sasa serikali au vikosi vyao vitawahudumia chakula hilo moja. Ndio maana utaona kuna *increase* hiyo.

Lakini pili tumesema maaskari wote ambao wako kambini wakati wote sasa watawajibikiwa kula kambini. Sasa inategemea *variation* kwenye kikosi ukubwa wake, ndio utaona tofauti wakati mwengine kubwa zaidi nyengine ndogo zaidi. Lakini sasa hivi serikali imeamua kwa hili tujipinde tunamshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha lakini maaskari wetu wale vizuri, hayo ndio maelezo niliyotaka kumpa tu Mhe Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo fasaha naomba nihakikishiwe moja tu halafu tukae tuendelee, kwamba kwa maelezo hayo aliyonipa Mhe. Waziri anakusudia kunambia kwamba yale makato waliyokuwa wakikatwa askari kuanzia sasa itakuwa si halali katika masuala mazima yanayohusu posho ya chakula wanapokuwa wanakwenda mafunzoni ambapo walikuwa wakikatwa kule, atoe hiyo kauli askari wake wasikie na baada ya hapo naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kuanzia sasa nasisitiza tena na Makamanda wananisikia, kwamba maaskari wote wasikatwe kwa posho ya chakula, hivyo hawatokatwa tena.

Kifungu 0201 Utawala Unguja	shs.7,504,000,000/=
Jumla ya Fungu	shs.7,504,000,000/=

FUNGU 18 CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 Idara ya Vyuo vya Mafunzo

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia katika Chuo cha Mafunzo nilizungumzia sana kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa pale chuoni, jinsi ya watu wanavyopekuliwa wakiwa uchi wa mnyama pamoja na kutumia mtondoo badala ya kutiliwa vyoo. Sasa majibu Mhe. Waziri sikuridhika nayo ninataka aniambie ni lini ndani ya magereza yetu mutajengwa vyoo na lini watu watapekuliwa watu wakiwa wafaragha badala ya kupekuliwa wakiwa uchi nje ya uwanja.

Mhe. Mwenyekiti: Maana nilijua tu mtondoo lazima utatoka tu pale.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Saleh kwa kutukumbusha hili. Ninafikiri nimeeleza kwamba tumeanza na ninakumbuka mwenyewe nilikwenda Kangagani, tukafanya mpango kule tukarekebisha mambo mazuri na hata Tungamaaa ninafikiri tumerekebisha.

Sasa mote humo lengo letu ni kurekebisha lakini kidogo urekebeshaji mwengine kama Wete una matatizo kwa sababu ya ile hali ilivyo. Lakini tumeshaanza kidogo sivyo ilivyokuwa zamani. Hiki chuo kipya tutajitahidi hilo ndio kabisa halitokuwepo.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, nimuhakikishie Mhe. Saleh kwamba kwa kweli tunapata credit kwa mabadiliko ya haki za binadamu serikali yetu, tulivyokuwa nyuma sivyo tulivyokuwa leo, hali imebadiliko ile experience aliyokuwa nayo wakati ule sasa hivi haipo tena.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, matatizo yaliopo katika Chuo cha Mafunzo hatukuanza kuyasema leo, nimesema mimi binafsi katika Mabaraza kadhaa yaliyopita nyuma.

Kimsingi sisi tumeapa hapa kwamba tutaitii Katiba ya Zanzibar. Inasikitisha sana ibara nambari 5 ya Katiba juu ya haki ya faragha inaendelea kuvunjwa. Leo ananiambia Mhe. Waziri kanijibu tutajenga na kujenga. Matendo yanakidhi haja maridhawa kuliko neno Mhe. Mwenyekiti, aniambie ni lini sasa magereza yote yatakuwa yameshatiwa vyoo ndani na watu badala ya kutumia mtondoo watatumia vyoo ni lini, kusudi tuweze kuweza kufuatilia.

Sio Mhe. Mwenyekiti, aniambie tu kwamba tupo mbioni au tumeshaanza. Hii inaonesha kuwa Pemba hakujaanza hata sehemu moja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, itakuwa vigumu kwa bajeti hii kubadilisha kwa mpigo mote lakini ninachukua ahadi Mhe. Saleh kama nilivyomwambia kuwa nimekwenda mwenyewe Kangagani, nimeshuhudi mwenyewe na nikatoa pesa mwenyewe kwa Afisa Mdhamini nikamuagiza na hali ni nzuri.

Kwa hivyo tumeanza. Naomba kutumia lile neno langu tuamini.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo linataka gharama na lile ambalo halihitaji gharama. Suala la ujenzi wa vyoo linahitaji gharama lakini la kumpekua mahabusu au mfungwa halihitaji gharama ni kutamka tu Waziri hapa kuanzia leo wakati makamanda wake wapo pale, kuanzia leo hakikisheni wakija watu munawapekua wakiwa faragha. Hili alitamke humu.

Watu wanapekuliwa wakiwa wazi kabisa sehemu ambazo hapana stara. Kwa hivyo leo atamke hapa Waziri awaagize makamanda wake kwamba wasimamie hii, maana yake makamanda wake wanavunja haki za binadamu na wanavunja Katiba ya ibara nambari 5 ya nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, tumesikia concern ya Mhe. Saleh na tutalirekebisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, sijamfahamu Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Rudia majibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ninasema kwamba tunamshukuru kwa *concern* yake na ninasema tumesikia na hiyo hali tutairekebisha kwamba isitokee tena.

Mhe. Mwenyekiti: Watarekebisha wasirejee tena.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, lugha nzuri ya kutumia kwa sababu sisi tukipitisha fungu hili itakuwa tunatumia pesa za walipa kodi kwenda kunyanyaswa pale, yaani kwenda kuvunjiwa heshima pale.

Sasa ninadhani Mhe. Waziri angesema kwamba kuanzia leo ninaagiza kuwa wakija mahabusu, wanafunzi wapekuliwa ili kila Mzanzibari afahamu hilo. Lakini tumefahamu tutajirekebisha katika jambo gani. Tusiwavunge wananchi, hebu tuwe very clear kwamba kuanzia sasa naagiza kwamba atakapokuja mahabusu au mwanafunzi apekuliwe faragha.

Hii ni lugha ambayo hata mkulima kule kijiji kwangu Vitongoni Mhe. Mwenyekiti, atafahamu hata Watumbatu na Nungwi watafahamu. Ninadhani ingekuwa vizuri ili Mhe. Mwenyekiti, ili tusitumie pesa za walipa kodi kwa kuwapiga makora kwa fedha zao, yaani kuidhinisha fedha za walipa kodi kwenda kuwanyanyasa kule, mimi ninadhani awe Mhe. Waziri very clear ili tusipoteze muda katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Saleh ninakubali kwamba tutajitahidi kuanzia sasa wanafunzi wanaokuja, wale mahabusu watapekuliwa, hii kupekuliwa hatuwezi kuepuka, watapekuliwa kwa faragha.

Mhe. Mwenyekiti: Nimemuona ametikisa kichwa kwa kukubali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipochangia sehemu hii ya Chuo cha Mafunzo nilisema kama malimbizo ya hawa askari wetu wanaosimamia wanafunzi kuwa wanapokwenda likizo hawapati malipo yao na pia fedha hizi za hali ngumu, wanapewa shilingi elfu moja na mia tano na nikalalamika kama kwa kweli shilingi elfu moja na mia tano hatuwatendei haki haziwezi kuwasaidia na nilisema kwa kelele kubwa, lakini Mhe. Waziri hakunijibu suala hilo.

Kwa hivyo naomba atupe maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Subeit alichangia suala hilo. Naomba kumuhakikishia tu sasa kwamba pesa za likizo zinatolewa kwa mpango maalum, kwa kila anayekwenda likizo ikifika wakati wake kwa mwaka ule basi wanapewa na alizungumza usafiri hilo tutajitahidi.

Lakini wale ambao wanakwenda baadae wanarudishiwa gharama zao na kama hawajarudishiwa basi tutalisimamia tuone kwamba linakaa sawa nalo ili lisilete usumbufu kwa maaskari wetu. Ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, unajua Mhe. Waziri ni mzuri sana wa maneno yake kujibu hayana utata katika kujibu lakini utekelezaji wake unakuwa ni mgumu.

Mhe. Mwenyekiti, muda umeshakuwa mkubwa tuendelee. Mimi ninamuani tuendelee lakini naomba akitujibu na utekelezaji uwende kwa sababu hiki ni chombo kizito, humu tunawatetea wananchi wetu na wanatusikiliza tukisema.

Kwa hivyo yale wanayoahidi viongozi wetu Mawaziri kwa sababu ndio watendaji wa serikali hii, basi waangalie kuyatekeleza. Tusije tukisema hapa halafu tukionekana kama tunakuja tukiimba tukiondoka. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu	shs.5,890,000,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.5,890,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201 Utawala	shs.9,650,000,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.9,650,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 32 KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru. Mimi nilimuuliza swali dogo tu Mhe. Waziri sijapata ufafanuzi.

Swali lilikuwa kwa nini hiki Kikosi cha Zimamoto majukumu yake makubwa lakini bajeti yake ni ndogo, na ndio maana yakawa yanatokezea mashaka makubwa katika kuzima moto.

Atupe kigezo gani anachotumia ili kutoa bajeti hii ya Kikosi cha Zimamoto.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama tungeona hayo mahitaji Zimamoto wanayoyataka ili waende kisasa basi mara tatu ya bajeti hii.

Lakini ndio ceiling tuliyopata. Sasa nilieleza kwamba kidogo kwa vifaa walivyonavyo wanajitahidi na tunazidi kuliendeleza lile jeshi la Zimamoto. Tatizo ni ile njia kidogo na ile mipango ya miji ilivyojengwa wanapata taabu zaidi kufika.

Lakini kwa vifaa wanajitahidi wana mtazamo wa mbele kila mara lakini kwa kweli ceiling iliyoopo tuliyopata kwa kikosi ni ndogo. Sasa tuendeleze mapato yetu tukisaidia na kikosi chetu. Ninafikiri tutajitahidi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inaingia katika mabadiliko makubwa. Kama nilivyosema mwanzo tuna kiwanja cha ndege cha kimataifa, mahoteli mengi na tunakaribisha wawekezaji.

Pattern iliopo hii haikuanza leo, ukirudia bajeti za miaka mingi kikosi hiki ndio kinachopewa bajeti ndogo kuliko vikosi vyote.

Sasa Mhe. Waziri ni nani anaeweka ceiling hii hata ikawa wewe unakubana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, ninadhani kaka yangu hapa Mhe. Rashid Seif Suleiman ameuliza swali zuri sana, nani anayeweka ceiling.

Ni uwezo wa serikali Mhe. Mwenyekiti. Uwezo wa serikali unapokuwa mzuri hali yetu kila taasisi zitakuwa nzuri na hata hivyo akiangalia mwaka jana, bajeti ya Kikosi cha Zimamoto cha mwaka jana na mwaka huu ambao tunaotaka kuanza sasa hivi ni tofauti kidogo, tumeongezeka kidogo.

Kwa hivyo ni lazima tu-appreciate kwamba hali kila inapokuwa nzuri basi taasisi zote zitakuwa nzuri.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, lakini akumbuke Mhe. Waziri kuwa kila kitu kimeongezeka, hakikuongezeka hiki tu.

Lakini ninamuomba yeye na Mhe. Waziri katika bajeti ijayo wajue kwamba kupanga ni kuchagua. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni kikosi muhimu. Bila ya hivyo nchi yetu itaingia katika mashaka ambayo tumeyakusudia.

Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, moja katika mchango wangu katika masuala ya vikosi nilizungumzia suala zima la utaratibu wa kutangazwa tenda katika shughuli zao kwamba zimekuwa hazipo hizi.

Sasa nilikuwa naomba anieleze hili Mhe. Waziri in relation kwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa sababu kama nilivyochangia kwamba kumekuwa na manunuzi pale, kwa mfano ya magari ambayo watu wengi wanalalamikia kuwa yapo chini ya viwango ndio maana yameshindwa kazi na askari wenyewe wamekuwa na malalamiko pale.

Hata kamati ya Mhe. Hamza Hassan Juma ilipokwenda pale yaliondoshwa yakapelekwa Airport ili asiyaone kutoka pale Kilimani yalipokuwepo.

Sasa ninataka kuuliza Mhe. Waziri kuwa na hizi taratibu za kufuata za tenda, kama zilivyo tenda nyengine za SMZ na sheria ile ya procurement imewafunga wote ana kauli gani kuhusiana na vikosi hivi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli suala hili lilikuja mpaka serikalini tukalifanyia kazi na tulichofahamu kabla kama nilivyosema kwamba zile tendering committee zilikuwa hazijafanywa.

Lakini baadae zikaundwa na sasa utaratibu wote utafuatwa. Hakuna pingamizi ushauri wake Mhe. Jussa tumeusikia.

Lakini lile suala lilipita kwenye mchakato mzima wa tendering committee ya ndani ya kikosi, wana utaratibu wao wenyewe wa kila kikosi wa tendering committee. Hivyo fahamisho walifanya ule utaratibu wote ukapelekwa serikalini.

Mhe Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0201 Utawala Unguja shs.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia jana niliuliza kuna utaratibu gani Mji Mkongwe kupata huduma za fire.

Na record zinaonesha kuwa si muda mrefu katika mwezi mmoja Mji Mkongwe umepata maafa ya umeme kuungua nyumba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nilieleza kwa kirefu kwamba tumejitahidi vifaa na magari tunayo, lakini tatizo la Mji Mkongwe zile narrow street kufika kwenye yale matukio kidogo ndio matatizo.

Sasa hata zamani kulikuwa kuna vile visaruji na nilisema kwamba kile kikiwepo kile ina maana na mpira wa maji pale ndio unapofungulia. Sasa wote ule mtandao umekufa, inabidi mfano gari kama lile tokezeo la juzi gari inabidi likae barabarani halafu mipira ya maji waunge kufikia kule.

Sasa naomba tushirikiane na Mhe. Jaku na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe tuvifufue vile vituo na maji yale kama hamna, lakini alau wakati mwengine uwongo tunaweza tukayagida tukasaidia hiyo hali. Tatizo ndio hilo tu kwamba ule mtandao uliopo kwenye tukio inakuwa shida kuufikia.

Mhe. Jabu Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0201 Utawala Unguja	shs.3,099,000,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.3.099,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 34 KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 0201 Utawala Unguja	shs.3,784,000,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.3,784,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 37 MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Kifungu 0401 Mpango na Sera	shs.354,680,000/=
Kifungu 0501 Wilaya ya Mjini	shs.410,267,000/=
Kifungu 0601 Wilaya ya Magharibi	shs.334,053,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.1,099,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 38 MKOA WA KUSINI UNGUJA

Kifungu 0401 Mipango na Sera	shs.332,444,000/=
Kifungu 0501 Wilaya ya Kati Unguja	shs.395,282,000/=
Kifungu 0601 Wilaya ya Kusini Unguja	shs.336,274,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.1,064,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 39 MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Kifungu 0401 Mipango na Sera	shs.286,048,000/=
Kifungu 0501 Wilaya ya Kaskazini "A"	shs.386,696,000/=
Kifungu 0601 Wilaya ya Kaskazini "B"	shs.320,376,000/=
Kifungu 0701 Wilaya Ndogo Tumbatu	shs.89,880,000/=

Jumla ya Fungu **shs.1,083,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 40 MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu 0401 Mipango na Sera	shs.471,531,000/=
Kifungu 0402 Baraza la Mji Chake-Chake	shs.363,000,000/=
Kifungu 0403 Baraza la Mji Mkoani	shs.209,000,000/=
Kifungu 0501 Wilaya ya Chake-Chake	shs.346,629,000/=
Kifungu 0501 Wilaya ya Mkoani	shs.350,840,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.1,741,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 41 MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu 0401 Mipango na Sera	shs.294,722,000/=
Kifungu 0402 Baraza la Mji Wete	shs.275,000,000/=
Kifungu 0501 Wilaya ya Wete	shs.378,270,000/=
Kifungu 0601 Wilaya ya Micheweni	shs.303,787,000/=
Kifungu 0701 Wilaya ya Kojani	shs.132,228,000/=
Jumla ya Fungu	**shs.1,384,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 43 OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kwa ufupi bajeti hii na baada ya kusikia kuwa baadhi ya majimbo hapa Unguja watu wote wanapewa vitambulisho, nilisema kuwa Pemba sio hali ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu kuna watu chungu nzima hawajapata vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi. Mhe. Waziri alipojibu, kaleta sheria zake kwamba uwe na cheti cha kuzaliwa, kama huna uwende mahakamani na kadhalika, na pia sheha akutambuwe kuwa ni mtu wake na mengineyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, yote hayo yanayosemwa hayamo kikamilifu katika katiba. Kwa hivyo, wananchi wanakoseshwa haki zao na ni kinyume na katiba yetu ya mwaka 2010 iliyoeleza. Je, Mhe. Waziri ataniambia vipi kuhusu wale watu ambao umri wao umeshatimia miaka 18 na wanapokwenda kwa sheha, hawapati barua za kwenda kuchukua vitambulisho na sheha anawaambia barua zimekwisha na wale watu ambao hapo mwanzo walikuwa ni wapiga kura na vitambulisho vya kupigia kura wanavyo, lakini hawana vyeti vya kuzaliwa pamoja na kuwa katiba haisemi hivyo.

Kwa hivyo, kwa ufupi Mhe. Waziri ataniambia vipi kuhusu wale wote ambao wameshatimia umri wa miaka 18 ambao hawajapata na wale watu ambao walikuwa ni wapiga kura katika kipindi cha nyuma, lakini kipindi hiki cha juzi wakaachwa kwa makusudi. Naomba Mhe. Waziri anieleze vipi hawa watatatuliwa matatizo yao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, najitahidi sana kueleza kwa kirefu sana utaratibu unaotumika na pale panapotokea matatizo tufanye nini.

Sasa mimi namuomba Mhe. Salim Abdalla Hamadi, kwa sababu ya kuokoa muda, hayo matatizo ya upande wake, mimi niko tayari nitatoka kwende zetu tukaonane na Mhe. Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na sheha tulimalize ili wenye haki ya kupata vitambulisho, basi wapatiwe kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, suala hili sio la Jimbo la Mtambwe tu, hili ni suala takriban la majimbo yote 18 yalioko Pemba. Wote wale waliopiga kura zamani, ulipokuja usajili mpya hapa juzi na ikawa hawana vyeti vya kuzaliwa, japokuwa wameshapiga kura zamani walikoseshwa. Wakati katiba Mhe. Mwenyekiti, inasema hivi, 'kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar na wananchi, na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya kijifungu cha (2) cha kijifungu hiki, pamoja na masharti mengine ya katiba hii na ya sheria iliyotumika Zanzibar kuhusu mambo ya uchaguzi.

Sasa kifungu hiki cha 2 kinasema hivi, 'Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria na kuweka masharti yanayoweza kuzuwia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura, kutokana na yoyote kati ya sababu zifuatazo. Sababu zenyewe Mhe. Mwenyekiti, ni nyingi, lakini mimi naisoma hii ya kifungu (d).

Kifungu cha (d)

1. 'Kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri,
2. Au kitambulisho cha uraia,
3. Au uandikishwaji kama mpiga kura.

Sasa wako wengi walioandikishwa kama wapiga wamekoseshwa. Kwa hivyo, hili sio suala la Jimbo la Mtambwe tu, ni suala la Pemba nzima. Kwa sababu katiba hii iliyotungwa na wananchi, inasema hivi katika kifungu cha 4.

Kifungu cha 4

'Katiba hii ni katiba ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote, isipokuwa kutokana na kijifungu cha 80. Hicho nilichokizungumza hapa, ikiwa sheria yoyote itatofautiana na katiba hii, basi katiba hii ndio itakayokuwa na nguvu na sheria hiyo, itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kimehitilafiana.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni katiba ya wananchi na kifungu hiki kimo katika kifungu cha kwanza cha sura ya kwanza, ni jumla ya vifungu ambavyo haviwezi kubatilishwa mpaka kwa kura ya maoni. Kwa hivyo, ina maana katiba hii ni ya mwisho kuliko hizo sheria za nyuma, ilikuwa zifutike moja kwa moja na hii katiba ifuate mkondo wake.

Kwa hivyo, kwa sababu tulikiuka katiba, mimi nataka nijuwe hao wote waliopiga kura na vitambulisho wanavyo, ni wazee wala hawana matatizo ya umri kwa nini wakazuiwa na ni kwa kifungu gani.

Kwa nini sheha aseme fomu hakuna na wakati fomu ni kutoa kopi tu akawapa watu wakapata haki zao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salim Abdalla, katoa maelezo marefu sana. Lakini mimi nimeshamueleza utaratibu na kama kuna matatizo, yeye basi ndio anakata *appeal* kwa waziri. Mimi nakubaliana na yeye kuwa hayo matatizo yapo sikatai. Sasa twende zetu *field*. Mkurugenzi wangu wa vitambulisho ananisikia yupo, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba yupo. Twende kwa pamoja tukayatengeneze ili kila mtu apate haki yake Wazanzibari, hakuna tatizo Mhe. Salim Abdalla. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa jibu la Mhe. Waziri, lakini ningeomba kuna jambo moja liko wazi kabisa, hili sio la kwenda kufanya uchunguzi na linajulikana. Katiba inasema wote wenye vitambulisho vya kupigia kura, hao ni wapiga kura na wameachwa kwa makusudi kwa sheria ambayo hatujui ilikuwa wapi.

Kwa hivyo, mimi kauli ninayoiomba ni kwamba hatujui Mhe. Waziri atakuwa na nafasi siku gani, kwa sababu keshaahidi mambo chungu nzima humu. Kwa vile wakuu wa mikoa wapo na wakuu wa wilaya wanaofanyakazi na masheha wapo na mambo haya yanasababishwa na masheha wao. Kwa hivyo, ningemuomba atowe maelekezo tu kwa wale ambao wanavyo vitambulisho vya kupiga kura kwa chaguzi zilizopita, basi katiba ifuatwe ili wapewe hii haki yao, ili waweze kwenda kabla huyo Mhe. Waziri hajenda.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, hili suala la fomu alitolee ufafanuzi, sio suala la kufuatilia. Mimi nilikula kiapo na nikisema kitu ambacho sicho hapa, basi nitakwenda kinyume na utaratibu. Katika jimbo langu wako wanaokwenda sheha anawaambia kanunuwe fomu, wanasema sina. Sheha mwengine anasema sisi hatujaambiwa tutowe vitambulisho, kwa hivyo, inakuwa ni adha tupu. Kwa hivyo, hili ni suala la kutoa maelekezo tu, yeye mwenyewe sheha akishamkubali kuwa huyu kweli ni mzaliwa katika shehia yake, basi hakuna sababu akose kitambulisho wakati cheti cha kuzaliwa anacho na hao waliokoseshwa kwa makusudi, pia ni kutoa maelekezo tu, halafu tukienda huko isiwe tunakwenda kutoa misimamo, lakini ni kuangalia utekelezaji.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, bado naomba kumnasihi na kumuomba Mhe. Salim Abdalla Hamad. Matatizo aliyoyasema mimi sikatai, itakuwa yapo yametokezea. Sasa twende pamoja, au sio lazima niende mimi, yeye mwenyewe tu. Iko Ofisi ya Wilaya kule ya Msajili, sisi tutamuagiza ofisa wetu aende na yeye wakakae pamoja kule, wawatengeneze ili waone tatizo likowapi, kwa mujibu wa utaratibu wanaostahiki wote basi wapatiwe vitambulisho. Hatutaki wanyimwe, lakini hizo taratibu ziliopo zifuatwe na yeye mwenyewe atuelekeze huko kwenye matatizo ili twende.

Mhe. Mjumbe, anasema waziri nimeahidi mengi. Mimi ndio waziri naahidi, lakini watendaji wangu wananisikia. Kwa hivyo, suala hili na wao tunalichukua kwa pamoja. Mimi ndio nasema, hawawezi wao kunisemea mimi hapa, mimi ndio nakubali, hayo ni yetu sasa hivi, ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, sipendi kuwa mkali, lakini natoa ushauri. Katika kipindi kilichopita kulitokea matatizo kama haya, tukamuomba aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Kiongozi, twende tukalifuatilie hili suala akaingia mitini. Kwa hivyo kwa kutahadhari hivyo ninaloomba kwa kuwa ni suala zito linalomgusa mwananchi na haki yake, basi tufanye utaratibu wa mheshimiwa kwenda atukusanye wawakilishi wote kule Pemba, na kila mmoja aliyekuwa na vielelezo vyake alete mbele ya wakuu wa mikoa wote, wakuu wa wilaya pamoja na masheha angalau atowe tamko ambalo litaondoa utata wote. Naomba jibu kwa sababu ni la kitaifa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia katika Ofisi hii ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, kwa masikitiko makubwa Mhe. Mwenyekiti, nilisema hapa na nikanukuu Hansard ya Mhe. Mshimba, kwamba kuna baadhi ya watu ambao sio Wazanzibari, kama vile Wakenya, Wamsumbiji na Waganda wamepewa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Nikaeleza wasi wasi wangu kwamba kuna siku Baraza hili litakuja kuwa na Wakenya na Waganda.

Je, Mhe. Waziri atanieleza nini kuhusu hawa ambao wamepewa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, wakati sio Wazanzibari ni lini watanyang'anywa. Pili, vile vile nilieleza kwamba ofisi hii ina ubaguzi. Tena kumbe Mhe. maalim Salima Abdalla kasema Wapemba tu kule hawapewi, lakini kumbe hata hapa Unguja kuna maeneo mengine wanawabagua.

Kwa mfano, Mhe. Salmin Awadh Salmin kasema hapana matatizo katika jimbo lake, watu wanapewa kama kawaida, lakini Mhe. Makame Mshimba hapa hapa Unguja, anasema kwamba huko kwao hawapewi. Kwa hivyo, ofisi hii ina ubaguzi mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazuwia shilingi hapa mpaka pale atakaponiambia waziri, ni lini itafanywa power study hapa Zanzibar, kufanya feasibility study ya wale wote waliokuwa hawahusike wananyang'anywa vitambulisho na ni lini waliokuwa wana haki ya kupewa vitambulisho hivi wanapewa.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi nazuwia shilingi katika bajeti ya wizara hii, mpaka pale nitakapopata maelezo ya kutosha, kwa kunitajia hasa, kwamba ni lini waliokuwa hawahusiki wananyang'anywa na wale waliokuwa wanahusika wanapewa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza ile karatasi aliyozungumza Mhe. Makame Mshimba na mimi ninayo hapa. Kesi za wanashakiwa wageni 14, aina ya kesi, anashakiwa na uraia wa Comoro na watu kama 10 hivi wanashukiwa na uraia wa Kenya. Wengine watatu wanashakiwa na uraia wa Msumbiji, maelezo yao ni kwamba kesi mfano watano hawa kesi zao ziko mahakamani, wengine kesi zao ziko uhamiaji na wengine kesi zao ziko polisi.

Kwa hivyo, kesi hizo zote zinashughulikiwa ipasavyo, halafu mwishoni watanyang'anywa ule Uzanzibari Ukaazi waliopewa, kesi zikishamalizika na ikithibitika tu tutawanyang'anya, hizo kesi ziko mikononi mwa sheria.

Lile suala alilosema nimuhakikishia, Mhe. Mwenyekiti, sikulipata vizuri.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilizungumzia suala la GNU, yaani *spirit* ya GNU ni kuleta *national unit* na wale wenye *spirit* ya GNU, pale anaponipa maneno haya na kutonitajia kwamba ni lini waliokuwa hawahusiki watanyang'anywa na wanaohusika watapewa vitambulisho hivyo, mimi simfahamu Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea kusema kwamba ni vyema iundwe kamati teule ya Baraza lako hili ili ifanywe *study* ya waliokuwa hawahusike wote wanyang'anywe na waliokuwa wanahusika wapewe vitambulisho hivyo. Mhe. Mwenyekiti, hii ni dhulma wanafanyiwa Wazanzibar, na wakati hii ni haki yao ya msingi.

Naendelea kusema kwamba Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, watu wanakosa ajira katika nchi hii, kwa sababu bila ya kitambulisho cha Mzanzibar hupati, wanakosa *pass port*. Watu wanafanywa manokoa katika nchi yetu. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, napendekeza aidha iundwe kamati teule ya Baraza hili kufanya *study* ama anihakikishie waziri, kesho au keshokutwa. Mimi aliniahidi Mkurugenzi wa Vitambulisho, nikampelekea umma akanikimbia. Ssa nashindwa kuamini maneno yao hawa.

Mimi nadhani jibu zuri litapatikana Mhe. Mwenyekiti, pale itakapoundwa kamati teule, kinyume na hivyo, mimi nitaendelea kukamata shilingi mpaka pale nitakapopata jibu la kurishisha juu ya hiyo kamati teule au ni lini tutakwenda kulishughulikia hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ambayo Mhe. Waziri ameyatoa kuhusu suala la vitambulisho vya Mzanzibari. Mhe. Mwenyekiti, suala hili limeonesha kuzungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, wakiwa na wasi wasi mkubwa kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba serikali imeyapokea kwa undani sana, malalamiko ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wameyatoa kuhusu utaratibu wa upatikanaji wa vitambulisho vya ukaazi wa Mzanzibari. Ni wajibu wa serikali kuhakikisha haki za wananchi wake zinalindwa na ni wajibu wetu ndani ya serikali kuona kila mmoja anapata haki yake. Kwa kuwa jambo hili limelalamikiwa, inaonekana wazi yapo matatizo.

Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe watupe subira, ili serikali ilishughulikie jambo hili kwa kina sana, ilifuatilie ile pale penye tatizo ilitatuwe na wananchi wote waweze kupata haki zao za msingi, ikiwemo kupewa kadi zao za ukaazi, ili kadi hiyo iwawezeshe kupata haki yao wakati wa kupiga kura na waweze kupiga kura bila ya matatizo na zile haki zao nyengine zote za msingi ambazo zinatokana na kuwanacho kitambulisho hiki waweze kupata.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ameeleza sana na inaonekana sana, na inaonekana Waheshimiwa Wajumbe bado hawajaridhika na jambo hilo. Tuwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe watupe fursa ili tulifuatilie jambo hili kwa kushirikiana na wizara husika na serikali kwa ujumla wake ili kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake na malalamiko haya yaweze kuondoka na yasiweze kurudiwa tena katika Baraza lako hili tukufu. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kuna sanaa za maonesho na kuna sanaa ya maneno. Napata wasi wasi katika hili kwamba majibu ya Waheshimiwa Mawaziri yasije yakaingia katika sanaa ya maneno, usanii katika mambo ya maneno. Mimi naomba sana na ninaheshimu sana kiti chako pia naziheshimu sana kanuni za Baraza letu, naomba sana katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wao wanasema tuwape muda. Sisi vile vile tumeshapiga sana kelele katika Baraza lako, tumeshapiga sana kelele kwenye serikali. Wakati wao unawapa muda, basi na sisi tunautayarisha umma huu. Kama ikiwa ni haki mtu kudai haki yake ni kuvunja GNU, basi katika hili mimi mara hii nasema na ivunjike. Ikiwa kudai haki ni kuhatarisha amani, basi katika hili mimi nitakuwa imamu katika kuona kwamba Wazanzibari wanadai haki na mimi nikiwa ni imamu wao. Kwa hivyo, tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla ya kuendelea, Mhe. Mjumbe umetaja kitu kizito sana kuvunja GNU. Hii ilipitishwa kwa kura za maoni na kuiondoa kwake ni kwa kura za maoni, tumefundishwa juzi. Kwa hivyo, huko usiende kwanza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa ufafanuzi wa serikali katika suala hili, mimi naamini sote tutashirikiana ili kulimaliza na kulinda haki za raia wote wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba niende katika suala jengine kwenye ofisi hii. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu niliomba maelezo juu ya vote 282100 ilioko katika ukurasa 642 sub vote 282113 ahadi ya mikataba, ambayo imetengewa 337,500,000. Niliomba maelezo kuhusiana na suala hili, lakini katika majibu ya Mhe.Waziri suala hili kabisa hakuligusia, naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, hii tumesema kwamba ni *licence payment* kwa kila mwaka, kwa wale Wayahudi, kampuni inayoitwa *ATI Company*. Wao wanafanya matengenezo na ada yao kila mwaka tunalipa ili ku-*maintain* zile *standard*, kwa vile vitambulisho na mambo mengine. Kwa hivyo hii *essential* ni *licence payment* kwa kila mwaka.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri hayathibitishwi na buku hili na maelezo yaliyokuwepo hapa. Kwa sababu kawaida *vote* zinapokuwepo kila mwaka huwa zinaonekana kila mwaka. Lakini tunaomba tufanye *replace* hapo hapo. Mwaka 2009/2010 *vote* hiyo hiyo ziro, mwaka 2010/2011, *vote* hiyo hiyo ziro, 2011/2012 na mwaka 2012/2013 vile vile kuna fedha hii. Naomba Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya kina, kwa nini tupitishe fungu hili, lina kitu gani ndani yake na huko nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, fungu hili zaidi linatia mashaka kwa sababu hata katika maelezo ya hotuba ya Mhe. Waziri katika kitabu hiki chote ukikipekua hakuna pahala popote katika maelezo ya ofisi hii tulitajiwa katika miradi au hayo malengo ya mwaka huu, kuna malipo kama hayo yakiasi kikubwa cha fedha kama hicho. Kwa hivyo nilikuwa naomba maelezo kwamba ni malipo kwa kila mwaka. Kitabu hiki hakithibitishi hivyo, kwa sababu kwa miaka mitatu mfululizo mbali ya mwaka huu hakuna matumizi ya aina hii. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tuelezwe hiki kifungu kinahusu nini Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mradi huu kwa miaka hiyo aliyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mradi huu ulikuwa kwenye miradi, sasa mwaka huu umefutwa. Kwa hivyo, malipo haya yatatokana kwenye *recurrent*. Ndio maana kwenye miaka hiyo uliyoiona huko kuna ziro ziro, ilikuwa nalipa huko, kwa hivyo mwaka huu tunalipa kwenye *recurrent* ndio inaonekana hapo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nina wasi wasi, lakini ili nisiendelee kuchukua muda wa Baraza hili, kama nilivyosema mapema kwamba mimi namuamini sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ofisi za Viongozi wa Kitaifa. Pia naiamini kamati yake vile vile, kwa hivyo moja katika malengo yetu ni kusimamia na naomba hili Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na kamati yake na kamati ya PAC kwa jumla, kwa sababu hao wote wanajukumu kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar kwa kupitia katika Baraza hili, kuchunguza matumizi ya fedha za walipa kodi, wajiridhishe sio tu kwa kwenda kupewa mkataba, lakini wajiridhishe kwa undani, kuzifuatia mpaka mwisho juu huko kuwa kweli zinafika kwa kima hiki au zinaishia mifukoni mwa watu wachache katika ofisi hii.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema naiamini kamati, naomba tuendelee, naamini kamati italifanyia kazi kwa niaba yetu. *(Makofi).*

Kifungu 0201 Utawala Unguja	1, 333,531,000
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	259,469,000
Jumla ya Fungu	**1,593,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 10 – OFISI YA RAIS IKULU

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia bajeti hii, mimi nakumbuka hata na Mhe. Omar, lakini kwa sababu nasema mimi najisemea mimi. Tulitoa hoja hapa juu ya *vote* hii ya 730000 uratibu wa fedha za

miradi, uimarishaji wa serikali za mitaa *local government reform.* Kasema kwamba mradi huu umekuwa ukijirejea kila mara na tukasema kwamba kama hatukupata maelezo ya kina hatuwezi kuidhinisha shilingi 150 milioni zilizotajwa hapo Mhe. Mwenyekiti katika sub vote hii, kwa sababu ni fedha nyingi zilikuwa zikiingizwa kila mwaka, lakini hatuoni *output* ya mradi huu wala hatuoni maendeleo ya mradi huu.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka maelezo ya kina ya Mhe. Waziri juu ya kwa nini tuziidhinishe fungu hili na mradi huu utakamilika lini ili tuone tija yake, vyenginevyo isije ikawa mradi huu kila siku tunaingiza fedha, lakini hakuna kinachotoka katika mradi huu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilieleza kwa kina kabisa mambo yale ambayo tulifanya kwa mwaka uliopita, katika ukurasa wa 43, Idara ya Waratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tulieleza kwenye ukurasa wa 44, tukatoa na malengo kwa mwaka huu. Kwa mwaka jana hasa tulikuwa tunakamilisha ile sera ya serikali za mitaa na hiyo tumetoka nayo na hiki kilikuwa kilio kikubwa sana. Waheshimiwa Wawakilishi mtakumbuka. Mageuzi mengi tunashukuru yamefanywa, kama kwenye *financial reform*, kwenye *judiciary reform,* kwenye utawala bora. Lakini bado serikali za mitaa ilikuwa haijakamilisha.

Kwa hivyo, serikali tunashukuru tumefanya kazi hiyo. Sasa hatua ilinayofuata baada ya Sera za Serikali za Mitaa, sasa tunakuja kuandaa sheria. Tutafanya semina kwa waheshimiwa mtajua hasa kwenye sera kuna lenga nini na nini muelekeo wetu na tumesema tutatizama miji yetu ikoje na mipaka yake inastahiki, Baraza la Manispaa kweli ndio lilivyo sasa hivi, wilaya zote mipaka yake ikoje. Kwa hivyo, kuna mambo mengi sana yatatizamwa. Ndio maana bado tunahisi mradi huu uendelee angalau tutizame hatua nyengine.

Kwa hivyo, *progress* ipo Mhe. Mwenyekiti, yapo yaliyofanywa, nafikiri ukisoma kwenye ukurasa wa 44 utayaona yale ambayo tuliyofanya na mapendekezo tuliyoyatoa, Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, suala la mradi huu nilitoa maelezo katika Baraza hili hili tuliloanza mwaka 2010. Mara kadhaa katika kuulizwa maswali Mhe. Waziri na mara nyengine hata maswali ambayo tulikuwa tukimuuliza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu tofauti ya serikali alikuwa akituambia kwamba kuna *package* ya *public service reform* na kuna *package* ya *local government reform*.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wakati fulani tulihoji hapa, juu ya utaratibu mzima wa uwajibikaji na hata muundo wake hizi serikali za mitaa, pamoja na siku zote kutokea kwa mfano migongano baina ya madiwani na masheha na mambo mengine kama hayo Mhe. Mwenyekiti, tukaambiwa suala hili litakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha na tuliambiwa tutaletewa sheria ambayo itatokana na mabadiliko ya sera na mpaka tutamaliza mwaka wa fedha Mhe. Mwenyekiti, hakuna suala hili. Ndio maana nikasema nataka maelezo kwamba hizi shilingi 150 milioni alizozitaka mwaka huu ni za kufanya shughuli gani katika suala la mradi huu. Huu ni mradi wa reform Mhe. Mwenyekiti, sio ule uliotajwa kwa urefu kwamba una fungu lake.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba angalau aniambie kwamba ni lini anategemea ndani ya mwaka huu wa fedha, wajumbe wa Baraza hili wakapata kuiona kwanza hiyo sera ambayo imeandaliwa kwa fedha nyingi ambazo tumeziidhinisha. Pili, aniambie suala lile la kina Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando, kuwa ni lini atatuletea mswada wa sheria ya mabadiliko ya sheria zile za serikali za mitaa ili kupata hiyo sheria mpya ambayo inaendana na maagizo. Kwa sababu *public service reform,* tumefanya na tumekamilisha tunaomba utekelezaji sasa, tunataka kuona utekelezaji kutoka serikalini. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, katika hili waziri anipe maelezo ya lini tutaletewa sera ya wawakilishi, lakini lini pia atatuletea sheria hapa ya kuzirekebisha hizo sheria zitakazopita ili tupate hizo *reform* zilizokusudiwa, naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, baada ya matamko ya sera au baada ya kutengeneza sera, hatua inayofuata sasa ndio hiyo ya sheria. Sasa tumekamilisha, nakubali, kweli tulichelewa kuikamilisha ile sera, lakini sasa nilisema kwenye hotuba yangu kwamba sera imekamilika na njia moja wapo *Alhamdulillah.* Sasa ndio tunakuja kutengeneza hizo sheria, tutakuja tusaidiane Mhe. Ismail Jussa Ladhu mwanasheria baada ya matamko ya sheria na tatafanya semina ili tuone waheshimiwa sera yetu ya serikali za mitaa inasemaje, ili matamko yale ya sera sasa tunabudi sheria, sheria zitaandikwa. Siwezi kusema nitaleta lini, kuandika sheria wewe mwenyewe unajua inachukua muda, lakini naahidi ndani ya mwaka huu wa fedha sheria tutaziandika, pengine moja au pili au tatu ambazo zitaweza kukamilisha hili suala la *reform* ya serikali za mitaa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo yake Mhe. Waziri. Naomba nimuambie kitu kimoja tu kwamba kwanza tunategemea tuione hiyo sera imefanyiwa kazi, tunategemea Waheshimiwa Wawakilishi watapata kuiona. Lakini pili nachukua *commitment* yake. Katika hili nafikiri wengine wajifunza kwamba mara nyengine tunaweza kudhani kuwa mwaka mmoja ni mwingi sana Mhe. Mwenyekiti. Mwaka jana tulipewa ahadi tunazisubiri mwaka huu hapa. Kwa hivyo, mwaka unakimbia. Mwaka jana alituahidi kwenye mwaka wa fedha, nataka nimwambie kwamba mwakani tukijaaliwa kama tutafika mwezi wa Juni kuja kupitisha bajeti hapa ikawa bado hatuna sheria ya serikali za mitaa, ikiwa moja, mbili au tatu patakuja kuwa na mbinde kweli kweli katika bajeti hii inayopita leo.

Naomba Mhe. Mwenyekiti tuendelee, haya tuliyosema tunataka kuona yanafanyika. Ahsante sana. (*Makofi).*

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	906,000,000
	Jumla ya Fungu	**906,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 17 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakumbushia tu Mhe. Mwenyekiti, tulikubaliana kwamba tuje tukutane huku. Sasa Alhamdulillah Mwenyezi Mungu katuweka hai tumekutana huku tuendelee katika ile shughuli yetu. Nataka maelezo sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe Mwenyekiti, nilijitahidi sana kumueleza, kumfahamisha, huyu ndugu yangu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mtando na zile *concept* za kilimo na utaratibu wake wa uzalishaji mbegu na mradi, sasa kama bado hajafhamu Mhe. Mtando bora atwambie hajafahamu nini, labda tumsaidie kidogo kwa sababu haya mambo mengine kutokana na ufahamu wetu mdogo atusaidie yeye sasa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anataka nimfahamishe sijafahamu nini, sijafahamu jinsi ya hizi fedha tunavyokuingizieni na mnavyozitumia. Kwa sababu sisi tunakuingizieni fedha kwa jambo kadhaa lakini matumizi yenu hayako sawa, nasema huu mradi ambao mnauendesha pale hauna tija kwetu kwa sababu tunaingiza fedha lakini hakuna faida tunayoipata, ndicho ninachosema na ndio maana nikawa nasema hakuna haja ya kuingiza fedha nyengine kwa sababu tunaingiza fedha faida haipatikani. Fedha zilizoingizwa katika mradi ule ni nyingi mno, tumeshakuja kufanya ukaguzi pale, *PAC* imekuja kufanya ukaguzi katika mradi ule na tumeona kwamba hakuna faida iliyopatikana tukaamua mradi ule ni bora usiwepo, wakasema aa tunafanya marekebisho sijuina nini, sasa leo Mhe. Waziri anakuja kuziomba fedha nyengine tuziingize tena kwenye mradi ule hebu atupe maelezo basi kwanza turidhike halafu tumuingizie hizi fedha kama hatukuridhika hatuziingizi hizi. Hayo ndio maelezo ninayoyataka Mhe. Mwenyekiti, atoe maelezo ya kujitosheleza kuhusu mradi ule.

Kwa sababu ule mradi ulipoanzishwa ulikuwa una maudhui yake haukuwekwa kwa ajili ya utafiti ule mradi. Mhe. Waziri anachupia tu huko kwenye utafiti umekuja hivi juzi, lakini mradi ulipoanzishwa ulikuwa ni mradi wa kilimo cha mbogamboga, lakini sijui kama kuna vicha hata kumi vya mchicha vilivyopatikana shilingi bilioni moja keshatumia itakuwaje, ndio shilingi bilioni moja imetumika sio milioni ni bilioni kwa sababu mia tano mia tano tuliziingiza mara mbili hatuoni kile kinachozalishwa. Sasa hebu atwambie pale nini hasa wanachokifanya kwamba kina tija kwa jamii au tunatumia pesa zetu pale. Sasa hapa anataka shilingi mia tatu nyengine tuziingize pale, ni vigumu Mhe. Mwenyekiti, kuziingiza nyengine kama zile zenyewe zimekwenda pale hatuoni tija yake inayopatikana. Hilo ndio lilikuwa langu Mhe. Mwenyekiti, kama ana maelezo Mhe. Waziri atusaidie tuweze kuziingiza hizi fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, labda nimfahamishe Mhe. Mtando kwamba mradi si wa kudumu, si wa siku zote, mradi una lengo fulani baada ya miaka miwili, mitatu,

minne, mitano na utapokamilika malengo yake basi mradi ule unaondolewa. Sasa niseme kwamba mradi huu na naomba nikariri tena nilimwambia hili la mradi wa mboga mboga sio hasa lengo lake mbogamboga kwa mamilioni haya tunauza wapi. Lakini ni utafiti wa mbegu, kuzalisha mbegu za hizo mbogamboga, nafaka pamoja hizo ndio kazi zinazofanywa Mhe. Mtando. Sasa acha twende nao nafikiri kama miaka mitano hivi tutafika mahala tutasema basi huu mradi tushafikia lengo letu au utaendeshwa kwenye *recurrent.* Lakini kwamba unasema tuuondoe na tumeshaupitisha tutafanya na *evaluation* tuta-*evaluate* malengo yake mradi umefikia vipi basi tutaamua. Narudia tena tumezalisha mbegu, kama vile mbegu za mtama, mahindi, *NERICA* na tumezitawanya na kuwapa wakulima na hizo ndio faida zenyewe, sasa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa hazioni hizi. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naziona kama maneno yake anayoyasema. Lakini nataka nimuulize ile dhana ya kuanzisha ule mradi hasa, maudhii ni nini? Kufanya utafiti au ni shamba la mboga mboga, ambalo litakuwa likizalisha na kufanya iwe ni biashara. Kwa hivyo, naomba anisaidie hili, kwani pale kuna ubia baina ya Misri na Serikali ya Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, lile ni jina tu la Mradi wa Mboga Mboga na wala hakuna mradi huu hasa. Kwa hivyo, hayo niliyomwambia ndio madhumuni ya shamba lile. *(Makofi)*
Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, vitu hivi wakati mwengine uone kwa macho kidogo, basi mimi naomba kesho au siku yoyote atapopanga yeye au wakati huu wa *session* hivi sasa, tufanye *field visit* na nimvalishe *rain boot*, kwa sababu kule kuna tope na dogo jekundu kama jimboni kwake, twende kidogo na ashuhudie kile kinachofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kumejengwa *dam* la maji kwa ajili ya kuzalisha kubwa sana na wala sijalione sehemu nyengine na fedha nyingi sana ambazo zimetumika, kuna mitandao ya umwagiliaji, hiyo *investment* anayosema ni kweli tena ni kubwa mno.

Kwa hivyo, sasa namualika yeye pamoja na kamati twende kutatembele na kuona yeye mwenyewe *on the spot* na matunda yanayozalishwa kule kama vile mabilingani, yaani wale Wamisri wamezoea kuchezea jua, yaani wamebadilika rangi hasa baada ya ule weupe wamekuwa weusi kwa jinsi wanavyojituma na watu wetu sio wao tu.

Sasa faida ndio hizo, labda hili jina ndio lina-*mislead* kidogo, lakini nimeshaeleza kwamba utafiti na uzalishaji mbegu pamoja na huo ni *model farm* na tunashirikiana na wenzetu hawa wa Misri.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Waziri bado hajanifahamu, kwa sababu sisi tulishafanya ziara pale Kamati yako ya Baraza ya *PAC* Mhe. Mwenyekiti, palikuwa na *quire* ya Mdhibiti pale juu ya matumizi ya zile fedha maana zimeonekana fedha nyingi zimetumika kuliko kilichozalishwa, yaani *value for money* haipo, Mhe. Mwenyekiti bilioni 1 tumeuliza kimezalishwa kitu gani hakifiki hata shilingi 300,000 hazijazalishwa na wala sikwambii shilingi milioni 3/=. *(Makofi)*

Lakini bado tunaendelea tena kuingiza fedha kwa ajili ya mradi na wala mradi ule si kwa lengo ambalo analolisema Mhe. Waziri na sisi tumeona mpaka hiyo mikataba ni Shamba la Pamoja la Mboga Mboga baina ya Serikali ya Misri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambao utakuwa unasimamiwa na JKU.

Mhe. Mwenyekiti, huko mwanzo ilikuwa sijui uende Wizara ya Kilimo, labda walipiga mateke na kupewa JKU. Sasa JKU wao umekuwa kama watizamaji tu na imekuwa kama yule Msiri ndiye mwenye shamba, pale kuna *quire* ya Mdhibiti na bado haijajibika mpaka leo, maana wameshindwa kutoa maelezo katika hili. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba mradi huu hakuna haja ya kuupelekea tena fedha, kwa sababu hatuoni ile *impact* ya ule mradi, itakuwa tunaingiza fedha tu na wala hakuna kinachozalishwa. *(Makofi)*

Kwa kweli dhana iliyokusudiwa pale sivyo anavyosema Mhe. Waziri na imekuja kubadilika hivi sasa baada ya kuona hakuzalishwi kitu na watu wa kilimo wanafanyia utafiti, kwa sababu lile shamba halina kazi, lakini fedha ni nyingi ambazo tunazoziingiza pale na wala faida yake haionekani.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiria katika hili sijapata maelezo ya kutosha, kwa hili namuomba Mhe. Waziri atusaidie kidogo, hii kusema kwamba twende pamoja na mambo mengine, kwani sisi tayari tumeshakwenda kama kamati na wala sina haja ya kwenda na Mhe. Waziri kwa kesho.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yako ya Baraza imekwenda pale na kuona yale madudu na tukakubaliana kwamba hapa hakuna haja ya kuingiza fedha tena, kwa sababu huu mradi hautunufaishi. Kwa hivyo, ni vyema tufute ule mkataba na wale wa Misri na kila kitu na badala yake wabakie JKU, kwani wanaweza kuliendesha na kufanya wanavyotaka na kuliko kuendelea kwamba tunafunga mikataba na wale watu na wala hakuna faida inayopatikana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri atakuwa amenielewa vizuri kidogo lile ninalolikusudia.

Mhe. Mwenyekiti: Kama ni mradi na umetengewa fedha, hebu tuzungumze zaidi kwenye hizo fedha za mradi na hilo ni moja. Lakini pili huwa naogopa sana kwamba Baraza hili lifute mikataba, kwa sababu mikataba ina conciquincies zake. Kwa mfano, unaweza kufuta mkataba na ukajikuta sasa wewe ndiye unaepata hasara, inapokuja *issue* ya kupelekwa mahakamani hatimaye unajikuta wewe ndiye unaepata hasara.

Lakini kwa kifupi niseme kwamba kwa kuwa ni mradi tunaouzungumzia, basi hebu tuone huko kwenye fedha za miradi nadhani umetengewa fedha huu na ndio tunazodadisi, kwamba fedha hizo zinazoingizwa kwenye mradi ule hazizalishi kile kitu kinachotegemewa kizalishwe.

Kwa maana hiyo, hii fedha ya uendeshaji wa hapa tumalize na tungojee kasma ya miradi ambayo iko kwenye ukurasa wa 700, tuone je fedha hizo zinafaa, nyingi, hazitoshi au namna gani, lakini hapa kwenye uendeshaji wa ofisi nadhani tuishie hapo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa busara zako tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, ili kuokoa muda pamoja na kuepuka kumsimamisha kila mara Mhe. Waziri, kuna hoja moja niliitoa na muomba hii akinijibu kwa hapa iwe imehusu vikosi vyote vitano. Kwa kweli nilihoji juu ya suala ya bajeti ilioko kwenye *vote* 211200 *sub vote* 211204 ambayo hii inajirejea kila pahala katika vikosi vyote kuhusu huduma za chakula cha askari.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kimsingi sina tatizo la kuongezwa bajeti, ili askari wetu wale vizuri, wawe na utulivu na wafanyekazi ya kutulinda vizuri na wala sina tatizo na hili. Lakini nilihoji kile kima cha uongezekaji. Kwa mfano, Kikosi cha Mafunzo naelewa kwa sababu Mhe. Waziri alituambia wanakusudia kuongeza milo wa watatu kwa wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo pamoja na askari wao.

Lakini sasa niliomba maelezo kwa jumla Mhe. Mwenyekiti na naomba kama nilivyosema anisaidie kwa yote kwa pamoja, kwamba fedha hii kwa mfano JKU tulipozungumza imetoka shilingi 38,000,000/= mwaka jana hadi 380,000,000/= na hilo ni ongezeko la asilimia 1,000/=.

Kwa hivyo, naomba Mhe. waziri anisaidie kwamba huko nyuma hiki chakula kinatolewa vipi na hivi sasa kinategemewa kutolewa vipi, ili ku-*justify* ongezeko hili na nikiridhika na hilo sina tatizo nitaruhusu bajeti hii iende. Mhe. Mwenyekiti, naomba anipatie maelezo kama nilivyosema si hichi tu, isipokuwa ni kwa vikosi vyote, ili nisimsimamishe kila kwenye kikosi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kutaka kufahamu zaidi juu ya hili ongezeko. Kwa kweli tulikuwa na matatizo ya askari wetu kwanza wakiwa mafunzoni na wala hawapati chakula na wanajigharamia chakula na sasa tumeliondoa hili. Kwa hivyo, wakiwa mafunzoni wakati wowote serikali au vikosi vyao vitawahudumia vyakula na hili namba moja, ndio maana utaona kuna ongezeko la aina hiyo. *(Makofi)*

Pili tumesema maaskari wote ambao wako kambini wakati wote sasa watawajibikiwa kula kambini. Sasa tunategemea variation kwenye kikosi ukubwa wake, ndipo utakapoona tofauti kwamba nyengine ni mkubwa sana na nyengine ni ndogo. Lakini hivi sasa serikali imeamua kidogo kwa hili tujipinde, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, lakini maaskari wetu wale vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo fasaha, naomba anihakikishie suala moja tu na halafu nikae tuendelee. Kwa mujibu wa maelezo hayo aliyonipa Mhe. Waziri anakusudia kuniambia kwamba

yale makato waliyokuwa wakikatwa askari, kuanzia sasa yatakuwa si halali katika masuala mazima yanayohusu posho ya chakula wakati wanapokwenda mafunzoni na sasa yawakuwa hayapo tena, basi atoe kauli, ili askari wake wasikie na baada ya hapo naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, nafikiri kuanzia sasa nasisitiza tena na makamanda wananisikia, kwamba maskari wote wasikatwe kwa chakula.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nawaona wenyewe makamanda wamepiga *salute*. Tunaendelea *(Makofi)*

Kifungu …	Utawala Unguja	7,504,000,000/=
	Jumla ya Fungu	**7,504,000,000/=**

FUNGU 18 – CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 – Idara ya Vyuo vya Mafunzo

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia katika sehemu hii ya Chuo cha Mafunzo, nilizungumzia sana kuhusu ukiukwaji wa Haki za Binadamu unaofanywa pale chuoni, jinsi ya watu wanavyopekuliwa wakiwa uchi wa mnyama pamoja na kutumia mtondoo badala ya kuwekewa vyoo na wala majibu ya Mhe. Waziri sikuridhika nayo.

Kwa hivyo, nataka aniambie ni lini ndani ya magereza yetu mtajengwa vyoo na lini watu watapekuliwa wakiwa faragha badala ya kupekuliwa wakiwa nje. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, majibu, nilijua mtondoo lazima utatoka pale. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kutukumbusha hili nafikiri nilieleza kwamba tumeanza, tena nakumbuka mwenyewe nilikwenda Kangagani na kufanya mpango kule tukarekebisha na mambo ni mazuri nafikiri hata Tungamaa tumerekebisha.

Kwa hivyo, mote humo lengo letu ni kurekebisha, lakini kidogo urekebishaji mwengine kama vile Wete una matatizo kwa sababu ya ile hali ilivyo, lakini tumeshaanza kidogo na sivyo ilivyokuwa zamani na hili ni hichi Chuo kipya tutajitahidi na hilo kabisa halitakuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako kwa jumla, kwa kweli tunapata *credit* kwa mabadiliko, yaani SMZ inapata *credit* kwa mabadiliko ya Haki za Binadamu katika Chuo cha Mafunzo, tulivyokuwa nyuma sio tulivyo leo hali imebadilika sana na ile *experience* aliyokuwa nayo wakati ule hivi sasa haipo tena. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, suala la matatizo yalioko Chuo cha Mafunzo hatukuanza kulisema leo, nimelisema mimi binafsi katika Mabaraza kadhaa liyoyopita nyuma. Kimsingi sisi tumeapa hapa kwamba tutaitii Katiba ya Zanzibar.

Kwa kweli inasikitisha sana ibara ya 5 ya Katiba yetu juu ya Haki ya Faragha inaendelea. Mhe. Mwenyekiti, leo ananiambia Mhe. Waziri amejibu kwamba tutajenga, matendo Mhe. Mwenyekiti nayakidhi haja maridhawa kuliko neno.

Kwa hivyo, aniambie ni lini sasa magereza yote yatakuwa yameshawekwa vyoo ndani na watu wakatumia vyoo badala ya mtondoo, aniambie ni lini kusudi tuweze kujua na kuweza kufuatilia, sio kuniambia kwamba tuko mbioni au tumeshaanza na wala Pemba hakujaanza hata sehemu moja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, itakuwa ni vigumu kwa bajeti hii kubadilisha kwa mpigo mote. Lakini nachukua ahadi Mhe. Mjumbe kama nilivyosema kwamba

nimekwenda mwenyewe Kangagani na kushuhudia mwenyewe na kutoa fedha mwenyewe na kubadilishwa, Afisa Mdhamini nikamuagiza na hali nzuri. Kwa hiyo, tumeanza naomba kutumia lile neno langu kwamba tuamini. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo ambalo linalohitaji gharama na lile ambalo halihitaji gharama. Kwa kweli suala la ujenzi wa vyoo linahitaji gharama, lakini suala la kumpekuwa mahabusu au mfungwa kumpekuwa halihitaji gharama ni kutamka tu Mhe. Waziri wakati makamanda wapo pale. Kwa mfano, kuanzia leo hakikisheni wakija watu mnawapekuwa wakiwa faragha na hili alitamke humu, kwa sababu watu wanapekuliwa wakiwa wazi kabisa, yaani sehemu ambazo hapana stara.

Kwa hivyo, leo atamke Mhe. Waziri hapa awaagize makamanda wake kwamba wasimamie suala hili, kwa sababu makamanda wake wanakiuka Haki za Binadamu wa wanavunja Katiba ya Zanzibar kifungu cha ibara ya 5.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, tumesikia *concern* ya Mhe. Saleh Nassor Juma na tutalirekebisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, sijamfahamu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba tunamshukuru kwa *concern* yake na ninasema tumesikia na tutalirekebisha, yaani hiyo hali tutairekebisha kwamba isitokee tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, watarekebisha wasirejee tena.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani lugha nzuri ya kutumia, kwa sababu sisi tukipitisha fungu hili itakuwa tunatumia fedha za walipakodi kwa ajili ya kwenda kunyanyaswa au kuvunjiwa heshima pale.

Sasa nadhani Mhe. Waziri angesema kwamba kuanzia leo naagiza kwamba wakija mahabusu au wanafunzi wapekuliwe faragha, ili kila Mzanzibari afahamu hilo, lakini tumefahamu tunajirekebisha katika jambo gani Mhe. Mwenyekiti na wala tusiwavunge wananchi.

Kwa maana hiyo, nafikiri tuwe *very clear*, kwamba kuanzia sasa atakapokuja mahabusu au mwanafunzi apekuliwe faragha lugha hii hata yule mkulima wa Vitongoji kijijini kwangu Mhe. Mwenyekiti atafahamu hata Watumbatu wenzangu kule Nungwi watafahamu. Nadhani ingekuwa vizuri kwa ajili ya kuepusha kuwapiga wananchi kwa bakora yao, yaani kuidhinisha fedha za walipakodi kwenda kuwanyanyasa kule, nadhani awe *very clear* kwa hili ili tusipoteze muda katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Saleh Nassor Juma nakubali kwamba tutajitahidi kuanzia sasa wanafunzi wanaokuja au mahabusu watatekuliwa na hii kupekuliwa hatuwezi kuepuka, isipokuwa watapekuliwa kwa faragha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nimemuona ametikisa kichwa kwa kukubali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia sehemu hii ya Chuo cha Mafunzo nilisema kwamba kuna malimbikizo ya hawa askari wetu wanaowasimamia hawa wanafunzi kuwa wanapokwenda likizo hawapati malipo yao.

Vile vile kuna fedha za hali ngumu wanapewa shilingi 1,500/= na nililalamika kwamba shilingi 1,500/= hatuwatendei haki na wala haiwezi kuwasaidia, tena nilisema kwa kelele kubwa, lakini Mhe. Waziri hakunijibu suala hilo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti anipe maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Subeit Khamis Faki alichangia suala hilo. Kwa hivyo, naomba kumhakikishia tu, kwamba fedha za likizo zinatolewa kwa

mpango maalum, yaani ni flat rate, yaani ni mpango maalum kwa kila anayekwenda likizo ukifika wakati wake kwa mwaka ule anapewa.

Vile vile alizungumzia kuhusu usafari na hilo tutajitahidi kweli, lakini wale ambao wanaokwenda baadaye wanarudishiwa gharama zao na kama hawajarudishiwa, basi tutalisimamia ili tuone linakaa sawa kwa lengo la kuepusha usumbufu kwa maaskari wetu. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, unajua Mhe. Waziri ni mzuri sana maneno yake kwa kujibu na wala hana utata wa kujibu, lakini utekelezaji wake unakuwa mgumu. Mhe. Mwenyekiti, muda umeshakuwa mkubwa tuendelee na mimi namuamini, lakini kwa kweli akitujibu basi utekelezaji uende, kwa sababu hichi ni chombo kizito kwani humu tunawatetea wananchi na wanatusikiliza tukisema. *(Makofi)*

Kwa hivyo, yale wanayoyaahidi viongozi wetu Mawaziri, kwa sababu ndio watendaji wa serikali hii, basi waangalie kuyatekeleza na tusije kusema hapa na kuonekana kama tunakuja kuimba na kuondoka. Mhe. Mwenyekiti, ahsante na tuendelee.

Kifungu 0201 –	Idara ya Vyuo vya Mafunzo	5,890,000,000/=	
	Jumla ya Kifungu		**5,890,000,000/=**

FUNGU 29 – KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201	–	Utawala	9,650,000,000/=	
		Jumla ya Kifungu		**9,650,000,000/=**

FUNGU 32 – KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu 0201 – Utawala Unguja

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nilimuuliza swali dogo tu Mhe. Waziri na bado sijapata ufafanuzi. Swali lilikuwa kwa nini hichi Kikosi cha Zimamoto na Uokozi majukumu yake makubwa, lakini bajeti yake ni ndogo na ndio maana ikatokezea mashaka makubwa katika kuzima moto. Kwa hivyo atupe kigezo gani wanachotumia kwa ajili ya kutoa bajeti hii kwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ungeona hayo mahitaji ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi waliyoyataka, ili waende kisasa basi labda ni mara tatu ya bajeti hii, lakini ndio *ceiling* tuliyopata.

Lakini nilieleza kwamba kwa vifaa walivyonavyo wanajitahidi na tunazidi kukiendeleza kile Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, tatizo ni njia na ile mipango ya miji ilivyojengwa wanapata tabu zaidi kufika, kwa upande wa vifaa wanajitahidi tena wanao mtazamo wa mbele kila mara, lakini *ceiling* tuliyoipata kwa kikosi ni ndogo. Sasa tuendeleze mapato yetu na tusaidie na kikosi chetu na tutajitahidi. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inaingia kwenye mabadiliko makubwa kama nilivyosema mwanzo tunacho Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa, tunazo hoteli nyingi na tunakaribisha wawekezaji na *pattern* iliopo haikuanza leo. Kwa mfano, ukirudia bajeti za miaka mingi kikosi hichi ndicho kinachopewa bajeti ndogo kuliko vikosi vyote. Sasa Mhe. Waziri ni nani mwenye kuweka ceiling hii hata ikawa wewe anakubana? *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kaka yangu Mhe. Rashid Seif Suleiman ameuliza swali zuri sana, kwamba nani anayeweka *ceiling*. Kwa kweli ni uwezo wa serikali, uwezo wa serikali unapokuwa mzuri na hali yetu kwa kila taasisi utakuwa mzuri. *(Makofi)*

Hata hivyo, akiangalia mwaka jana bajeti ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na mwaka huu ambao tunataka kuanza hivi sasa ni tofauti kidogo, yaani tumeongeza kidogo, hivyo lazima tu-*appreciate* kidogo, kwamba kila hali inapokuwa nzuri, basi taasisi zetu zote zitakuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti: Tukizingatia kwamba hatuna uwezo wa kuongeza fungu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, akumbuke kwamba kila kitu kimeongezeka na wala hakikuongezeka hichi tu. Lakini namuomba Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika bajeti ijayo ajue kwamba kupanga ni kuchagua, kwamba Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni kikosi muhimu bila ya hivyo nchi yetu itaingia kwenye mashaka ambayo tunayakusudia. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, moja katika mchango wangu kuhusu masuala ya vikosi nilizungumzia suala zima la utaratibu wa kutangazwa *tender* katika shughuli zao ambazo hazipo hizi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anieleze *immolation* ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, kwa sababu kama nilivyochangia kwamba kumekuwa na manunuzi pale kwa mfano ya magari yale ambayo watu wengi wanalalamika kwamba yako chini ya viwango na ndio maana yameshindwa kazi, askari wenyewe wamekuwa na malalamiko hata Kamati ya Mhe. Hamza Hassan Juma walipokwenda pale waliondoshwa na kupelekwa *Airport* ili wasiyaone kutoka pale Kilimani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachotaka kuuliza Mhe. Waziri katika hili vikosi hivi vinafuata taratibu za *tender* kama zilivyo idara nyengine za SMZ na kwa sababu Sheria ile ya *Procument* inawafunga wote, ana kauli gani kuhusiana na vikosi hivi? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kweli suala hili lilikuja mpaka serikalini na tukalifanyia kazi na tulichokifahamu kabla ukweli ilikuwa zile *Tendering Committee* zilikuwa hazijafanywa, lakini baadaye zikaundwa na sasa utaratibu wote utafuatwa na wala hakuna pingamizi na ushauri wake Mhe. Ismail Jussa Ladhu tumeusikia.

Lakini hilo suala limepita kwenye mchakato mzima wa *Tendering Committee* ya ndani ya Kikosi, kwa sababu kuna utaratibu wao kila kikosi wanayo *Tendering Committee*, kwa hiyo walifanya ule utaratibu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, hoja ni kwamba fedha nyingi zimeingizwa katika mradi ule zaidi ya bilioni moja. Sasa zishazoingizwa ziache ziingizwe zilizokwishakwenda ziache ziendelee kwenda, lakini kuingiza fedha nyengine zaidi pale ni tatizo. Kwa sababu mradi ule kwa mujibu wa maelezo tuliyoyapata kwanza haukufanyiwa *feasibility study* waliibuka tu watu wakazua wazo mradi ukafanyiwa kazi, na JKU wao walikabidhiwa tu kwamba endesheni ule mradi hasa ni wizara lakini walikabidhiwa JKU waendeshe tu. Kwa hivyo, wao kwa kweli hawajui chochote licha ya kusimamia.

Sasa kwa kuwa haukufanyiwa *feasibility study* ndio maana sasa tukatoka kwenye uzalishaji wa mbogamboga kama lengo la asili lilivyokuwa sasa kumekuja hii *concept* kwamba ni kituo cha utafiti wa mbegu, kitu ambacho hata na Kamati yangu tulipokwenda hicho ki- *plot* cha *NERICA* tulichooneshwa, mtoto mdogo tu akisema kwamba akitie maji basi chote kinarowa kwa sababu ni ki- plot kidogo sana. Hata mkataba wake kwa kweli una matatizo kwa sababu hakulinda *interest* ya serikali. Ndio maana fedha ndogo iliyopatikana kama laki, 7 yule Mmisri aliyekuwepo kaanza kutumia fedha zile wala JKU wao wapo wanaangalia macho tu.

Ndio tukasema katika mazingira kama hayo serikali kui-nject tena fedha nyengine, ndio tukasema pale ni tatizo kwa vyovyote vile. Kama ikiwa tumefika pahala tumeona kama tatizo, basi ni vyema serikali irudi ifanye tathmini ya kina ili baadae tuangalie tunakwenda katika hatia gani. Kulikoni kuwa tumeshafeli halafu tukaingiza fedha zaidi na tukaendelea kufeli. Sisi kama Wawakilishi wa wananchi hatuwezi kukubaliana na hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi |Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, napenda sana niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya PAC. Inaonekana wazi wamefanya kazi nzuri ya kufanya tathmini ili weweze kuona jambo jema na zuri kwa nchi yetu. Kwa kuwa wameanza vizuri na nia yetu siku zote sio kuharibu fedha ya serikali, nia yetu ni kutengeneza. Naomba Waheshimiwa Wajumbe wazidi kutupa nafasi ili tulifanyie kazi jamo hili. Maana ni

kweli panahitaji kufanyiwa tathmini kuoma umuhimu wa mradi hii tunakwenda nao vipi kwa sasa. Ili fedha zetu za umma zitumike vizuri na zitumike kwa maendeleo ya nchi yetu.

Sasa hivi tuna umuhimu wa kweli kweli wa kukuza kilimo chetu. Eneo lile kufanywa kituo cha kuzalisha mbegu bora nisehemu ya kukuza kilimo nchini. Kwa hivyo ni muhimu tukafanya tathimini na pale penye mapungufu Mhe. Mwenyekiti, tukapaondoa ili manung'uniko ya Waheshimiwa Wajumbe yakaondoka na mradi ule ufanyika vizuri kwa maslahi ya kukuza nchini na kwa maslahi ya watu wetu.

Kwa hivyo nawaomba tuupokee ushauri wa wenzetu huu ili tulifanyie kazi vizuri jambo hili, lilete tija na manufaa kwetu sote. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kama nimemfahamu vizuri Mhe. Waziri kwamba tutoe mda, wajipange, wafanyeutafiti na mambo mengine. Sasa mimi nilikuwa nina wazo Mhe. Mwenyekiti, kwanza nahisi 300 tuzizuie, tusiziingize kwanza. Ili waendelee na utafiti wao na mambo yao, mwakani Ishallah wakishakuonja mambo yamekuwa mazuri waje waziombe tena tuwaingilizie wakishakutupa utaratibu mzuri, tutawaingilizia wakishakutupa tu utaratibu mzuri, tutawaingizia mwakani lakini, tutawapa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tumeshajaribu zaidi na milioni moja zimeshakwenda, pesa za walipa kodi, hakuna kinachozalishwa, tukaidhinishe na nyengine. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii itakuwa ngumu. Waache wakafanye utafiti sisi tunawasubiria, lakini hizi tuzizuie kwanza, zisiingiwe tena pale zikenda zikaungua. Wacha wakafanye utafiti, wafanye na mambo mengine, takapokuja mwakani watakuja na utaratibu mzuri, ikiwa tumeridhika tutawaingizia hata zaidi ya 300 wala hakuna tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mtando afahamu kwamba hapa kuna mchango wa serikali, milioni 150 halafu kuna *grand* ya hao Wamisri aliowasema kwa milioni 150. Jumla ndio zimeangukia milioni 300. Sasa ina maana tunachia sisi na mwenyetu anachangia. Ina maana tukiuwacha mwaka huu tutazikosa hizi. Kuonyesha ule mzito wa mradi wenyewe na huyu mwenzetu katika huu mradi na yeye anachangia hichi kiapa kimewekwa *foreign grand* 150 milioni.

Mimi ningeshauri sana na kumuomba Mhe. Mtando na Mhe. Omar Ali Shehe wa (PAC). Unajua kuna tofauti kati ya miradi ya kilimo, nilieleza sana wakati ule. Miradi ya kilimo tija zake huzioni hapo hapo. Mradi wa kilimo kuzalisha mbegu ndio tija moja wapo hiyo. Kufanya utafiti matokeo yake ndio unapata, tunampa mwengine. Tumezalisha mbebu ya NERICA haipawahi kuzakushwa mbegu hiyo. Wee Bambi kuzalishwa mpunga umesikia lini. Bambi haujazalishwapo mpunga. Imekwenda kuzalishwa mbegu ya NERICA. Sasa hiyo ndio tija yenyewe hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Shida ninayoipata ni moja tu, unapokuja kwenye suala la utafiti, basi tija yake huioni ile *in put* na *out put* ukalinganisha ukasema faida ni hii, si rahisi. Lakini unapokuja kama ni mradi kama vile mfano wa biashara ndio sasa unaweza kulinganisha tumeingia hichi, tumetoa hichi kwa hivyo mradi huu umeleta faida au laa. Sasa Waziri anasema hapa kinachofanywa ni pamoja na suala la utafiti, ambao tathmini yake inakuwa ni ngumu kidogo.

Maana ukienda kwa mfano Kizimbani pale, utafiti wa muda mrefu si rahisi kutathmini kifedha lakini utafiti unaendelea tangu kituo kile kianzishwe. Sasa Waheshimiwa Wajumbe hapa tuangalie maeneo yote mawili ili tufikie uwamuzi wa fungu hili, tunafanyaje, maana yake nini?

Tunazungumzia kwamba tunafunga kabisa jambo lile. Maana kama hatukutia mchango wetu maana yake haya yule *grand* yake anaweza asilete, makubaliano yakoje. Labda Waziri ungetusaidia maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, juu ya maelezo mazuri uliyotueleza lakini pia kuna suala la mahusiano ya nchi na nchi. Wenzetu Waigipt walikubali kwa nia njema na tukafanya nao mkataba. Sasa vile vile tunapovunje tu bila ya kufanya tathmini hiyo ya undani pia nayo inaweza kutugharimu kwa njia nyengine. Kama ulivyoeleza matokeo ya faida ya utafiti huwezi kuyaona hapo kwa hapo.

Kwa hivyo hapa tunayo mambo matatu yaliyokuwepo mbele yetu.

1. Faida ya Utafiti.

2. Mahusiano ya nchi na nchi.

3. Mkataba ambao tayari tumekubaliana nao.

Kwa hivyo ni vizuri Waheshimiwa wakatupa fursa yote haya tuyatizame, tutakapoondoa sasa hivi tutakuwa tumejirudisha nyuma kwenye jambo hili. Naamini tutakapokuja mwakani tutakuja vizuri na maelezo ya kina na yale yote yaliyokuwa na mapungufu tutakuwa tumeyasawazisha Mhe. Mwenyekiti, ili tuwe na mradi mzuri, mradi endelevu unaosaidia nchi yetu kwa manufaa yetu sote. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, lakini nataka nikwambie huu mradi Mhe. Mwenyekiti, kwanza sio wa leo, haukuanza mwaka huu. Huu mradi ni wa siku nyingi na si mradi wa utafiti, haukuanza na utafiti, hata ukisoma kwenye hichi kitabu chenyewe kinakwambia humu kwamba "kilimo cha mboga mboga" si utafiti, kama ni utafiti ungepelekwa Wizara ya Kilimo. Huku lilikuwa ni shamba la kilimo cha mboga mboga, baina ya serikali ya Misri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
Mhe. Mwenyekiti, hakuna tija pale katika mradi ule, tumeshakwenda tumeona, mimi nitashangaa sana kama Waheshimiwa Mawaziri watakuwa wanang'ang'ania katika hichi kwamba tukaingize fedha nyengine za walipa kodi, ni kitu cha ajabu sana kitakuwa, badala ya kukaa tukaangalia faida tunayoipata au hasara tukasema huku kuna hasara. Anasema aah mahusiano na mwenzetu, hivi hata kama tunakula hasara?

Mhe. Mwenyekiti, ili tusivunje mahusiano na mwenzetu, yeye yuko tayari kula hasara, mbona yeye anachukua kinachopatikana pale, hatupati sisi. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti mimi sikubaliani nalo, hatuwezi kuingiza hizi, wacha na hizo zake asilete tukakae tena upya, ndio mambo yanavyokwenda. Kama tumefika pahala hatupati kitu tukae, pamoja tuanze kutizama tatizo ni nini. Lakini sio tunaendelea kutumia tena aaa, tukae kwanza tukajiulize, mwakani tukija, tutakuja tumeshafanya utafiti wetu, tumeshafanya nini, tutakuja tutakaa pamoja tutaanze tena huo mradi. Kama ni wa utafiti kama wa nini.

Mhe. Mwenyekiti: Maana yake tupige kura, ndio maana yake. Tukipiga kura tupige kura kwa milioni 150.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia. Kuna masuala unaweza kusema Juma Duni vua kofia nitavua. Kuna masuala ya kitaalamu huwezi kusema tu hicho funga. Huu mradi ulipoanza kuna investment serikali imeshatoa ya bilioni 1. Sasa huwezi kusema kesho funga, nao vile vile ni hasara. Ushauri uliotolewa ukafanyiwe tathmini, utakapofanyiwa tathmini kama hauna maana ndio utafungwa lakini utajulika *what is next* na hivyo ndivyo miradi yote ya kitaalamu ndivyo inavyofanywa.

Mimi nakubaliana na wajumbe kabisa kwamba wanaona faida hakuna. Lakini faida hakuna si kwa kusema. Faidha hakuna kwa kwenda kufanya tathmini ya kitaalamu ndio miradi inavyofanywa, haifungwi tu kama vile ni shikamoo, marahabaa. Kwa hivyo tunachowaomba Waheshimiwa *reservation* zao ni sahihi. Mhe. Waziri wa Nchi anasema tupeni nafasi tuufanyie tathmini na hata mkiona mwenzetu kakubaki kuna milioni 150 basi si ajabu kuna kitu cha faida. Hilo moja Mheshimiwa.

Lakini pa pili moja tunacholaumiwa sote Waafrika kwamba tunafanya mambo bila ya kuwa na *research*. Sasa kama hapa panafanywa *research* huwezi kukategemea kesho upate matokeo, matokeo yanaweza kuonekana miaka 5 au miaka 10 ijayo. Hizo unazosikia *research* za mbegu zinazopandwa sasa, research imefanywa zamani. Kwa ufupi ninachowaomba waheshimiwa waiwachie Serikali ikafanye tathmini kitaalamu halafu liletwe jibu kama ule mradi umeonekana *not feasible* au viable pia hayo ni mambo ya msingi ya kufanya.
Mhe. Mwneyekiti, huwezi tu ukasema tukate pesa ikisha iwe kila kitu kimekwama, tuachieni serikali tukalishughulikie. Mheshimiwa huo ndio ushauri wangu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, bado narudia tena kusema kwamba mradi huu ni wa pande mbili na pande zote mbili zilifungwa na makataba. Mkataba unasema huu ni mradi wa kilimo cha mboga mboga na hata Wamisri wao wanatambua hivyo kwamba ule ni mradi wa kilimo cha mboga mboga.

Mhe. Mwenyekiti, tulifika pahala kama Kamati tukajiuliza huu mradi umekusudiwa Wamisri kuwasaidia Wazanzibari au Wamisri walikuwa wanatafuta shamba walime ili wapate vitu vya kupeleka kwao. Tulikuwa tunajiuliza tatizo ni lipi, tukafika pahala tukaona kwamba inaonekana Wamisri walikuwa wanatafuta shamba la kuja kulima, wakachukua fedha wakapeleka nyumbani kwao. Hivyo ndivyo inavyoonekana kwamba sasa hivi kile

kidogo kilichoonekana kwamba tayari sasa hivi wameanza kuvuna na kupeleka nyumbani na Wazanzibari tukaendelea kukodoa macho.

Tukizuruhusu hizi tutakuwa tayari tumetia pale zaidi ya bilioni 1.3 na mradi sio wa leo, mradi una zaidi ya miaka 7 sasa hivi. Kama ni kupata maana yake ni tayari tungekwisha pata. Sasa bado narudia kwamba Mhe. Mwenyekiti, inaonekana mradi umefeli kwa lengo lake la msingi. Na limefeli kwa kuwa mradi haukufanyiwa *phisibility study*, walikurupuka tu watu matokeo yake sasa hivi tunatoka kwenye mboga mboga tunaingia kwenye utafiti. Lakini ni utafiti gani, Zanzibar tunayo taasisi inayofanyiwa utafiti na sio JKU.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nishauri kwamba tuwape mda serikali. Kwanza hizi zilizopo tuzizui na tumkabidhi pale somo yangu azuie Waziri wa Fedha, serikali ifanye *phisibility study*, iyangalie wapi tumejikwaa, tukifika pahala tukiona sasa ni sawa kufanya basi tufanye, fedha zitakuwa zipo zimetulia hazina tatizo lolote. Lakini kwa sababu Baraza hili lisiinginishe fedha hiyo kwa ajili ya watu kwenda kuvuruga Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, tuna mambo mawili hapa nadhani Waheshimiwa Wajumbe tutakubaliana na mimi kwa upande wetu serikali tunapata kuyaangalia. Kwanza kuangalia mkataba kama tunahitaji kuendelea na mradi au hatuhitaji kuendelea na mradi. Hawa kwa kuzingatia kwamba mikataba yote yote ambayo tutakayosaini serikali na wenzetu wowote wale iwe na tija na nchi yetu. Kwa hivyo hili la kwanza nadhani tutamuomba Mwanaria Mkuu basi tuliangalie kwa pamoja kwa upande wetu wa serikali. Kwa sababu mikataba yoyote kisheria mnaweza ukai- *review* haikufungini maisha iwe ndio vile vile, mnaweza ukai-*review* kwa makubaliano. Hilo la kwanza.

La pili tufanye kazi moja nzuri basi mimi nakubaliana na wazo la somo yangu hapa Mhe. Omar Ali Shehe, sisi kwa upande wetu wa serikali tutafute vijana wataalamu walifanyie tathmini ule mradi mzima, tupate ripoti ya kitaalamu kwamba mradi unaweza kuendelea na tija ukaleta tija au mradi kuendelea kwake hautoleta tija. Wakati huo tunafanya tathmini kwa nguvu nilizonazo, lakini sitaweza kuzizuia hizi pesa kama nyinyi hamjazipitisha Baraza. Baraza lazima zipitishwe hizi pesa halafu mimi nazizuia sitozitoa kwanza mpaka tathimini ikamilike.

Imani yangu kwamba tathmini inaweza ikachukua miezi miwili mitatu , tukapata ripoti ya tathmini halafu tukaendelea. Lakini tunazuia nini? Tunazuia ule mchango wa serikali ambao wa milioni 150 ile *grand* hatutoweza kuizuia. Kwa hiyo kama kufanya kazi ile grand inaweza ikaanza kufanya kazi halafu *the next six moths* ile ya serikali inaweza ikaingia baada ya kuweza kupata hiyo ripoti ya tathmini. Ripoti ikituelekeza kwamba mradi hauna manufaa basi serikali itafanya maamuzi ya kuifunga. Lakini kama ripoti itatuelekeza kwamba mradi unamanufaa tutekeleza moja, mbili, tatu, basi serikali tutatekeleza hayo.
Mimi nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi watupatie hiyo nafasi kama walivyotoa *suggestion* Mhe. Omar Ali Shehe na mimi niko tayari kuitekeleza hiyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa busara ambazo zimetumika na hasa kwa heshima ya Mwenyekiti wangu wa PAC busara zake mimi nakubaliana nazokwamba tunaweza tukazipitisha hizi lakini zikazuiliwa na utafiti ukafanyika baada ya kupata hiyo ripoti ndio tukakubaliana kwamba sasa sikatumike au laaa. Mimi nakubaliana katika hilo. Vyenginevyo msimamo wangu ubakie pale pale kwamba tusizipitishe moja kwa moja. Lakini kama tunazipitishwa ni kwamba zizuiliwe kwamba zisiendi kule mpaka wamalize utafiti wao, uchungu wao na kila kitu chao, ndio ndipo tupewe taarifa ya mradi ule kwenye Baraza lako hili halafu ndio tuseme kwamba sasa ziendele kwenda kuzitumia au laa.

Mhe. Mwenyekiti: Maamuzi tunayotaka kupitisha hapa tunapitisha fedha lakini fedha hii isitumike mpaka baada ya utafiti huo na taarifa yeke kuja hapa tukaipokea. (*Makofi*)

Kifungu 0201	Utawala Unguja	300,000,000
Jumla ya Fungu		**300,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 – CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201	Idara ya Vyuo vya Mafunzo	400,000,000
Jumla ya Fungu		**400,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 – KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201 Utawala	200,000,000
Jumla ya Fungu	**200,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 34 – KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 0201 Utawala Unguja	100,000,000
Jumla ya Fungu	**100,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(*Baraza lilirudia)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nawashukuru sana wajumbe kwa changamoto kubwa sana. Sasa Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi, imejadili na kupitisha Makadirio ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mabadiliko yake, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ni dhahir kwamba kiafya haikubaliki, kuja saa 11, ambapo pana muda wa sasa moja tu, ambao ningewambia basi tubaki humu humu tuendelee. Kwa hivyo nafikiri ni busara shughuli iliyobaki ifanyike kesho. Kwa hivyo tumuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, atutolee utaratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda umekuwa mkubwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walikuwa na Bajeti ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais kutokea saa 6 mpaka sasa. Na kwa kuwa leo jioni ilikuwa Mhe. Waziri wa Nchi Anayeshughulikia Utumishi na Utawala Bora aweze kusoma bajeti yake. Lakini hakika Mheshimiwa kutokana na afya zetu kama binaadamu kwa vyovyote vile Mhe. Waziri wa Nchi, atakuwa naye amechoka na wajumbe wamechoka. Kwa hivyo naliomba Baraza lako tukufu liahirishe kikao chake hichi mpaka keso asubuhi, saa 3:00.
Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nimeombwa niwatangazie Wawakilishi wa upande wa CCM kama ule mkutano wa CCM uliokuwa ufanyike mara baada ya kuahirisha kikao saa 7:00 hautokuwepo tena kwa leo. Badala yake utakuwa kesho panapomajaaliwa pahala pale pale mara baada ya kuahirisha shughuli zetu pale mchana saa 7:00.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwashukuru sana, maana niliogopa Mhe. Muasisi aliposema kwamba sasa tuelekee kuvunja GNU, duuu hiyo kazi kubwa kweli. Maana kuwakusanya wananchi ili kutoa maoni yao tuendelee na GNU au laaa, heee! Hiyo kazi kubwa nap engine tungekuja kuambiwa tunafanya

matumizi yasiyokuwa na msingi. Lakini haraka nilielekeza kwamba hilo jambo kwa mjibu wa taratibu tena za Kikatiba inabidi turudi kwa wananchi waliosema utaratibu huu uwepo.

Nashukuru kwamba tumefahamiana juu ya hilo na kwa kweli tunapaswa kuwa na busara sana hasa juu ya mambo yaliyowekewa utaratibu kwa mujibu wa sheria, hasa katiba. Itakuja kuwa ni aibu kubwa kufika pahala chombo chetu hichi kiwe ndio cha kwanza kuvunja katiba, itakuwa si jambo la busara hata kidogo. Kwa hiyo tuwe makini sana tunapofanya shughuli zetu tuelewe kwamba tunakwenda kwa mujibu wa taratibu za katiba na sheria zinazoongoza. Mambo yaliyopo katika shughuli zetu ili tusije tukafikia pahala tukawa chombo hichi ndicho kinacho wa- *miss lead* wananchi wa kuelekea kwahala ambako hatutegemei tuelekee.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru tena zaidi Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na Mawaziri kwa busara kubwa hasa juu ya masuala haya ya vitambulisho. Mimi nilikuwa napata tabu sana kufika pahala kwamba tuunge Kamati iteule juu ya suala la vitambulisho. Kwa sababu hili suala ni kubwa mno, utapoangalia kwa undani mtakubaliana nami kwamba katika jambo ambalo lina utashi mkubwa mno wa kisiasa ni hili. Kuja kuipeleka Kamati Teule ikakumbana na vikwazo vya kisiasa wakati jambo lenyewe linahusu utekelezaji. Chombo cha kutekeleza kipo, sheria zinazoongoza jambo hilo zipo vyombo vya kushauriana na kusaidiana vipo ikiwa ni pamoja na Mikoa, Wilaya, Masheha, wapo na vyombo hivyo vyote vinapaswa kufata utaratibu wa sheria. Kwa kweli hilo jambo nilikuwa naliogopa sana. Linaweza kutupeleka pia kuonekana kwamba tunatumia fedha isivyoelekea.

Lakini zaidi ya hivyo kwamba chombo hichi cha tasisi ya vitambulisho inazitambulisho vingi ambavyo vimekaa, tumeambiwa laki moja elfu kumi na mbili (112,000) hii nayo ni kazi ya utekelezaji, kutuma Kamati ya Baraza ikafanye kazi hiyo hapana. Utendaji itakuwa tunauingilia na tutaonekana kama haikufanikiwa basi chombo hichi nacho kimekwenda kuingilia kwenye shughuli ambayo ilikuwa ifanywe na wandaji wanaohusika. Mimi nielekeze tu kwamba kwa kuwa taasisi hii ya vitambulisho ipo, Viongozi wa Mkoa na Wilaya wapo, Masheha wapo na Waziri yupo, basi kazi hii ifanyike ili vitambulisho hivi ambavyo vimeshafanyiwa kazi, imeshatumika pesa kuvitoa viwafike wenyewe kama wapo.

Kwa sababu nayo itakuja kuwa ni usumbufu katika maelezo kuna baadhi ya wananchi wanaona ni usumbufu wa kwenda na kurudi. Sasa tusinune kiasi hicho. Tukiangalia mambo ya msingi yanayohitajika kwenye kitambulisho hichi kwa kweli kuna haki nyingi ambazo wananchi wetu wanaweza wakakosa, kwa kukosa kitambulisho cha Ukaazi. Taasisi yetu imeshavitoa lakini sasa ikawa vimekaa havitumiki,kwa kweli hilo itakuwa sio jambo la msingi.

Vyombo vinavyohusika kwa mashirikiano ya pamoja tuone jambo hii linafikia pahala linakwenda vizuri. Lisituletee misuguano ya kisiasa na mivutano hatamaye ikatuvunjia amani yetu iliyopo. Kwa sababu masuala yanayohusu hatimaye uchaguzi katika mazingira ya aina kama haya yanaweza yakatufikisha pahala pasipo pazuri, pasipo elekea. Sisi hapa ndio viongozi tukubaliane kwa pamoja kwamba vyombo vinavyohusika vifanye kazi yao kutekeleza juu ya vitambulisho vilivyotengenezwa. Lakini na wale ambao wanakubalika kisheria kupata basi na wao wapatiwe vitambulisho kama sheria inavyoelekeza.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni tena kwa kazi nzuri mnayoifanya na kwa mashirikiano makubwa. Baada ya hayo basi tukubaliane tuakhirishe shughuli zetu hizi hadi kesho tarehe 4/7/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 10: 01 Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 4/7/2012 saa 3:00 asubuhi)